SUPA JACKPOT
TZS. 1,062,078,169
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 12

**ASKOFU** awakemea wanaotaka utajiri kwa njia ya mkato


Nipashe
TESA
Jumanne Januari 3, 2023
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Mapinduzi ya elimu kuboresha usomaji yaanza kwa kasi Pwani
Ukurasa 14

Hili lisipuuzwe mwaka huu, linaua wanafunzi, mabinti
Ukurasa 15

SAYANSI
NA MWANDISHI WETU

Kero ya kila mwaka hata 2023 Watanzania wametinga nayo

wako wa ndugu yako atakwenda na kukutana na foleni na msongamano. Kadhalika usipokwenda hospitalini basi mtoto wako au ndugu yako yeyote yule atafuata matibabu na kupata adha hiyo iwe ni kumwona daktari, maabara, chumba cha x-ray na kurudisha matokeo ya vipimo kwa daktari.

Ukisema unaamua kununua na kutumia gari binafsi ili kuepuka msongamano kwenye daladala au basi la umma, wazazi wako jamaa zako watapanda daladala au mwendokasi na kupata kadhia hiyo ya foleni na msongamano. Wakikosa hao basi mjomba au ndugu yako mwingine atapata kadhia hiyo ya foleni na msongamano. Kwa maneno mengine foleni na msongamano lazima inagusa jamii nzima ya waliokuwa vijijini na mijini na kwa kuwa huduma wanazozifuatilia zina watu wengi.

MADHARA YA USUMBUFU
Kwa sasa kuna madhara mengi yatokanayo na misongamano hiyo katika maeneo mbalimbali ya kupata huduma ikiwa ni pamoja

UKURASA 13


Jumanne Januari 3, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581179
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Shule yatoza 'motisha kwa walimu', tuisheni

**MKUU** wa Shule akana, wazazi watumiwa ankara...
*Endelea uk. 2*


JINA LA MWANAFUNZI ____ SHULE YA SEKONDARI ASHIRA
MADENI YA NYUMA: ____ MWAKA ____

KIDATO CHA TANO

MUHULA I
Ada
Kukodi godoro 1000/=
Mpishi 2000/=
Ulinzi 2000/=
Taaluma 2000/=
Ream
Kitambulisho 500/=
Tahadhari 500/=
Matibabu binafsi 1000/=
Ukarabati wa samani 1500/=
Jumla 10500/=

MUHULA WA II
Ujenzi wa uzio 10000/=
Ada —
Motisha kwa watumishi 2500/=
Mahafali 1000/=
Ream Alet ream
Jumla 13500/=

KIDATO CHA SITA

MUHULA I
Ada
Kukodi godoro
Mpishi
Ulinzi
Taaluma
Ream
Tahadhari
Matibabu
Ada Mitihani:
- Taifa (NECTA)
- Utamirifu Mkoa (MOCK)
- Pre-Mock
- Pre – NECTA
- Photo entry NECTA
Jum'a

MUHULA WA II
Ada
Mahafali
Mafunzo rekebishi
Ream
Jumla

Saini
E. Abdallah
MKUU WA SHULE
ASHIRA GIRLS' SECONDARY SCHOOL
MOSHI

Ankara ya malipo iliyotumwa kwa mmoja wa wazazi kutoka Shule ya Sekondari ya Wasichana Ashira

# TRA yajivunia makusanyo ya kodi kwa 99%

UKURASA 7



# Mwili wa Papa Benedict XVI kuagwa siku tatu

UKURASA 4

Mwili wa aliyekuwa Papa wa Kanisa Katoliki, Benedict XVI (95) ukiwa kwenye eneo la wazi katika Kanisa la Mater Ecclesiae, mahali alipokuwa akiishi tangu alipostaafu mwaka 2013. **PICHA: MTANDAO**

**MICHEZO** **SIMBA BILA CHAMA MAPINDUZI CUP** UK. 32 **KATUNI** UK. 6

WAKATI MARUFUKU ADA, TUISHENI...

# Shule yatoza 'motisha kwa walimu', darasa la likizo

● Mkuu wa Shule akana, wazazi watumiwa ankara

**Na Mwandishi Wetu**



Mwonekano wa shule ya Ashira

NI hali inayoibua mkanganyiko wa tafsiri kati ya watendaji, uongozi wa shule dhidi ya watendwa, wazazi wa wanafunzi kuhusu malipo ya kipekee yenye sura tatu; motisha kwa watumishi, malipo kwa ajili ya madarasa ya likizo na gharama za kujenga uzio.

Utata huo ambao baadhi ya wazazi wa watoto wanaosoma katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Ashira mkoani Kilimanjaro, wamelazimika kujikusanya na kuzifikia ofisi za Nipashe kuwasilisha madai hayo, umelifanya gazeti hili kusaka usahihi wa dai hilo, ikipatiwa jibu la 'ni hiari ya wazazi'.

Mkuu wa Shule hiyo, Elizabeth Abdallah, akizungumza na Nipashe, alikiri kuwapo katazo la michango kisheria, akiwarejeshea wazazi hao kwamba waliamua katika mkutano wao hivi karibuni.

"Mimi sihusiki kama Mkuu wa Shule, kwa sababu siruhusiwi kukusanya michango yoyote kwa mujibu wa sheria, taratibu na miongozo ingawa wazazi walikubaliana kuhakikisha wanamaliza uzio ili watoto waweze kukaa sehemu salama ukiangalia ni wanafunzi wa kike," alisema.

Mkuu wa Shule alifafanua kwamba ni pendekezo la wazazi kuwapa walimu motisha ili watoto wabaki shuleni kipindi cha likizo fupi pamoja na kujenga uzio kwa ajili ya usalama wa watoto wao.

Nipashe ilipomtafuta Mwenyekiti wa Wazazi wa Shule hiyo, Michael Magaya, alisema kuwa walilazimika kuweka michango ya Sh. 55,000 kama motisha kwa walimu ili wabaki na wanafunzi shuleni kwenye likizo fupi za kuelekea kwenye kipindi cha mitihani.

"Matokeo ya mwaka jana hakukuwa na zero (daraja sifuri) wala daraja la nne, hivyo tumeiga mbinu ya watangulizi wetu ili kuhakikisha watoto wanafanya vizuri zaidi.

"Na kuhusu uzio, sisi wazazi tulikubaliana kila mtoto anapoingia kidato cha tano kuchangia Sh. 100,000 kwa ajili ujengaji wa uzio utakaosaidia kuwapo usalama wa kutosha kwa watoto wa kike.

"Hii imesababisha kila mtoto kuchangia Sh. 100,000. Shule yetu haina kidato cha kwanza hadi cha nne. Wanafunzi wa kidato cha tano na sita ni zaidi ya 700," Magaya alifafanua.

Nipashe ilipomtafuta Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu kuzungumzia suala hilo, alisema kuwa ikiwa wazazi wamekaa kikao na kuona kuna umuhimu wa kuchangia kwa ajili ya maendeleo ya shule na ustawi wa wanafunzi na wakapata kibali hicho, michango hiyo ni halali.

"Sisi hatutapinga uamuzi wa wazazi ikiwa wamekubaliana katika kikao, kwani wao wana sababu za msingi kwa maendeleo ya shule na watoto wao," alisema Babu.

### UTATA WA TARATIBU

Wakati serikali imefuta ada ya Sh. 70,000 kila mwaka kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita, mwanafunzi anayesoma katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Ashira anatakiwa kulipa Sh. 295,000.

Kutokana na kutoza michango hiyo, shule hiyo yenye zaidi ya wanafunzi 700, inakusanya zaidi ya Sh. milioni 206.5 kwa mwaka.

Kwa mujibu wa ankara za malipo walizotumiwa wazazi na Mkuu wa Shule hiyo, Elizabeth, kila mwanafunzi wa kidato cha tano anatakiwa kulipa Sh. 100,000 kwa ajili ya ujenzi wa uzio, Sh. 25,000 kwa ajili ya motisha kwa watumishi, Sh. 55,000 kwa ajili ya malipo kwa walimu wakati wa likizo na Sh. 10,000 kwa ajili ya mahafali.

Malipo mengine yanayohitajika shuleni huko ni kukodi godoro Sh. 10,000, mpishi Sh. 20,000, ulinzi Sh. 20,000, taaluma Sh. 20,000, kitambulisho Sh. 5,000, tahadhari Sh. 5,000, matibabu Sh. 10,000 na ukarabati wa samani Sh. 15,000.

Vilevile, baadhi ya wazazi waliofika kwenye ofisi za Nipashe walikuwa na risiti za benki za malipo ya ada ya shule iliyofutwa na serikali.

Wakati hayo yakiendelea shuleni Ashira, mwishoni mwa mwaka juzi, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknoloajia kupitia kwa aliyekuwa Waziri wake, Prof. Joyce Ndalichako, ilitoa mwongozo wa kupiga marufuku wanafunzi kubakishwa shuleni wakati wa likizo.

Katika kudhibiti hali hiyo, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) mwanzoni mwa mwaka jana ilitoa tamkoa la kukemea tabia ya kulazimisha wanafunzi kubaki shuleni wakati wa masomo, akiagiza mihula ya masomo iheshimiwe.

"Watoto wakifunga shule waende nyumbani, kama kuna hitaji la kufanya masomo ya ziada kipatikane kibali kutoka kwa Katibu Tawala wa Mkoa kufanya hivyo," Ummy Mwalimu, aliyekuwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI, alisema.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 inaelekeza kuwapo siku 194 za masomo kwa mwaka, hivyo kulazimisha wanafunzi kubaki shuleni wakati wa likizo ni kwenda kinyume cha sera hii kutokana na kuzalisha siku za ziada za masomo shuleni.

Novemba 24, 2021 Chama cha Madaktari Tanzania (MAT) kilisema kimeanza utafiti kubaini athari wanazozipata wanafunzi ambao hukaa zaidi ya saa 12 shuleni kwa siku na wanaobeba mabegi mazito.

### JICHO KISHERIA

Wakati Shule ya Sekondari ya Wasichana Ashira ikichangisha kila mwanafunzi Sh. 55,000 kwa ajili ya kuwalipa walimu ili wabaki na wanafunzi wakati wa likizo, Sheria ya Kazi na Uhusiano Kazini inazuia mwajiri kumlipa mwajiriwa ili abaki kazini wakati wa likizo.

Hali kadhalika, Kifungu cha 7(3) cha Sheria ya Mapato ya Mwaka 2014, kiliondoa posho za nyumba, usafiri, madaraka, kufanya kazi kwa saa za ziada, kufanya kazi katika mazingira magumu na honoraria kwa watumishi wa serikali au taasisi ambayo bajeti yake hulipwa yote au kwa kiwango kikubwa na ruzuku ya serikali.

Kwa mantiki hiyo, walimu wa Shule ya Sekondari ya Wasichana Ashira kulipwa fedha kwa kufanya kazi kwa saa za ziada kunafanyika kinyume cha sheria.

### MIONGOZO SERIKALINI

Wakati wa kuahirisha Mkutano wa Bunge la Bajeti Juni mwaka jana, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, pamoja na mambo mengine, alitoa ufafanuzi kuhusu ugharamiaji wa elimu unavyotekelezwa na serikali kupitia Mpango wa Utoaji Elimumsingi Bila Malipo.

Alisema kuwa serikali kupitia Waraka wa Elimu Na. 5 wa mwaka 2015 na Waraka wa Elimu Na. 6 wa mwaka 2015, imetoa maelekezo bayana kuhusu utekelezaji wa elimumsingi bila ada.

Waziri Mkuu alisema maelekezo hayo ni pamoja na matumizi ya fedha za utawala ambazo hutolewa Hazina na kupelekwa moja kwa moja katika akaunti za shule za msingi na sekondari nchini kwa ajili ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia, uendeshaji wa mitihani ya ndani, utawala na ukarabati.

Wakati kukiwa na mwongozo huo wa kitaifa, Shule ya Sekondari ya Wasichana Ashira kila mwanafunzi anatakiwa kuchangia Sh. 15,000 kwa ajili ya ukarabati.

Wakati wa mkutano tajwa wa Bunge, Naibu Spika wa Bunge, Mussa Zungu alisema kuna kero kubwa ya michango shuleni inayowaumiza wananchi, akiitaka Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuchukua hatua madhubuti.

Zungu alisema wananchi wanabebeshwa mzigo wa michango ambayo inapaswa kugharamiwa na halmashauri zenyewe.

"Dodoma wameonyesha njia, ninapongeza sana Halmashauria ya Dodoma, gharama za umeme, ulinzi zinafanywa na halmashauri," alisema.

"Hii michango na Waziri wa TAMISEMI uko hapa, hatuoni sababu kwanini halmashauri zisigharamie ulinzi, umeme. Kwanini wazazi wachangie ulinzi na umeme? Mnaumiza wazazi sana kwa michango kama hii," alisisitiza.

Zungu alisema serikali imeondoa ada lakini bado kuna michango ya ziada inawasumbua wazazi, hivyo akamtaka Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - TAMISEMI kuchukua hatua za haraka kuhusu suala hilo.

Juni 25 mwaka jana, Nipashe ilichapisha ripoti maalum kuhusu kero ya michango kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha tano mwaka huu wa masomo katika shule mbalimbali za Tanzania Bara.

Michango inayolalamikiwa inajumuisha gharama za ulinzi wa shule, wapishi wa shule, fedha za matibabu, tahadhari, ununuzi wa vitabu, michezo, gharama za mitihani na taaluma, kukodi godoro na ununuzi wa vifaa vingine vya shuleni.

Hayo yanafanyika katika kipindi ambacho serikali imefuta ada kwa kidato cha tano na cha sita ili kuwapunguzia gharama wanafunzi.

Kwa mujibu wa Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kwa sasa wanafunzi wa kidato cha tano ni takribani 90,825 na kidato cha sita ni 56,880 na mahitaji ya fedha ni Sh. bilioni 10.339.

"Ili kuwapunguzia gharama watoto hawa, kama Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan alivyoielekeza wizara, ninapendekeza kufuta ada kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

"Kwa hatua hii, elimu bila ada ni kuanzia shule za msingi mpaka kidato cha sita. Serikali itajipanga kuangalia namna ya kusaidia vyuo vya kati kadri hali ya uchumi itakavyotengemaa," Dk. Mwigulu alisema bungeni mwezi Juni mwaka jana alipowasilisha kwa mara ya kwanza pendekezo la kufuta ada ya kidato cha tano na sita.

Alisema Rais Samia ameguswa na watoto kukatisha masomo kutokana na sababu mbalimbali, miongoni mwake zikiwa umaskini wa kipato kwenye familia, mimba za utotoni, mwamko duni wa elimu kwa baadhi ya jamii, utoro na wasioendelea kwa mujibu wa sheria (ufaulu duni).

# DC atoa siku 10 wakulima na wafugaji kuondoka hifadhini

**Na Idda Mushi,** KILOMBERO

MKUU wa Wilaya ya Kilombero, Hanji Godigodi, ametoa siku 10 kuanzia Desemba 31, mwaka jana, kwa wafugaji, wakulima na wavuvi waliovamia eneo la kitalu cha uwindaji cha Kilombero Northern Safari kilichoko Halmashauri ya Mlimba.

Kitalu hicho kimo ndani ya Bonde la Mto Kilombero ambalo maji yake yanategemewa kwa kiasi kikubwa kwenye mradi wa kuzalisha umeme wa maji wa Julius Nyerere.

Kukamilika kwa mradi huo wa umeme kunatarajiwa kuzalisha megawati 2,115 ambazo zitasaidia kuondokana na adha ya uhaba wa nishati ya umeme.

Hata hivyo, uharibifu unaoendelea kwenye vyanzo vya maji vinavyopeleka maji Mto Rufiji ambao maji yake yanahitajika ili kujaza Bwawa la Nyerere, unatishia matarajio hayo.

Agizo hilo la Mkuu wa Wilaya limekuja baada ya Kamati yake ya Ulinzi na Usalama kufanya ziara ya kushtukiza kwenye kitalu cha uwindaji cha mwekezaji Kilombero Northern Safari ambacho kipo ndani ya kitalu cha Mlimba Northern na kujionea uharibifu mkubwa uliofanywa na wakulima, wafugaji na wavuvi.

Jamii hiyo imekata miti na kuanzisha mashamba makubwa ya mahindi na ufuta huku wengine wakiweka makazi ya kudumu bila ya kuhofia wanyama wakali walioko kwenye maeneo hayo.

"Serikali haiwezi kuvumilia kuona wananchi wachache wanahujumu uchumi wa nchi, uharibifu unaofanywa kwenye vyanzo vya maji unaathiri moja kwa moja uwekezaji mkubwa wa zaidi ya Sh. trilioni 6.5 uliofanywa na serikali katika mradi wa kufua umeme wa Julius Nyerere huko Rufiji mkoani Pwani," alisema.

Alisema ofisi yake ipo tayari kusafirisha wafugaji wote wavamizi na wakulima waliovamia eneo hilo ili kuhakikisha mito yote iliyoko kwenye Bonde la Kilombero inarudi kwenye hali yake ya kawaida na maji ya kutosha yanakwenda kwenye Bwawa la Nyerere.

Godigodi alisema kuwa baada ya muda uliotolewa kutoka kwa hiari kumalizika, serikali haitamwonea huruma mwananchi yeyote atakayekaidi kwa kuwa Rais alishatoa tamko la kulinda vyanzo maji na kuhakikisha ulinzi wa vyanzo vya maji vinavyopeleka maji Mto Rufiji.

Kiongozi wa doria kutoka Kitalu cha Uwindaji cha Kilombero Northern Safari, James Bebe, alisema kuwa kutokana



na uharibifu mkubwa wa mazingira unaofanywa, wanyamapori wamekosa maeneo ya kuishi na kutoa mwanya kwa majangili kutekeleza uhalifu kwa njia rahisi zaidi.

Alilishukuru Jeshi la Polisi kupitia Kituo cha Polisi Mlimba, Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (TAWA) na Halmashauri ya Wilaya ya Mlimba kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa katika kuhakikisha wavamizi na majangili wanakwisha kwenye kitalu hicho.

Awali akitoa elimu kwa wananchi wa Kijiji cha Idundembo kuhusu makosa mbalimbali na hatua zitakazochukuliwa kwa wahalifu, Mkuu wa Kituo cha Polisi Mlimba, Donati Mhina aliwataka wakazi wa vijiji vinavyozunguka Kitalu cha Mlimba Northern kuacha tabia ya kulima kwenye maeneo hayo na hata kuingiza mifugo kwa kuwa kufanya hivyo ni kosa kisheria.

Baadhi ya wananchi wanaoishi pembezoni mwa kitalu hicho, walisema chanzo cha uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji ni viongozi wa vijiji na kata ambao wamekuwa wakiwakaribisha wageni na kuwaonyesha maeneo ambayo yamehifadhiwa na kuchukua fedha kwao.

"Viongozi wa vitongoji wamekuwa wakichukua fedha za wakulima na wafugaji jamii ya Wasukuma na kuwapeleka kuwaonyesha maeneo kwenye kitalu cha uwindaji cha Mlimba Northern, alisema Shukrani Dodonda, mkazi wa Kijiji cha Idundembo.

Wananchi hao pia walibainisha kuwa baadhi ya viongozi wa vitongoji, vijiji, kata, watendaji pamoja na wa chama wanaogombea nafasi za kuchaguliwa, wakiwamo madiwani, wamekuwa wakipiga kampeni kupitia kugawa mashamba huko kwenye vyanzo vya maji.

## CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA SERIKALI ZA MITAA TANZANIA (TALGWU)

## TANGAZO LA UCHAGUZI WA NAFASI YA NAIBU KATIBU MKUU WA CHAMA

Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (TALGWU) kinatarajia kufanya Kikao cha Baraza Kuu la Taifa ambapo pamoja na mambo mengine kwa kuzingatia Ibara ya 5.16.3 (xi)(a) ya Katiba ya Chama toleo la 2016 Kikao hicho kitafanya Uchaguzi wa kujaza nafasi ya Naibu Katibu Mkuu wa Chama.

Uchaguzi unatarajiwa kufanyika tarehe 17 Januari 2023 katika ukumbi wa Mikutano wa Hoteli ya Royal Village Jijini Dodoma kuanzia saa 03:00 Asubuhi.

Wagombea wote mnahimizwa kufika mapema katika eneo la ukumbi utakapofanyika uchaguzi. Aidha kwa wagombea ambao sio Wajumbe wa Kikao cha Baraza Kuu watahudhuria uchaguzi huo kwa kujigharamia wenyewe.

**Imetolewa na**

.................................

**Rashid M. Mtima**

**KATIBU MKUU – TALGWU TAIFA**

217213502






Mkuu wa Wilaya ya Hanang', Janeth Mayanja (katikati), akiwa amevalia vazi la kitamaduni la Kidatoga sambamba na Wanakidatoga katika sherehe za kuukaribisha mwaka mpya mwishoni mwa wiki. **PICHA: GIFT THADEY**

# Mwili wa Papa Benedict kuagwa siku tatu

**Na Mwandishi Wetu**

MWILI wa aliyekuwa kiongozi wa Kanisa Katoliki duniani, Papa Benedict XVI, umeanza kuagwa jana na unatarajiwa kukaa katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Petro, Vatican kwa siku tatu kabla ya maziko kutoa fursa kwa waamini na watu wengine kuuaga.

Kwa mujibu wa taarifa zilizowekwa Deutsche Welle (DW) na Vatican News, mwili wa kiongozi huyo umehifadhiwa katika Monasteri ya mama wa kanisa, ukiwa na mavazi ya kanisa badala ya jeneza kama ilivyozoeleka.

Kiongozi huyo aliyekuwa raia wa Ujerumani, alifariki Jumamosi akiwa na umri wa miaka 95, aliliongoza Kanisa Katoliki kwa muda wa miaka minane kabla ya kuwa Papa wa kwanza katika kipindi cha karne sita kujiuzulu mwaka 2013.

Mrithi wake Papa Francis ataongoza ibada ya mazishi Alhamisi katika uwanja mkuu wa Mtakatifu Peter, kabla ya kuzikwa kwenye makaburi yaliyoko katika Kanisa la Mtakatifu Petro.

Benedict alifariki katika nyumba ya watawa ya Mater Ecclesiae ndani ya bustani ya Vatican, ambayo yalikuwa makazi yake kwa muongo mmoja uliopita.

Kiongozi huyo ambaye jina lake halisi ni Joseph Aloisius Ratzinger, alipendwa na wengi, lakini alikosolewa na wengine, alikuwa Mjerumani wa kwanza kuwa Papa baada ya miaka 500 iliyopita.

Hatua yake ya kujiuzulu Februari 28, 2013 ilikuwa ya kihistoria akiwa kiongozi aliyesisitiza umuhimu wa hitaji la kiroho na wa kanisa katika ulimwengu wa kisasa ulioelimika.

Baada ya Makardinali kumchagua Mwadhama Joseph Kardinali Ratzinger, aliyekuwa na umri wa miaka 78 kuchukua nafasi ya Papa John Paul II kuliongoza Kanisa Katoliki, kardinali huyo alitoka kwenye kibaraza cha Kanisa Kuu la Mtakatifu Peter mjini Roma Aprili 19, 2005 na kusema:

"Makardinali wamenichagua mimi, mfanyakazi wa kawaida, mnyenyekevu katika shamba la mizabibu la Bwana."

Papa Benedict XVI alikuwa mhafidhina, ambaye hata hivyo aliwashangaza wafuasi na wapinzani, hasa kwa sababu alikuwa mcha Mungu na alikuwa na shauku kubwa ya kujifunza.

Alisisitiza umuhimu wa huduma ya kichungaji, alihisi kufadhaishwa na mizozo mingi iliyolikumba Kanisa Katoliki wakati wa uongozi wake.

Alizaliwa Aprili 16, 1927 katika Jimbo la Bavaria, ambako baba yake alikuwa polisi, mwishoni mwa miaka ya 1950, Ratzinger aliheshimika kama Profesa wa Theolojia.

Alipewa daraja la upadri mwaka 1951, sawa na kaka yake mkubwa George. Baada ya kuwa na uhusiano wa karibu na Askofu Mkuu wa Cologne, Josef Richard Frings, Ratzinger alihudhuria Baraza la Pili la Vatican kuanzia mwaka 1962 hadi 1965, na alihutubia kuhusu uhusiano kati ya Kanisa Katoliki na ulimwengu wa sasa.

Mwaka 1997 aliteuliwa kuwa Askofu Mkuu wa Munich na Freising na muda mfupi baadaye kuwa Kardinali. Miaka minne baadaye, Papa John Paul II alimpeleka Roma, ambako aliteuliwa kuwa Mkuu wa Shirika la Kipapa la Mafundisho ya Imani. Wakatoliki wa Ujerumani walifurahi wakati Ratzinger alipochaguliwa kuwa Papa mwaka 2005.

Wengine walisema papa huyo alikuwa mzee sana kuliongoza kanisa, huku wengine wakiwa na wasiwasi kwamba uhafidhina wake unaweza kumfanya ashindwe kushinikiza mageuzi katika kanisa.

Kwa mujibu wa Vatican News, kwa mtazamo wa kisiasa, uongozi wake wa miaka minane ulikuwa wakati wa mpito, bado Papa Benedict XVI alitaka kuweka alama yake. Wakati wa kipindi chake cha kukalia kiti cha Mtakatifu Peter, pia aliwaweka wakfu zaidi ya nusu ya makardinali ambao baadaye Machi, 2013 walimchagua mrithi wake Papa Francis.

Papa Benedict hakuchoka kusisitiza mazungumzo kuhusu uhusiano kati ya dini na jamii ya kisasa, na mara nyingi alisisitiza imani yake kwamba Kanisa Katoliki linapaswa kuongoza Jumuiya ya Wakristo jambo lililoleta mvutano wa kiuhusiano na dini nyingine.

Uongozi wa Papa Benedict uligubikwa na ufichuzi kuhusu miongo kadhaa ya unyanyasaji wa kingono kwa watoto wadogo, ambao ulifanywa na makasisi wa Kanisa Katoliki kwenye nchi kama Ireland, Marekani, Australia, Ubelgiji na hata Ujerumani.

Wakosoaji baadaye walilishutumu kanisa kwa kukwepa kuchukua hatua stahiki kwa wahusika na badala yake liliwahamisha wahusika hao na kuficha uhalifu walioufanya, na alitaka kuliangazia suala hilo la kukosekana haki kwa waathirika.

"Ninasikitishwa na mateso yaliyosababishwa na unyanyasaji wa watoto hasa ndani ya kanisa na wahudumu wake zaidi ya yote ninaelezea masikitiko yangu makubwa kwa waathirika wasio na hatia wa uhalifu huu usioelezeka, pamoja na matumaini yangu kwamba kwa uwezo wa Neema ya Kristo, kujitoa kwake au upatanisho wake utaleta uponyaji wa ndani na amani katika maisha yao," alifafanua Benedict XVI.

**MANENO YA MWISHO**

Kwa mujibu wa wasaidizi wake, kabla ya kufikwa na mauti kwa sauti ya chini kwa lugha ya Kitaliano alisema: 'Bwana nakupenda".

**Chanzo: Vatican News, DW**

## Rais Samia kukutana na viongozi vyama vya siasa

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS Samia Suluhu Hassan leo anatarajiwa kukutana na viongozi wa vyama vya siasa nchini kwa ajili ya kujadili masuala mbalimbali kwa mustakabali wa nchi katika kuendeleza shughuli zao.

Kikao hicho ni cha kwanza mwaka huu kuwaleta pamoja viongozi wa vyama mbalimbali vya siasa huku kukiwa na mwendelezo wa maridhiano baina ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) katika kujenga nchi.

Hiki ni kikao cha kwanza kuwakutanisha viongozi wa vyama vyote kwa pamoja kwani mwaka jana walikutana kwa makundi tofauti kwa kundi la vyama vyote ambalo CHADEMA waliweka msimamo wa kutokushiriki.

Safari hii CHADEMA wanashiriki, ikiwa ni siku chache baada ya Mwenyekiti wa chama hicho, Freeman Mbowe kukutana na Rais Samia na Makamu Mwenyekiti wa CCM Taifa, Abdulrahman Kinana Ikulu jijini Dar es Salaam.

Mwaka jana Rais alikutana na viongozi wa vyama vya siasa na kujadili mambo mbalimbali ikiwamo mikutano ya hadhara, akisisitiza yuko tayari kusikiliza, kuvumilia na kusamehe kwa yote yatakayoelekezwa ingawa anataka vifanye kazi kwa kuzingatia sheria na taratibu za nchi.

Wakati mkutano huo ukifanyika, Mbowe alikuwa gerezani akikabiliwa na kesi ya ugaidi na hivyo mkutano wa leo utakuwa wa kwanza kwake na chama chake kuhudhuria tangu kumalizika kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020 ulioacha makovu ya kisiasa.

Mkutano huo ulikuwa wa kwanza kwa Rais Samia ikiwa ni miezi saba tangu aingie madarakani, akisisitiza kusamehe na kuzika tofauti zilizojitokeza kutokana na uchanga wa demokrasia na kuangalia namna bora ya kushirikiana kuendesha nchi.

Katika mkutano huo, Kiongozi wa ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, aliomba kuachiwa kwa Mbowe ili washirikiane kufanya siasa zenye tija kwa maslahi mapana ya nchi.

Siku chache baadaye, Mbowe aliachiwa na kwenda Ikulu ambako alikutana na Rais Samia na kujadili masuala mbalimbali ya kisiasa na baadaye kiongozi huyo wa upinzani aliwaeleza Watanzania kile walichokubaliana.

"Tumekubaliana njia nzuri ya kuwa na maridhiano, ni wakati kuwa na haki. Tumepitia madhila mengi, hakuna haja ya kuyarudia mara kwa mara badala yake tunapaswa kusonga mbele na kuwa na siasa safi na kuiunga mkono serikali. Tunatumaini kuwa serikali itatuunga mkono katika shughuli zetu ili kila mtu afurahi," alisema.

Baadaye kilifanyika kikao cha kwanza cha maridhiano Mei 20 mwaka jana, kikihudhuriwa na viongozi wa upande wa CHADEMA na CCM.

# Ewura kudhibiti bei, ujazo gesi majumbani kulinda mazingira 2023

**Na Mwandishi Wetu**

MWAKA 2022 umefikia ukingoni. Sasa tumeingia mwaka mpya wa 2023. Taasisi nyingi za umma na binafsi zinahesabu mafanikio yake kwa mwaka uliomalizika.

Moja ya taasisi za umma ni Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) ambayo ina mengi ya kujivunia iliyofanya katika sekta za nishati na maji ambazo imepewa mamlaka ya kisheria kuyadhibiti.

Meneja Mawasiliano kwa Umma EWURA, Titus Kaguo, anasema moja ya maeneo yaliyofanikiwa kuyasimamia na kuyadhibiti kwa mwaka 2022 ni la bei na viwango vya tozo na ujazo wa gesi ya majumbani (LPG).

Kaguo anasema, EWURA imepewa mamlaka ya kisheria na kisera, kufanya mapitio ya viwango, bei, na tozo za gesi ya majumbani (LPG) yakiwasilishwa na mwombaji au wakiona ni muhimu kama ilivyoainishwa katika ibara ya 17 Sheria ya EWURA, Sura ya 414. Utaratibu wa maombi ya viwango vya bei za nishati hiyo umeainishwa katika mwongozo wa bei za umeme na gesi asilia, 2017.

Anasema uhitaji wa kudhibiti uchumi katika gesi asilia unachagizwa na ukweli kuwa watoa huduma wanaohodhi shughuli za gesi asilia wakiachwa bila kudhibitiwa, basi wanaweza kutumia vibaya uwezo wao, na kusababisha utoaji wa huduma kuzorota na kuathiri uchumi wa nchi.

"EWURA inadhibiti kiuchumi sekta hiyo kwa kuweka utaratibu wa kupanga bei na kuhuisha bei hizo na tozo baada ya kupokea maombi au inapoona umuhimu wa kufanya hivyo kwa maslahi ya umma wote."

Ili kumwezesha mwombaji mwenye leseni ya kuuza gesi ya majumbani kuleta maombi ya bei kupitiwa na kuidhinishwa, EWURA inatumia mwongozo wa bei na tozo ya mwaka 2009. Kwa mujibu wa tovuti ya EWURA, moja ya mapitio ya bei na tozo za bei za gesi majumbani (LPG) yalifanywa Juni mwaka 2021.

Hata hivyo, mtikisiko wa masoko ya nishati hiyo duniani, kama ilivyo kwa bidhaa za mafuta ya dizeli na petroli, haujaiacha salama sekta hiyo na hivyo kufanya serikali itoe agizo la nishati hiyo kuletwa pamoja kuipa unafuu.

Kuanzia Septemba 2016, serikali ilianza uagizaji wa pamoja wa gesi hiyo baada ya kukutana na wadau, kupata uzoefu kutoka nchi zilizoendelea na pia kutatua changamoto usambazaji, usalama na ujazaji wa mitungi.

Uagizaji wa gesi hiyo ya mitungi unafanywa kwa pamoja sasa kuhakikisha kuwa kodi ya serikali inakusanywa ipasavyo na wafanyabiashara hao hawamiliki soko hilo. "Bei ya gesi ya mitungi inayotumika majumbani ni ghali, upatikanaji wake ni mgumu na pia haipatikani kwa mitungi midogo zaidi ambayo kila mwananchi wa kawaida anaweza kumudu," Waziri wa zamani wa Nishati, Dk. Medard Kalemani alisema mapema 2016.

Kwa kutambua umuhimu wa sekta ya nishati katika kupambana na janga la athari za mabadiliko ya tabianchi hivi sasa, serikali imeamua kuongeza jitihada za udhibiti wa matumizi ya LPG ili kulinda mazingira.

Mwaka 2023, Wizara ya Nishati inayoongozwa na January Makamba imeagiza kampuni za nishati ya LPG kusambaza katika vipimo vya ujazo mdogo ili watu zaidi waitumie kuokoa mazingira.

Agizo la wizara limetolewa Desemba 28, 2022 likilenga kutoa fursa kwa kampuni za uuzaji LPG kuandaa ujazo wa chini ya mitungi ya kilo tano ambayo kwa sasa ndio kiwango cha chini cha gesi ya majumbani inayouzwa.

Uzoefu unaonesha kampuni nyingi za gesi huuza zaidi gesi iliyo kwenye mitungi ya kilo tano, 15 kwa wateja wa matumizi ya nyumbani na mitungi mikubwa zaidi ya hapo kwa wenye hoteli, karakana za ufundi na viwanda.

Utafiti wa Shirika la Afya Duniani (WHO) umeonesha nusu ya watu duniani watakaoitumia gesi hiyo wataokoa kiasi cha Dola za Marekani bilioni 900 kuelekea karne ijayo.

Takwimu za matumizi ya gesi hiyo nchini zinaonesha utumiaji wa mitungi umekua kwa kiasi kikubwa na mwaka 2010 hadi 2011 tani 2,225 zilitumika ikilinganishwa na tani 5,762 za 2014 -2015.

Upatikanaji rahisi na wa kiwango kikubwa wa LPG unaelezwa na wataalamu mazingira na mafuta kuwa utaleta ushindani mkubwa wa kibiashara na kulinda mazingira kirahisi ikilinganishwa na mafuta ya taa ambayo ndio pekee yanapatikana kwa urahisi zaidi.

Katika hotuba yake ya bajeti ya mwaka wa fedha wa 2022/23, Waziri wa Nishati, Makamba alisema bungeni kuwa, malengo yake makuu ni kushuhusha bei ya nishati na kuhakikisha inapatikana kwa wingi zaidi.

Alisema, mwaka 2022/23, serikali imetenga Sh. bilioni 3.89 kuisambaza gesi asilia katika makazi na viwanda Dar es Salaam na Pwani kuongeza matumizi ya nishati hiyo.

Licha ya kuwa gesi ni rafiki wa mazingira na afya, ripoti ya Energy Access Situation ya mwaka 2016 inaonyesha ni asilimia 7.2 pekee ya kaya nchini zinatumia nishati hiyo kupikia ongezeko kutoka asilimia 0.3 mwaka 2011/2012. Kaguo anasema EWURA ikishirikiana na wadau itaongeza nguvu kuhamasisha wananchi kutumia gesi kuepusha nchi na uharibifu mazingira. Inakadiriwa hekta milioni nne za misitu huteketea kwa kuchomwa kuni au mkaa.

Ripoti ya Ewura ya mwaka 2017 inaonesha mwaka wa fedha 2015/16 na 2016/17 ongezeko la asilimia 50 lilirekodiwa mara 16 ya asilimia 3.12 za mwaka 2014/15 na 2015/16. Mwaka 2016/17 futi za ujazo 107,083 ziliingizwa na futi za ujazo 71,311 ziliingizwa 2015/16.

Mikoa inayoongoza kwa kupikia gesi ni Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Kilimanjaro, Mbeya na Manyara, Dar es Salaam takwimu zinaonyesha asilimia 26.7 ya wakazi wanatumia gesi kupikia, mafuta ya taa (22.1), kuni (14.3) mkaa (88.2) Simiyu inaongoza kutumia kuni kwa 94.3%.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Puma Energy Tanzania, Lameck Hiliyai, anasema wanaunga mkono serikali kukuza teknolojia, usalama wa gesi kwa mtumiaji na utunzaji wa mazingira.

**BEI ZA GESI**

Upangaji bei ya gesi hutofautiana kati ya nchi na nchi. Hakuna bei moja ya kimataifa. Bei ya jumla ya gesi huamuliwa na kiasi gani inagharimu wasambazaji wa nishati kununua kutoka wazalishaji wa ndani na nje.

**ANAYEFAIDIKA**

Kampuni zinazochimba na kusafirisha gesi zimenufaika na ongezeko la mahitaji. Sehemu kubwa ya LNG inatoka Australia, Qatar na Marekani. Gesi pia iko Norway na Bahari ya Kaskazini. Tanzania pia imegundua gesi asilia.




## NGOMENI ENTERPRISES

**NOTISI YA SIKU KUMI NA NNE (14) YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA.**

Kwa idhini na mamlaka tuliyopewa na benki ya **CRDB BANK PLC** makao makuu Dar es salaam tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) tu ili uweze kulipa deni lako lote unalodaiwa Pamoja na gharama za dalali. Kukaidi au kushindwa kulipa deni hilo tutauza dhamana uliyoweka kwa mnada wa hadhara kama inavyoonesha kwenye jedwari hapo chini.

| S/N | JINA LA MDAIWA | DHAMANA / MAHALI | TAREHE/ MUDA |
|---|---|---|---|
| 1. | AVIT DAMACEN MLINDA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO KIMARA STOP OVER, DAR ES SALAAM | 17.01.2023, KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA. |
| 2. | THAMES VALLEY COMPANY LIMITED | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO BUNJU WILAYA YA KINONDONI DAR ES SALAAM | 21.01.2023, KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 3. | JOYCE GUNTRAM LYASSA | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO MAKONGO JUU, DAR ES SALAAM | 24.01.2023, KUANZIA SA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 4. | KHARID RAJABU ABEDNEGO | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO VIKONGORO WILAYA YA ILALA, DAR ES SALAAM | 27.01.2023, KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| 5. | ALTO LEONARD NGUNYALI | NYUMBA YA MAKAZI ILIYOPO MBWENI MPIJI WILAYA YA KINONDONI DAR ES SALAAM | 30.01.2023, KUANZIA SAA 4 ASUBUHI NA KUENDELEA. |

**MASHARTI YAMNADA.**

1. Dhamana itauzwa kama zilivyo.
2. Mnunuzi atakayeshinda atalipa malipo ya awali ya asilimia 25 ya bei itakayofikiwa siku ya mnada na asilimia 75 atalipa ndani ya siku 14.
3. Mnunuzi atakayeshindwa kumalizia salio la asilimia 75 katika muda uliopangwa hapo juu, hatarudishiwa fedha alizolipa awali na mnada utarudiwa siku nyingine itakayopangwa.
4. Gharama zote za kubadilisha hati miliki, kutwaa nyuma na gharama nyinginezo zitakuwa juu ya mnunuzi.
5. Wateja wote mnakaribishwa kuona na kukagua nyumba muda wote isipokuwa usiku.

**MAWASILIANO:**
**CRDB BANK PLC HEAD QUARTER, NGOMENI ENTERPRISES, DSM. SIMU: 0719974916/ 07842520480784252048**

217213402


**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 145 OF 2022**

**In Matter of the Estate of the Late ANNA ELISA PALANGYO**

**By 1. ELISHILIA RUBEN URIO**
**2. ..................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.

Objection to the grand should be field on or before the **26TH** day of **January / 2023.**

Dated at **Morogoro**, this **19th** day of **DECEMBER 2022**

RESIDENT MAGISTRATE

**FOMU YA MIRATHI-2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo BOMA**
**Wilaya ya MOROGORO**
**Mkoa wa MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 01/2023**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHENU BLANDINA PIUS ALBART WA BONG'OLA KILAKALA**
**KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA COSTANTINE ELIAS LUANDA**

**TANGAZO**

(Kanunu ya 5 (2) kanuni za usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 26/ Mwezi 01 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Zingatia;

Endapo kuna yeyeto mwenye Wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.

* Wosia wa Marehemu huyu upo Mahakamani na waweza kukaguliwa
* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa leo tarehe 02 mwezi 01 mwaka 2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika mahakama ya mwanzo PONGWE usimamizi wa mirathi 87/2022 ombi la RAHEL ISAKA NYAKANGA kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu JACOB MANYIKA**

**Kwa YOYOTE ANAYEHUSIKA TANZANIA BARA**

Kwa watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 12.01.2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani inaweza kukaguliwa Tarehe 21.12.2022

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO PONGWE

## KUPOTEA KWA VYETI



**SHARIF AMIN MWALE** anatangaza kupotelewa na vyeti,cha kidato cha nne chenye index namba **S0720/0075** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya sekondari ya **MPITIMBI** mwaka 2013 na cheti cha UALIMU kilichotolewa na chuo cha **USHARIKA NAMTUMBO TEACHERS COLLEGE** kilichotolewa mwaka 2016,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi taarifa **KAR/BUK/RB/426503/2022**

## VYETI VIMEPOTEA



**MUNIRA AMIN MRISHA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba index no **S0188/0031** cha Kirinjiko Islamic Secondary, kimetolewa mwaka 2015. Cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0671/0537** cha Ubungo Islamic Secondary, kimetolewa mwaka 2018. Cheti cha Chuo chenye namba **MOCU/BABEC/134/17** cha Moshi Cooperative University kimetolewa mwaka 2020. Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/MSI/RB/1308/2023.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera Meya kuwakumbuka waandishi Mwaka Mpya

**MWAKA** Mpya umeanza vizuri kwa waandishi wa habari wa Mkoa wa Iringa baada ya Meya wa Manispaa ya Iringa Ibrahim Ngwada, kuukaribisha mwaka 2023 kwa kuwakopesha viwanja vya makazi na biashara ili kutatua tatizo la makazi ya kudumu kwa wanahabari hao.

Wanahabari 40 kati ya 80 walioomba kupatiwa viwanja na halmashauri hiyo kwa mkopo wamekopeshwa.

Tunasema hiyo ni hatua nzuri aliyoanza nayo Meya wa Manispaa Iringa na ni mfano wa kuiga katika kuimarisha ushirikiano kati ya wanahabari na ofisi yake.

Orodha ya majina ya waandishi waliobahatika kukopeshwa viwanja hivyo, imekabidhiwa rasmi kwa Mwenyekiti wa Klabu ya Waandishi Mkoa wa Iringa (IPC), Frank Leonard kwa hatua zaidi.

Kutimizwa kwa ahadi hiyo, kumekuja kutokana na waandishi hao kuomba kupatiwa viwanja vinavyotolewa na halmashauri hiyo kwa mkopo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Mei 2022.

Kutimizwa kwa ahadi hiyo kunatia matumaini kwa wengine ambao waliomba kukopeshwa viwanja ili waondokane na adha ya kukosa nyumba za kudumu na usumbufu wa kupanga na kudaiwa kodi huku wengine wakidhalilika wakati mishahara inapochelewa.

Waandishi wa habari wanafanya kazi kubwa ya kuelimisha kupitia kalamu zao na vile vile kuhabarisha na kuburudisha. Pia wanapitia mazingira magumu katika ukusanyaji habari hizo.

Kama wanakumbana na changamoto katika kazi zao na wanaporudi nyumbani wanakosa amani kwa sababu ya kero za wenye nyumba kudai kodi, hata umakini unakosekana wanapokuwa wanafanya kazi ya kukusanya habari.

Katika yaliyopitishwa na Mkutano Mkuu Maalum wa IPC ni pamoja na la kutengeneza mwongozo maalum wa utatuzi wa migogoro utakaotumiwa na klabu zote, yenye (maazimio) kaulimbiu ya kutoka kuzuri kwenda kuzuri zaidi (moving from Good to Great).

Meya huyo alifafanua kuwa idadi ya waandishi wa habari wanaohitaji viwanda ni kubwa, lakini kwa kuanzia wametoa viwanja 40 kulingana na uwezo uliopo na wataendelea kutoa kwa waliobaki kadiri ya fursa zinapotokea.

Hata hivyo, Meya alisema uwezo wa halmashauri kuwapatia waandishi wote viwanja bure haupo, lakini uwezo wa kusubiri kwa kipindi kirefu kwa kuzingatia vipato upo.

Suala la makazi ya kudumu kwa waandishi wa habari ni msingi sana kwa vile wengi wao wanaishi katika nyumba za kupanga zenye changamoto mbalimbali na kusababisha baadhi yao kushindwa kufanya kazi zao kwa weledi.

Waandishi wa habari kama walivyo wafanyakazi wa tasnia nyingine wana mahitaji mengi kutokana na kazi zao kufanya katika mazingira magumu.


Waandishi wa nchi zingine zilizoendelea, husaidiwa kupata kadi zinazowawezesha kununua vitu katika maduka makubwa hata kama mshahara ukichelewa, wana uhakika wa kuishi na kufanyakazi bila mawazo.

Kazi yoyote mtu anapofanya anatakiwa asiwe na mawazo wapi atapata chakula au pesa ya kulipa kodi, mbali na changamoto zingine za ada za watoto, ili aifanye kwa weledi na asipate kishawishi cha kupokea rushwa.

Baadhi ya wafanyakazi hujiingiza katika matatizo sio kwa kupenda, lakini ni kutokana na mazingira yanayomlazimu kufanya hivyo na kujikuta akiingia matatani.

Meya wa Iringa umeonyesha mfano na viongozi wengine waige kuisaidia tasnia ya habari iweze kufanya vizuri zaidi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Madereva anzeni sasa kuwalinda wanafunzi

**WANAFUNZI** wa kike ni waathirika wa rushwa ya ngono inayotokana na lifti za madereva wa bodaboda na daladala, wanaowarubuni kwa chips, daftari, pesa za matumizi, maji, soda kwenye jua kali vyote vikipalilia uhusiano unawakwamisha mabinti kielimu

ili kukabiliana na tatizo hilo, kampeni ya nyingi zinafanywa na mikakati ya kuwanusuru wanafunzi mkoani Dar es Salaam zimeshika kasi.

Mathalani, kuna kampeni ya safari salama bila rushwa ya ngono, inayofanyika kwenye wilaya za Ilala, Kinondoni na Temeke.

Ni katika harakati za kupinga ukatili wa kijinsia na udhalilishaji wasichana hivyo shule zinapotarajiwa kuanza wiki ijayo madereva wazingatie hilo wawe walinzi badala ya wanaoangamiza wanafunzi.

Katika kampeni hiyo ya safari salama bila rushwa ya ngono inatoa elimu nyumba kwa nyumba, shuleni na vituo vya daladala, bodaboda na bajaj, kuwahamasisha madereva na jamii kuacha kuwarubuni wasichana.

Madereva hao wanaodaiwa kuhusika na kuwaingiza wasichana kwenye rushwa ya ngono kwa lifti, wanaelimishwa kuwalinda na kuwasaidia kufika salama shuleni na kurudi nyumbani pia.

Shirika la Wanawake Katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), ndilo linalofanikisha kampeni hiyo kwa kushirikiana na kamati zilizoundwa na madereva hao, wanachama wa shirika hilo.

Kwa hiyo elimu ya kupinga vitendo hivyo, isaidie na ulinzi wa watoto ufanikiwe si shuleni, nyumbani na vituoni walipo madereva.

WAJIKI inawahimiza kuacha kulaghai wasichana pia kuwapa na kubandika stika kwenye vyombo hivyo vya usafiri vyenye ujumbe wa safari salama kwa wasichana na wanafunzi bila rushwa ya ngono.

Kwa Dar es Salaam zipo kamati 72 zilizoundwa na madereva wa bodaboda, bajaj na daladala takribani 30,000 wilayani Kinondoni na Ilala.

Hivyo mbali na kutoa elimu madereva wawazuie wanafunzi kuzagaa vituoni, lakini watafutie usafiri wa haraka, ili wawahi shule au nyumbani wakisafirishwa na daladala hata bajaji na pikipiki kama si eneo lenye umbali mrefu.

Madereva wakumbuke wana jukumu la kuwaokoa wanafunzi na mimba zinazopatikana kwenye lifti.

Lakini hata wanafunzi nao waanze kujitambua na kujiamini kuwa kupewa lifti siyo sababu ya kurubuniwa na kujiingiza kwenye uhusiano unaosababisha kuvuruga masomo.

Ni muhimu madereva kujua kuwa kazi yao ni muhimu lakini isiwe chanzo cha kuwaangamiza mamia ya wasichana wa Tanzania kwenye upotovu na kuvuruga maisha yao.

Wazazi, walezi na walimu wanaamini madereva na makondakta wakiamua kuacha kuhadaa wanafunzi ukatili huo wa kijinsia na unyanyasaji havitashamiri katika jamii.

Madereva wasaidie watoto wetu wanapokwenda shuleni kuanzia wiki ijayo wasafiri salama na kutimiza malengo yao ya elimu na kupunguza ukatili wa ngono kwa wanafunzi.

Takwimu za polisi, zinaonyesha matukio ya ukatili kwa watoto yanazidi kuongezeka, kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu yamefikia 6,168."

Kati ya hao wasichana ni 3,287 na wavulana ni 881, huku waliobakwa wakiwa 3,524 na waliolawitiwa ni 637, wavulana ni 567 na wasichana ni 70.

Mambo hayaishii hapo waliopata mimba ni 1,887.

Kampeni ya safari salama kwa wasichana na wanafunzi bila rushwa ya ngono inawezekana ianze kuzaa matunda sasa mwaka huu wa 2023 unapoanza na kukomesha ukatili wa kijinsia kwenye jamii na kulinda watoto.

Pamoja na madereva kila mmoja anatakiwa kutimiza wajibu wake kukomesha vitendo hivyo, ikiwamo kutoa za taarifa kwa vyombo vya dola, badala ya kuiachia serikali na asasi za kiraia zinazopambana na ukatili wa kijinsia.

Kwa hiyo mwaka mpya unapoanza madereva, walezi, wazazi timizeni wajibu wa ulinzi kwa watoto ili wasichana wetu na wavulana wawe na hatima bora kielimu.

HABARI KITAIFA

# TRA yajivunia makusanyo kodi kwa 99%

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imesema katika kipindi cha nusu ya kwanza ya mwaka wa fedha 2022/23 kuanzia Julai hadi Desemba mwaka jana, imekusanya Sh. trilioni 12.46, sawa na asilimia 99 ya lengo la makusanyo ya Sh. trilioni 12.48.

Pia imesema imevuka lengo la makusanyo kwa kipindi cha Desemba mwaka jana kwa kukusanya Sh. trilioni 2.77 kati ya lengo iliyokuwa imejiwekea la kukusanya Sh. trilioni 2.60 ikilinganishwa na kilichokusanywa katika mwezi kama huo mwaka 2021.

"Makusanyo ya mwezi Desemba mwaka jana yana ufanisi wa asilimia 106.5 sawa na ukuaji wa asilimia 10.3 ukilinganisha na makusanyo ya Desemba 2021," ilisema taarifa ya Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata.

"Pamoja na makusanyo haya kuvuka lengo la Desemba 2022, ndicho kiwango cha juu zaidi kukusanywa kwa mwezi tangu kuanzishwa kwa mamlaka mwaka 1996, tunaendelea kuwashukuru walipakodi na wadau wetu mbalimbali kwa kujitoa katika kipindi cha nusu mwaka ambapo mwenendo wa ulipaji kodi kwa hiari na mahusiano baina ya mamlaka na walipakodi umeendelea kuimarika kwa kiwango cha kuridhisha."

Kwa mujibu wa Kidata, makusanyo hayo ni ongezeko la Sh. trilioni 1.35 ikilinganishwa na kiwango cha makusanyo cha Sh. trilioni 11.11 kilichokusanywa kwa kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2021/22 na ongezeko hilo ni sawa na ukuaji wa makusanyo wa asilimia 12.2.

Kidata alisema bado kuna umuhimu wa kuongeza kiwango cha makusanyo kwa kuinua kiwango cha ulipaji kodi kwa hiari ili kuwezesha serikali kuongeza wigo wa utoaji huduma kwa wananchi wote ikiwamo ulinzi, miundombinu ya barabara, huduma za kijamii ikiwamo elimu, afya, maji, umeme na nyingine.

"Kwa namna ya pekee, TRA inatoa shukrani kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kusaidia katika utekelezaji wa mikakati mbalimbali ya kiutendaji. Mamlaka itaendelea kufanyia kazi maelekezo na miongozo ya serikali namna bora ya kukusanya mapato bila matumizi ya nguvu na kujenga mazingira wezeshi ya uwekezaji na ufanyaji biashara nchini,"alisema Kidata.

**"Makusanyo ya mwezi Desemba mwaka jana yana ufanisi wa asilimia 106.5 sawa na ukuaji wa asilimia 10.3 ukilinganisha na makusanyo ya Desemba 2021," ilisema taarifa ya Kamishna Mkuu wa TRA, Alphayo Kidata.**



Meya wa Manispaa ya Iringa, Ibrahim Ngwada (kushoto), akimkabidhi Mwenyekiti wa Iringa Press Club (IPC) orodha ya majina ya waandishi wa habari waliyokopeshwa viwanja vya makazi na biashara jana. **PICHA: FRIDAY SIMBAYA**

# Jela miaka 30 kusafirisha dawa za kulevya gramu 75

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Wilaya ya Kigamboni mkoani Dar es Salaam imemhukumu kifungo cha miaka 30 jela Ally Issa (40) baada ya kukiri kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroine hydrochloride gramu 75.62.

Mbali na Issa, maarufu kama Mpeche, washtakiwa wengine ni Abdulrahman Sinauwanja (40) na Mariam Fundi (28), wote wakazi wa Kibugumo, Kigamboni ambapo wao hawakukiri kosa hilo na kesi yao inaendelea leo.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Janeth Mgaya wa mahakama hiyo wakati washtakiwa hao walipofikishwa mbele yake kwa ajili ya kusomewa mashtaka yao.

Baada ya washtakiwa hao kusomewa kosa lao, mshtakiwa Issa alikiri kusafirisha dawa hizo kinyume cha sheria ndipo mahakama ikamtia hatiani kwa kosa hilo na kumsomea adhabu yake.

Hakimu Mgaya alisema mahakama inamtia hatiani mshtakiwa kwa kukiri kosa lake, hivyo atatumikia kifungo cha miaka 30 jela.

Inadaiwa kuwa Desemba 9, 2022, washtakiwa wakiwa eneo la Kibugumo kwa Mbezi, Kigamboni ndani ya Mkoa Wa Dar es Salaam, walikutwa wakisafirisha dawa za kulevya aina ya heroine gramu 75.62.

Hata hivyo, baada ya kusomewa mashtaka yao, washtakiwa Sinauwanja na Fundi walikana kuhusika na tuhuma hizo huku Issa akikiri kutenda kosa hilo.

**KABWELA** Fadhili Mohamed



# TPA yatoa utaratibu wa utoaji mizigo bandarini

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA), imesema shughuli za uendeshaji wa kitengo cha makasha cha gati namba nane hadi 11 za Bandari ya Dar es Salaam zitakuwa chini ya mamlaka hiyo.

Kwa mujibu wa tangazo lililotolewa na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, TPA imeanza kufanya shughuli hizo tangu Januari mosi, mwaka huu baada ya mkataba kati ya TPA na kampuni Binafsi ya Kuhudumia Makontena Tanzania (TICTS) kufikia ukomo.

"Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania inautaarifu umma, wadau na wateja kwamba kuanzia Januari mosi mwaka huu, shughuli zote za uendeshaji wa kitengo cha makasha cha gati namba nane na 11 za Bandari ya Dar es Salaam zitakuwa chini ya TPA," lilisema tangazo hilo.

"Hii ni baada ya mkataba na kampuni ya International Container Terminal Service Limited (TICTS) kufikia ukomo wake Septemba 2022 na kukabidhiwa TPA Desemba 31, mwaka jana."

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, kuanzia Januari mosi mwaka huu, kila mteja mwenye mzigo wake katika eneo ambalo lilikuwa chini ya usimamizi na uendeshaji wa kampuni ya TICTS na ambaye atapeleka mzigo kupitia gati namba nane hadi 11 za Bandari ya Dar es Salaam, atatakiwa kufanya malipo yote ya gharama za huduma za Bandari kwa kutumia mwongozo wa gharama bandari uliokuwa wa kampuni ya TICTS kupitia benki kwenye akaunti zilizowekwa.

"Katika kipindi hiki cha mpito, anwani za mawasiliano na ofisi ambazo zitatumika kutoa huduma zitaendelea kuwa kama ambavyo ilikuwa ikifanyika wakati wa uendeshaji wa shughuli za kampuni ya TICTS hadi pale utaratibu mpya utakaotumika," alieleza.

TICTS imehudumu katika Bandari ya Dar es Salaam kwa miaka 22, tangu iliposaini kutoa huduma ya makontena na mizigo mingine, kazi ambayo itafanywa pia TPA.

Desemba 21, mwaka jana, akizungumza wakati akifunga semina ya kuwajengea uwezo waandishi wa habari kuhusu utendaji kazi wa mamlaka hiyo, Naibu Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Juma Kijavala, alisema wafanyakazi wote wa TICTS ajira zao zipo salama na wataendelea kutekeleza majukumu yao upande wa makontena na watalipwa stahiki zao kama ilivyokuwa awali na TPA.




Mwongoza watalii wa Kampuni ya Utalii ya ZARA Tours, Faustine Chombo (kulia), akiwa pamoja wageni kutoka mataifa mbalimbali katika kilele cha Mlima Kilimanjaro cha Uhuru Peak chenye urefu wa mita 5,895 kutoka usawa wa bahari mwishoni mwa wiki. **PICHA: JAMES LANKA**

## Mkurugenzi ashindwa kulipa bil. 2/-, aendelea kusota rumande

**Na Grace Gurisha**

MKURUGENZI Mtendaji wa Kampuni ya JATU Public Ltd, Peter Gasaya (32), anayetuhumiwa kujipatia Sh. bilioni 5.1 kwa udanganyifu, ameelezwa na mahakama kuwa ili awe nje kwa dhamana anatakiwa awasilishe mahakamani Sh. bilioni 2.6.

Gasaya anatuhumiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam kujipatia kiasi hicho cha fedha kutoka SACCOS ya JATU kwa madai kuwa ataizalishia faida huku akijua si kweli. Sharti hilo la dhamana lilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Mary Mrio wa mahakama hiyo wakati kesi hiyo ilipoitwa kwa ajili ya mshtakiwa kusomewa masharti ya dhamana.

Hakimu Mrio alimweleza mshtakiwa kuwa anaweza pia kuwasilisha hati ya mali isiyohamishika yenye thamani ya kiasi hicho cha fedha.

Pia mshtakiwa huyo atatakiwa awe na wadhamini wawili wenye barua za utambulisho na vitambulisho ambavyo kila mmoja atatia saini bondi ya kiasi hicho cha fedha.

Baada ya mshtakiwa kusomewa masharti hayo, alishindwa kuyatimiza na alirudishwa rumande hadi Januari 11, mwaka huu, kesi yake itakapotajwa tena.

Awali akisoma hati ya mashtaka, Wakili wa Serikali, Tumaini Mafuru, alidai kuwa kati ya Januari Mosi, 2020 na Desemba 31, 2022, mshtakiwa akiwa ndani ya Jiji na Mkoa wa Dar es Salaam kama Mkurugenzi wa kampuni hiyo, alijipatia Sh. 5,139,865,733 (Sh. bilioni 5.14) kwa njia ya udanganyifu kutoka JATU SACCOS.

Mshtakiwa anadaiwa kuchukua fedha hizo kwa madai kuwa atazipanda fedha hizo na kuzalisha faida huku akijua si kweli.

Baada ya mshtakiwa kusomewa shtaka lake, alikana kuhusika na tuhuma hizo, Hakimu Mrio akisema mahakama hiyo haina mamlaka ya kutoa dhamana inayozidi Sh. milioni 300.

## Mbunge ataka wananchi wajikinge UVIKO-19

**Na Halfani Chusi**

MBUNGE wa Kinondoni, Abbas Tarimba amewataka wananchi kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Tarimba alitoa rai hiyo juzi mkoani Dar es Salaam kwenye mkutano wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi Kata ya Makumbusho.

Alisema kwa sasa kumeanza kuibuka magonjwa ya mlipuko na mafua makali, akiwataka wananchi kujitokeza kuchanja ili kuwa salama.

"Achaneni na mawazo potofu ya wale wanaosema ile chanjo ina madhara, hao ni waongo. Mimi mwenyewe nimechanja na sijaona madhara yoyote zaidi ya kuona mwili wangu umezidi kuwa imara zaidi.

"Ukichanja hata ukitaka kwenda nchi za nje, ukionyesha tu kile cheti unakuwa salama na mlolongo wake unakuwa mdogo tofauti na mtu ambaye hajachanja," alisema Tarimba.

Katika mkutano huo, pia alikemea baadhi ya wafuasi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) na viongozi kwenye kata hiyo kuwekeana bifu, hali iliyosababisha baadhi yao kutokuwa na maelewano mazuri ndani ya chama.

Alisema ilani ya chama hicho inasisitiza kila mmoja kuhubiri amani, lakini amebaini kwenye Kata ya Makumbusho kuna baadhi ya wanachama wasio waadilifu wanataka kutingisha msimamo wa wengine.

"Na wala hatutokubali, pale tutakapomwona mtu anaunda vigenge kwa ajili ya kukiharibu chama chetu, tunapaswa kukitumikia chama chetu na sio kutumikia watu na wala mtu asifikirie anaweza kutingisha misingi ya chama hiki.

"Hatutokubali, tutatumia nguvu kuhakikisha kila mtu anafuata misingi ya chama hiki, kwa hiyo sihitaji kuona matabaka katika kata hii, hayo yanaweza kuwa sehemu ya kutufanya tukaanguka katika uchaguzi ujao," alionya.

Vilevile, aliwataka wazazi kuungana na serikali kupinga vita dhidi ya ukatili kwa kufuatilia mienendo ya watoto wanapokuwa nyumbani na shuleni.

Diwani wa Makumbusho, Mohamed Mohamedi, alimshukuru mbunge huyo, akisitiza kwa muda aliokaa madarakani, amefanya mambo ya maendeleo.

"Kwa kipindi kifupi Tarimba amesababisha miradi mingi kukamilika, zaidi ya miradi 18, tumezindua kituo cha afya cha kata pamoja na kuzifanyia ukarabati shule zote zilizomo ndani ya kata hii, pamoja na kuzifanyia ukarabati barabara za mitaa.

"Ukiachana na nafasi ya kuwa yeye ni mbunge lakini kuna muda huwa anatumia taaluma yake ya sheria kuhakikisha miradi ndani ya kata hii inaenda na amefanya hivyo mara nyingi," alisema.

HABARI KITAIFA

## DAWASA yaboresha upatikanaji maji

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA) Ukonga imeboresha upatikanaji wa huduma ya maji na kuongeza idadi ya wateja kutoka 5,978 hadi 7,262 kwa mwaka jana.

Ongezeko la wateja kwa Mkoa wa Ukonga limetokana na maboresho ya huduma yaliyofanywa kwenye maeneo mbalimbali yaliyokuwa na changamoto ya maji ikiwamo mitaa ya Kisumu, Mwakanga, Kinyamwezi eneo la Mapensheni lililoko Kata ya Pugu.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Meneja wa DAWASA Ukonga, Sirila Josephat, alibainisha hayo wakati wa mahojiano kuhusu utekelezaji wa miradi ya maji.

Aliitaja mitaa mingine iliyokuwa na changamoto ya maji kuwa ni ya Kichangani Radar, Bwera na Bombambili iliyoko Kata ya Majohe na Mitaa ya Guluka, Kwalala na Gongo la Mboto.

Alisema ofisi ya DAWASA Ukonga imetekeleza kazi mbalimbali ikiwamo kubadilisha miundombinu chakavu na kutandaza mabomba mapya pamoja na kutekeleza miradi ya maji kwenye maeneo husika yenye shida katika upatikanaji wa maji.

Alisema mkoa uliwekeza nguvu nyingi katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maji ikiwamo ya maunganisho mapya ukiwamo mradi wa Majohe, Mapensheni wa kusogeza huduma Kisiwani na Buyuni.

"Tulichukua hatua madhubuti za kutekeleza miradi mbalimbali ya maji kwa lengo mahususi la kuwezesha wananchi kupata maji hasa kwa maeneo yaliyokuwa na shida ya maji ya muda mrefu," alisema Sirila.

Alibainisha kuwa miradi iliyotekelezwa ilihusisha ulazaji wa mabomba ya ukubwa wa inchi nane, sita, nne na tatu kwa umbali wa kilomita 14.25 kwenye eneo la huduma.

"Mradi wa kusambaza maji Kisiwani ulihusisha ulazaji wa bomba la inchi 1.5 na inchi mbili kwa umbali wa mita 750, mradi wa Mapensheni ulihusisha ulazaji wa mabomba ya inchi 1.5 kwa umbali wa mita 600 na mradi wa Buyuni ulihusisha ulazaji wa mabomba ya inchi 1.5 kwa umbali wa mita 450," alisema.

Sirila alisema kupitia maboresho yaliyofanyika, huduma ya maji kwa sasa imeimarika na imesaidia kuondoa shida ya maji iliyokuwapo kwenye maeneo ya Gongo la Mboto, Ulongoni A, Darajani, Jeshini, Songas, Kajiungeni, Ulongoni B, Shamba la Mpunga, Pugu Station, Kirumba na Kisumu.

Alisema kwa sasa huduma ya maji kwenye maeneo mengi ya Jimbo la Ukonga imeimarika na wananchi wanaendelea kufurahia huduma.

Kazi inaendelea ya kuhakikisha maeneo yaliyosalia yakiwamo ya Mwakanga CCM, Mwakanga kwa Minja, Pugu Sekondari, Mwakanga Kanisa la Mabati, Mwakanga Hija na Kibiriko Juu yote yanapata maji kikamilifu.

"Tunaendelea na kazi ya kuboresha huduma ya maji na mipango iliyoko kwa mwaka ujao 2023/24 ni kuongeza usambazaji wa huduma kwenye maeneo yote ambayo bado hayajafikiwa na huduma," alisema.

Mkoa wa DAWASA Ukonga unatoa huduma katika kata 10 za Pugu, Pugu Stesheni, Gongo la Mboto, Ukonga, Majohe, Buyuni, Chanika, Zingiziwa, Msongola na Kipunguni B zenye jumla ya wananchi 7,262 wanaopata huduma.

# Wanafunzi wafa maji kwa kuzama kwenye kisima

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

WATOTO wawili wamekufa maji baada ya kuzama kwenye kisima wakati wakifua nguo eneo la mtaa wa Mwilima Kata ya Kasamwa, mkoani Geita.

Watoto waliokufa maji ni Janeth Edward (13), mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi Mwilima na Janeth Amos (12) ambaye ni mwanafunzi wa darasa la tano katika Shule ya Msingi Nyalwanzaja. Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani hapo, Edward Lukuba, alisema tukio hilo lilitokea Desemba 31, 2022 majira ya saa sita mchana.

Lukuba alisema siku ya tukio walipata taarifa kutoka kwa Ofisa Tarafa Kasamwa kuwapo kwa watoto wawili wanaoelea juu ya maji kwenye kisima. Alisema baada ya taarifa hizo, askari wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji walienda eneo la tukio na kukuta miili ya watoto hao ikielea kwenye kisima na kwa kushirikiana na askari polisi waliitoa na kuipeleka katika Kituo cha Afya Kasamwa kwa uchunguzi zaidi.

Alisema chanzo cha kifo hicho ni Desemba 30, 2022 watoto hao ambao kwa sasa ni marehemu waliambiwa na wazazi wao kwenda kufua nguo kwenye kisima cha maji baadaye watoto hao hawakurudi nyumbani, ilipofika majira ya saa 10 jioni wazazi walipata wasiwasi na kuanza kuwatafuta watoto hao bila ya mafanikio.

Alisema Desema 31, 2022 majira ya saa moja jioni watoto hao walielea juu ya maji kwenye kisima na ilipofika majira ya saa mbili usiku watoto hao waliopelewa kutoka kwenye kisima wakiwa wameshafariki dunia na kupelekwa Kituo cha Afya Kasamwa kwa uchunguzi.

Kaimu Kamanda, alisema matukio mengi ya vifo vya watu kuzama maji katika mkoa wa Geita yanajitokeza mara kwa mara na kuwaomba wazazi kuhakikisha wanaacha tabia ya kuwaagiza watoto wadogo kwenda kufua nguo kwenye visima.

Mganga Mfawidhi wa kituo hicho, Emmanuel Alex, alithibitisha kupokea miili ya watoto hao na kwamba anaifanyia uchunguzi ili kuikabidhi kwa ndugu kwa ajili ya mazishi.



Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii, Kata ya Songe, Wilaya ya Kilindi, Mkoa wa Tanga wakipima mpaka wa pori la mifugo eneo la Kwenyengo lenye mgogoro baina ya wafugaji na wakulima, (wa pili kushoto) ni Ofisa Mifugo wa Kata, Ismael Niilo. **PICHA: DEGE MASOLI**

## Tanga yajivunia miradi ya kubadili maisha ya wakazi

**Na Mwandishi Wetu,** TANGA

MKOA wa Tanga umesema kwa kipindi cha mwaka mmoja na nusu cha Rais Samia Suluhu Hassan umenufaika na miradi ya maendeleo ambayo imeboresha maisha ya wananchi katika sekta mbalimbali.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini hapo mwishoni mwa wiki, Katibu Tawala wa Mkoa wa Tanga, Pili Mnyema, alisema miradi hiyo ni ya sekta za afya, kilimo, maji, ufugaji na bandari ambazo zote zinagusa maisha ya wananchi.

Alisema kwa kipindi cha mwaka mmoja na nusu, mkoa ulipokea zaidi ya Sh. bilioni 23 za ujenzi wa madarasa ya shule za sekondari, zikijumuisha Sh. bilioni 9.9 mwaka 2021 zilizotolewa kwa ajili ya ujenzi wa vyumba 495 vya madarasa na kulikuwa vyumba 228 vya shule shikizi.

Alisema mwaka jana walipokea Sh. bilioni 4.98 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 249 vitakavyopokea wanafunzi wa kidato cha kwanza wanaofungua wiki ijayo na hakuna mwanafunzi aliyeachwa.

Kwa mujibu wa Pili, katika sekta ya afya walipokea Sh. bilioni 6.54 kuboresha sekta ya afya kwenye miradi ya ujenzi wa vituo vya afya, hospitali za wilaya na vituo vya huduma za dharura.

"Sekta hii inakwenda kugusa maisha ya wananchi wa kawaida kabisa, tunaposema afya inamgusa mwanamke kwa sababu ndiyo mlezi wa jamii, elimu napo tunamgusa," alisema. Pia alisema kwa kipindi hicho kwenye sekta ya maji walipokea Sh. bilioni 15 za utekelezaji miradi, ikiwamo kuboresha upatikanaji wa maji katika wilaya za Tanga, Muheza na Pangani na Sh. bilioni 9.8 zinatumia kufanya upanuzi wa chanzo cha maji Mto Zigi. Alisema hivi karibuni waliingia mkataba wa kuboresha upatikanaji wa maji wilaya ya Mkinga wa Sh. bilioni 35 na mwingine utekelezaji wa kuboresha upatikanaji wa maji Mji wa Kabuku.

"Tuna miradi ya uboreshaji wa maji kwenye miji 28, Tanga imepata miji ya Korogwe, Handeni na Muheza kwa gharama ya Sh. bilioni 171. Tunatatua matatizo, badala ya kujikita kwenye shughuli za nyumbani, wanawake wanatafuta maji, kutokana na miradi hii watatumia muda wao kutekeleza majukumu mengine ya kujiingizia kipato kwa sababu maji yapo," alisema.

Kwa upande wa barabara, alisema kuna mradi wa Handeni-Pangani-Garo hadi Dodoma, pia kilomita 50 ya Pangani-Kwamsisi-Makurunge hadi Bagamoyo ambazo zikikamilika zitafungua mkoa huo na kuvutia uwekezaji.

Kwenye sekta ya viwanja wa ndege, alisema wanaendelea na maboresho ili ndege kubwa zitue na tayari zimetengwa Sh. bilioni 55 kwa ajili ya kazi hiyo.

Kwa mujibu wa Pili, mkoa umeendelea kusimamia uzalishaji wa mkonge ambao ni dhahabu ya mkoa huo kwa kufufua mashamba na kukaribisha wawekezaji kuwekeza kwenye zao hilo la kibiashara.

# Upelelezi kesi kocha wa makipa Simba wakamilika

**Na Grace Gurisha**

UPELELEZI wa kesi ya kusafirisha dawa za kulevya aina ya heroine kilo 34.89 inayomkabili aliyekuwa Kocha wa Makipa wa Klabu ya Soka ya Simba, Mwalami Sultan na wenzake watano umekamilika.

Mbali na Sultan washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni mmiliki wa Kituo cha Soka cha Kambiasso Sports Academy, Kambi Seif, Maulid Mzungu, Said Matwiko, John John na Saraha Eliud. Taarifa hiyo ya kukamilika kwa upelelezi ilitolewa jana na Wakili wa Serikali, Caroline Matemu mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Mary Mrio wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Matemu alidai kuwa upelelezi umekamilika na wameshapeleka taarifa Mahakama Kuu, hivyo wanasubiri taarifa hiyo irudi ili wawasomee washtakiwa maelezo ya mashahidi wa kesi hiyo.

Hakimu Mrio baada ya kusikiliza hayo, aliahirisha kesi hiyo ambayo ilikuwa inaendeshwa kwa njia ya mtandao hadi Januari 16, mwaka huu, itakapokuja tena kwa ajili ya kutajwa. Ilidaiwa kuwa Oktoba 27, 2022 huko Kivule, ndani ya Wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, washtakiwa walikutwa wakisafirisha kilo 27.1 za dawa za kulevya aina ya heroine.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Novemba 4, 2022, huko Kamegele, Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, washtakiwa walikutwa wakisafirisha kilo 7.79 za dawa za kulevya aina ya heroine.

Hata hivyo, washtakiwa hawakuruhusiwa kujibu kitu chochote mahakamani huko kwa kuwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu haina mamlaka ya kusikiliza kesi za uhujumu uchumi.



Mkurugenzi Mkuu wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mhandisi Hassan Saidy (kulia), akimkabidhi Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Tanga na Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashimu Mgandilwa, mkataba wa usambazaji umeme vijijini katika mkoa huo uliosainiwa juzi jijini Tanga. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Waandishi wa habari wakopeshwa viwanja

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

MEYA wa Manispaa ya Iringa, Ibrahim Ngwada, ametuma salamu za Mwaka Mpya 2023 kwa waandishi wa habari mkoani Iringa kwa kuwakopesha viwanja kwa ajili ya makazi na biashara ili kutatua kero ya makazi kwa kundi hilo.

Waandishi wa habari 40 kati ya 80 walioomba kupatiwa viwanja na halmashauri hiyo kwa mkopo, wamekopeshwa ili kutatua kero inayowakabili katika kupata makazi.

Orodha ya majina ya waandishi wa habari 40 waliopatiwa viwanja hivyo, ilikabidhiwa rasmi kwa Mwenyekiti wa IPC, Frank Leonard kwa hatua zaidi.

Kutimizwa kwa ahadi hiyo, kumekuja kufuatia waandishi wa habari mkoani humo kuomba wapatiwe viwanja vinavyotolewa na halmashauri hiyo kwa mkopo wakati wa maadhimisho ya Siku ya Uhuru wa Vyombo vya Habari Mei mwaka jana ambayo meya huyo alikuwa mgeni rasmi.

Meya Ngwada alitimiza ahadi hiyo wakati wa Mkutano Mkuu Maalum wa Klabu ya Waandishi wa Habari Mkoa wa Iringa (IPC) uliofanyika Desemba 31, mwaka jana, ukilenga kujadili mambo mbalimbali pamoja na kupitisha maazimio 10 ya Mkutano Mkuu wa Umoja wa Vilabu vya waandishi wa Habari Tanzania (UTPC).

Moja ya maazimio yaliyopitishwa na Mkutano Mkuu Maalum wa IPC ni kutengeneza mwongozo maalum wa utatuzi wa migogoro utakaotumiwa na klabu zote.

"Ninakumbuka kwenye siku ile ya maadhimisho ya Siku Uhuru wa Vyombo vya Habari duniani yanayofanywa kila mwaka mwezi Mei, mlinialika kuwa mgeni rasmi, mlinieleza changamoto mbalimbali, lakini mkaniomba jambo moja muhimu la changamoto ya makazi ya kudumu kwa vile wengi wenu mnaishi katika nyumba za kupanga," alisema.

Alifafanua kuwa idadi ya waandishi wa habari wanahitaji viwanda ni kubwa, hivyo kwa kuanzia wametoa viwanja 40 kulingana na uwezo uliopo kwa sasa na wataendelea kutoa kwa waliobaki kadri fursa zinapotokea.

"Baada ya kulipeleka jambo hilo katika Baraza la Madiwani la Manispaa ya Iringa, tuliamua kuwakopesha baadhi ya waandishi wa habari viwanja vya kujenga nyumba kwa utaratibu wa kulipa kidogo kidogo mpaka watakapomaliza," alisema Ngwada.

Aliongeza kuwa uwezo wa halmashauri wa kuwapatia waandishi wa habari wote viwanja bure haupo, lakini uwezo wa kusubiri kwa kipindi kirefu kwa kuzingatia vipato upo.

"Tulipokea majina mengi ya waandishi wa habari lakini uwezo wa kutoa viwanja kwa waandishi wote kwa mara moja haukufanyika, lakini tuliona tuanze na wachache.

"Kadri fursa zinavyotokea tutaendelea kutoa na kwa waliobaki, ili halmashauri iweze kujiendesha kimapato," alisema Meya Ngwada.

Meya huyo pia aliwataka waandishi wa habari mkoani Iringa na kwingineko kuzingatia maadili ya taaluma yao pamoja na kufanya kazi kwa weledi zaidi ili kuleta maendeleo katika jamii na taifa kwa ujumla.

Aliwataka waandishi wa habari kuzingatia maadili ya uandishi wa habari na weledi wakati wa utekelezaji majukumu yao ya kila siku ili kuleta ufanisi.

Aliongeza kuwa kazi ya mwandishi wa habari ni kuelimisha, kukosoa, kuweka uwiano wa mambo katika jamii na kusifia mtu anapofanya vizuri ili kuleta maendeleo.

Meya Ngwada alisisitizia waandishi wa habari kujenga utamaduni wa kukosoa pamoja na kusifia pindi wanapofanya vizuri katika nyanja mbalimbali na kuhakikisha wanafanya msawazo wa habari na kuzifanyia utafiti wa kutosha, ili kupunguza malalamiko katika jamii.

"Tunaomba waandishi wa habari mnapopata jambo lolote msisite kutushirikisha ili tuone namna ya kulitatua jambo hilo, milango ipo wazi tunawakaribisha, ili kutangaza mambo mazuri yanayofanywa na Manispaa ya Iringa na mkoa mzima wa Iringa," alisema.

Mwenyekiti wa IPC, Frank Leonard alimpongeza meya huyo na halmashauri yake kwa hatua hiyo.

Alisema mwaka 2022 ulikuwa wa ushirikiano, hivyo kuomba ushirikiano huo uendelee mwaka huu wa 2023 ili kuleta maendeleo kwa jamii.

Leonard pia alimshirikisha meya huyo mipango mbalimbali inayotkelezwa na IPC, ikiwamo mpango mkakati wa miaka mitano unaoangazia maeneo matatu muhimu ya afya ya mama na mtoto, elimu pamoja na demokrasia na utawala bora.

# Wadau wapendekeza kuwe na bajeti ya utafiti shuleni

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

MRATIBU wa Taasisi ya Young Scientist Mkoa wa Pwani, Paul Balibate, amesema ili kuongeza idadi ya wanasayansi, kuna haja wakuu wa shule kutoa ushirikiano kwa walimu wanaohusika kushirikiana na wanafunzi katika kuboresha mawazo ya utafiti.

Balibate aliyasema hayo mwishoni mwa wiki alipozungumza na Nipashe kuhusu wanasayansi chipukizi kwenye shule zilizopo Mkoa wa Pwani ambao wamekuwa wakiibua mawazo yao ya kufayanyia utafiti na kushindanishwa na shule zingine kwa usimamizi wa taasisi hiyo.

Alisema wapo baadhi ya wanafunzi mawazo yao yamekuwa yakishinda ngazi ya kitaifa na wanapofika hatua ya kwenda kuyafanyia utafiti, wengi wamekuwa wakiishia njiani kutokana na kushindwa kumudu gharama.

"Mawazo yanakuwa mazuri na yanakidhi sifa na kuchaguliwa lakini wanakwama kwenye hatua ya utekelezaji ambayo ni kukusanya data na Taasisi ya Young Scientist Tanzania haina bajeti kwa ajili ya mradi wowote, hivyo fursa hiyo kutotumiwa na wanafunzi na walimu kufikia hatua ya juu," alisema.

Alisema uibuaji wa mawazo ya kuyafanyia utafiti ni moja ya hatua ya kuongeza uwezo wa kufanya utafiti na kuandaa wanasayansi bora nchini, pia walimu wanapata nafasi ya kuongeza ujuzi.

Baliabate aliwaomba wadau wa elimu kutoka maeneo mbalimbali kujitokeza kufadhili mawazo ya miradi inayoibuliwa na wanafunzi ili kuwawezesha ambao wamekuwa wakikwama kutokana na kukosa fedha za kuendeleza mawazo yao.

Alisema taasisi hiyo kwa Mkoa wa Pwani inaendelea kuhamasisha shule mbalimbali kujitokeza kushiriki katika mashindano hayo huku akibainisha kuwa wanaoshiriki siyo wanafunzi wa masomo ya sayansi pekee, bali pia wa masomo ya sanaa.

"Mwaka huu tunatarajia kuwa na maonyesho ya kimkoa, wanafunzi watapata fursa ya kuonyesha miradi (mawazo) waliyoyaibua ambayo yatashindanishwa ngazi ya kitaifa na hii itakuwa fursa kwa shule nyingi zaidi kushiriki," alisema.

Wanafunzi wawili wa kidato cha tatu katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Kibaha, Gloria Tibaijuka na Halima Muhunzi mwezi Desemba mwaka jana walikabidhiwa zawadi mbalimbali baada ya kuibuka washindi wa jumla katika shindano la wanasayansi chipukizi.

Utafiti wao ulihusu kutambua tatizo la upungufu wa upatikanaji wa maji kwenye chanzo cha maji cha Mto Ruvu ambao unasambaza maji kwenye mikoa mitatu ya Pwani, Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Morogoro wakilenga kutafuta suluhisho la tatizo hilo.



## Shirika latoa kadi iCHF watoto 326 Simanjiro

**Na Allan Isack,** SIMANJIRO

SHIRIKA lisilo la kiserikali la AKO Tanzania Community Support limetoa msaada wa kuwalipia Bima ya Afya ya Jamii iliyoboreshwa ya (iCHF) kwa watoto 326 wa vijiji vya Kambi ya Chokaa na Losoito wilayani Simanjiro mkoani Manyara.

Mkurugenzi wa AKO Tanzania, Hilda Kimath, alisema shirika hilo limewalipia watoto hao Sh.milioni 1.9 ili wapatiwe bima hiyo.

Mratibu iCHF, Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara , Ibrahim Yeo, amekiri kwamba watoto 326 wa vijiji hivyo viwili kulipiwa kiwango hicho cha fedha kwa ajili ya bima hiyo.

Hivyo aliwashukuru viongozi wa shirika hilo kwa kuwalipia kiasi hicho cha fedha watoto hao ambao watapatiwa huduma ya matibabu bila kutozwa gharama yoyote.

Mkazi wa Kijiji cha Kambi ya Chokaa, Elias Loshilaa, aliwashukuru viongozi wa shirika hilo kwa kufanikisha jambo hilo kwa kuwa watoto hao sasa hivi watakuwa na uhakika wa kupata matibabu endapo wataugua.

Alisema: "Mashirika mengine yasiyo ya kiserikali yaige mfano wa AKO Tanzania kwa namna wanavyohudumia jamii hasa zilizo pembezoni ambazo zina uhitaji mkubwa".

**Mratibu iCHF, Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara , Ibrahim Yeo, amekiri kwamba watoto 326 wa vijiji hivyo viwili kulipiwa kiwango hicho cha fedha kwa ajili ya bima hiyo.**

# Wanaobeza mchakato Katiba mpya wamchefua Askofu

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Elim Pentekoste Tanzania (KEPT), Peter Konki, amewashukia watu wanaobeza kuendelezwa kwa mchakato wa kupatikana kwa Katiba mpya.

Kadhalika amewaonya watu wanaohusika kuibeza Katiba ya mwaka 1977, akisema waache tabia, huku akisema wawape nafasi serikali kuendelea na mchakato huo pale watakapoona kama kuna uhitaji.

Konki aliyasema hayo jana Mjini Babati mkoani Manyara, baada ya kuwekwa wakfu kuendelea kuwa Askofu Mkuu wa Kanisa hilo kwa awamu ya nne.

Hata hivyo alisema ni vizuri kupata Katiba mpya lakini kwa kufuata mchakato ulioko ambao unaratibiwa na serikali.

"Mchakato uendelee ila tusitukane serikali tuache mchakato wa katiba mpya uendelee kwa kufuata utaratibu unaotakiwa,"alisema Konki.

Aidha, alisema hakuna haja kwa watu kutukana Katiba inayotumika sasa kwa kuwa hakuna hoja ya msingi ya kuibeza kwamba cha msingi wanapaswa kuwa wavumilivu.

"Naomba tuvute subira ili serikali iendelee kuchakata mchakato wa kupatikana kwa Katiba mpya kwa amani," alisema.

Vile vile alisema Katiba iliyoko haipaswi kubezwa kwa kuwa ina mambo mengi mazuri yakiwamo uhuru wa kuabudu na kuwapo kwa demokrasia ambayo inasaidia kuwa na amani nchini.

Hivyo, alitumia fursa hiyo kuwaomba Watanzania kuipenda nchi yao na aliwatakia kheri ya Sikukuu ya Mwaka Mpya Rais Samia Suluhu Hassan, Makamu wake, Dk.Philip Mpango, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa na Watanzania.

Mchungaji Abiud Solomon kutoka Tarime, alisema askofu huyo ataleta mabadiliko makubwa kwa kuwajengea shule na zahanati.

Mwenyekiti wa Vijana, Daniel Sarwat, alisema ana imani kubwa na kiongozi huyo kwa kuwa ameahidi kujenga vyuo vya Kiingereza, shule za sekondari na hospitali mkoani Dodoma.



Ofisa Rasilimali Watu wa Kiwanda cha Mati Super Brands Limited, Doreen Raphael (wa pili kushoto), akikabidhi misaada kwa Muuguzi Msaidizi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Josephine Mosha, mwishoni mwa wiki. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# H'shauri yakabidhi pikipiki 18, mashine kutotoresha vifaranga

**Na Allan Isack,** ARUMERU

HALMASHAURI ya Meru wilayani Arumeru mkoani Arusha, imekabidhi pikipiki 18 za Sh. milioni 45 kwa vikundi vitatu vya vijana pamoja na mashine ya kutotolea vifaranga ya Sh. milioni nne.

Kutolewa kwa vitu hivyo ni sehemu ya mkopo wa Sh.milioni 237 uliotolewa na halmashauri hiyo kupitia mapato ya ndani na kutoa kwa kundi la vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Mbunge wa Arumeru Mashariki, Dk. John Pallangyo, aliwataka vijana hao kutumia pikipiki hizo kujikwamua kiuchumi kuzitunza na kuzingatia sheria za usalama barabarani ili kuepuka ajali zisizokuwa na tija.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Meru, Jeremia Kishili, alisema halmashauri hiyo itaendelea kukusanya mapato na kupeleka maendeleo kwa wananchi kama ilivyokuwa lengo la serikali kuwahudumia watu wake.

Pia alitumia fursa hiyo kwa kutoa wito kwa waendasha pikipiki kuwa waadilifu na kutumia vyombo hivyo kujiletea maendeleo kwa kuongeza kipato cha familia na jamii kwa ujumla.


Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Meru, Zainabu Makwinya, alisema ushirikiano kati ya madiwani na wataalamu umesaidia kuhakikisha mapato yanakusanywa na kufanikisha utoaji wa mikopo hiyo na utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Alisema licha ya halmashauri hutoa msaada huo aliomba Ofisi ya Waziri Mkuu kutoa vifaa vingine ikiwamo vifaa kama vyerehani kwa vijana ili wajiajiri na kujikwamua kiuchumi.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Meru, Flora Msilu, alisema vifaa hivyo vya Sh.milioni 53 vimenunuliwa kupitia mapato ya ndani ya halmashauri na ni sehemu ya mkopo usiokuwa na riba.

Alisema Sh. milioni 237 zilitolewa kwa vikundi vya wanawake 36, vikundi 18 vya vijana na vikundi vinne vya watu wenye mahitaji maalum kwa kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka huu wa fedha 2022/2023.

Katibu wa Siasa na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Meru, Kennedy Mpumilwa, aliipongeza halmashauri kwa kuwawezesha wanawake, vijana na watu wenye ulemavu ili wajikwamue kiuchumi.



# Askofu akemea wanaotaka utajiri kwa njia ya mkato

**Na Oscar Assenga,** TANGA

ASKOFU Mkuu wa Kanisa la Free Pentecostal Church, Stivie Mulenga, amewataka vijana kufanya kazi kwa nguvu na kwa bidii badala ya kutamani utajiri wa haraka, maisha mazuri, magari na fedha.

Alisema baadhi ya vijana wamekuwa wakijiingiza kwenye shughuli ambazo siyo halali ikiwamo kutumia nguvu za giza, ushirikina na ujambazi ili kuwa na maisha mazuri kitendo ambacho kitawaingiza kwenye hatari ya maisha yao.

Aliyasema hayo juzi katika Kanisa la Free Pentecoasal Church Novelty jijini Tanga, wakati wa ibada ya kusherehekea Sikukuu ya Mwaka Mpya.

Alisema wamekuwa wakitumia njia hizo, wakidhani zinaweza kuwasaidia kupata fedha pamoja na maisha bora hivyo alitoa rai kwa kundi hilo, kutumia fursa zilizoko kujikwamua kiuchumi.

Kadhalika aliwataka vijana hao watumie rasilimali zilizoko nchini ikiwamo ardhi, maziwa, bahari kujipatia kipato halali ambacho kinaweza kuwakwamua kiuchumi.

“Ulimwengu wa sasa wako vijana ambao wanatamani utajiri wa haraka kwa kutumia njia za mkato, niwaombe waache kufanya hivyo badala yake watumie fursa zilizoko kujiletea maendeleo na siyo kutumia njia mbaya,” alisema.

Katika hatua nyingine, aliwataka wahubiri kuwahubiria watu maneno ya sahihi na sio vinginevyo.

“Unakuta kuna wahubiri wanawaambia watu waombe kitu chochote watapewa kwa masharti akitoa hiki atapata kitu kingine hiyo siyo sahihi lazima tuhimize watu kufanya kazi kwa bidii,” alisema Askofu Mulenga.

Akizungumzia kikundi cha wezi wanaotambulika kwa jina la watoto wa ibilisi, alisema chimbuko lake ni kwa wazazi kwa kuwa wamekosa nafasi ya kuwalea watoto wao hivyo kuwapa uhuru wa kufanya mambo wanayotaka.

Alisema kuna umuhimu kwa wazazi na walezi kubadilika na kuhakikisha wakarudi kwenye mstari wa kuwalea watoto katika maadili sahihi ambayo yanampendeza Mungu.



Mkurugenzi Mkuu Tume ya Taifa ya Umwagiliaji, Raymond Mndolwa, akitoa maelekezo kwa wataalamu wa tume ngazi ya mkoa katika skimu ya umwagiliaji ya Kirya juzi, baada ya kuvunja mkataba wa makandarasi wawili wa kampuni ya Engineer Plus na Petra wanaojenga mradi wa mfereji wa umwagiliaji wenye thamani ya Sh. bilioni 1.6 urefu wa mita 3,400 baada ya kushindwa kutekeleza. **PICHA: MARY MOSHA**

## REA yatuma salamu kwa makandarasi wababaishaji

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

MKURUGENZI Mkuu Wakala wa Nishati Vijijini (REA),Hassan Saidy, amesema hawatahusika kubeba majukumu ya aina yoyote ya mkandarasi ambaye atashindwa kutekeleza mradi wake kwa mujibu wa makubaliano ya mkataba waliosaini kati ya pande hizo mbili.

Aliyasema hayo jana jijini Tanga kabla ya kutia saini na makabidhiano ya mkataba wa mradi wa REA III na Mkurugenzi wa Kampuni ya Ok Electrical and Electronic Service Ltd, Mrisho Masud.

Mkoa huo utatumia zaidi ya Sh. bilioni 11 kutekeleza mradi huo wa REA III katika wilaya sita kati ya nane mkoani humo.

Aidha, alisema moja ya makubaliano kati ya REA na mkandarasi huyo ni kutumia rasilimali watu na vitu ndani ya eneo linalotekelezwa mradi, pia kuhakikisha wanatumia vifaa vyenye ubora ili kuondokana na kero ya kukataliwa katika utekelezaji wao.

“Hakikisheni kwanza makandarasi wote wanafanya kazi zao kulingana na mikataba kwenye kazi ambazo hazihitaji utaalamu tumieni vijana wa eneo husika kufanya kazi hizo, pia hakikisheni mnapofanya nao kazi muwalipe kwa wakati.

“Hatutalipia fedha kwa vifaa vya ujenzi visivyo na ubora kwa kuwa tunasisitiza kazi zifanyike kwa ushirikiano hasa kwa kuwashirikisha wenyeji na viongozi wa eneo husika,” alisema.

Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Tanga, ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashimu Mgandilwa, alisema serikali imedhamiria kujenga uchumi wa nchi na kwa mtu mmoja mmoja kwa kuendelea kujenga miradi mbalimbali ambayo inatoa ajira kwa vijana wanawake.

Alisema: “Fedha za mradi huu ni Sh. bilioni 79 zilizotolewa kwa nchi nzima kutekeleza miradi ya REA III, tumepata bahati ya kuletewa kiasi cha zaidi ya Sh. bilioni 11, mradi huu tumepewa utekelezwaji wake ukamilike kwa miezi 18,” alisema Mgandilwa.

Mgandilwa alitoa tahadhari kwa viongozi na wananchi na watakaojaribu kuharibu miundombinu hatua kali zitachukuliwa kwa kuwa hatakuwa na nia njema na serikali kwa kuwa atakuwa ametenda kosa la kuhujumu uchumi.

# Wanaouza ardhi kiholela waonywa

**Na Mary Mosha** SAME

SERIKALI wilayani Same mkoani Kilimanjaro imetoa onyo kwa wenyeviti wa vijiji na vitongoji katika Kata ya Ruvu, Makanya, Hedaru na Mabilioni, kuacha tabia ya kugawa na kuuza ardhi kiholela ili kuepukana na migogoro kati ya wakulima na wafugaji.

Onyo hilo limetolewa siku chache baada ya Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa, kuwaagiza wakuu wa mikoa na wilaya nchini, kuhakikisha wanakutana na wakulima na wafugaji kufanya mazungumzo ili kumaliza migogoro kati ya pande hizo mbili.

Aliyasema hayo jana Mkuu wa Wilaya ya Same, Edward Mpogolo, wakati wa mkutano wa hadhara uliofanyika katika Kijiji cha Ruvu Marwa Kata ya Ruvu kwa lengo la kutatua mgogoro wa wakulima na wafugaji.

Alisema kuwa chanzo cha mgogoro huo ni baadhi ya viongozi wa vitongoji kumega maeneo ya wafugaji katika eneo la pori tengefu na kulitumia kwa ajili ya shughuli za kilimo, hivyo amewaonya viongozi kuacha tabia ya kujihusisha na ugawaji wa ardhi.

“Lile pori tengefu la Ruvu lililoko tangu mwaka 1974 ambalo haliruhusiwi kufanyika kwa shughuli za ufugaji lakini viongozi wamekuwa wakigawa maeneo hayo kinyemela kwa ajili ya shughuli za kilimo na kupelekea kuwapo kwa migogoro,” alisema Mpogolo.

Mkuu huyo wa Wilaya alisema katika Kata ya Ruvu viko vijiji vinne vya Ruvu Marwa, Mrefejini, Muungano na Jiungeni na Kata ya Makanya, Hedaru na Mabilioni viko kwenye eneo la pori tengefu.

Alisema hivyo wanamwomba Rais Samia Suluhu Hasan kupitia mawaziri kuangalia namna ya kuacha baadhi ya vijiji vilivyoingia kwenye pori tengefu kusomeka kama vijiji ili kuiwezesha halmashauri kupanga matumizi bora ya ardhi.

“Tunashindwa kupanga matumizi bora ya ardhi katika vijiji tisa vya kata hizi, kutokana na maeneo yake kusajiliwa ndani ya pori tengefu na nimewapiga marufuku viongozi kuendelea kugawa maeneo hayo na kumega mashamba yaliyoko katika Mto Ruvu kwa kuwa kufanya hivi bila kuwa na matumizi bora ya ardhi italeta shida badaaye,” alisema Mpogolo.

Pia walimwomba Rais Samia kupitia mawaziri kuangalia maeneo ambayo pori hilo tengefu litaonekana kuwa na umuhimu wa kuendelea kubaki yaendelee kubakia kwa kuwa wanyama kama vile tembo wanatoka Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi kufuata maji Mto Ruvu.

Alisema katika Wilaya ya Same, kuna wanyama kuna umuhimu wa kutengwa maeneo kwa ajili ya shughuli za ufugaji, kilimo pamoja na wanyama pori.

Aidha, aliwaomba viongozi wa kimila wakiwamo viongozi wa mabaraza ya wafugaji na wakulima kukaa pamoja na kuhakikisha wanadhibiti migogoro hiyo, kadhalika aliwataka wananchi kuepuka kuchukua sheria mkononi.

Kamanda wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Wilaya ya Same, Jane Mgaya, aliwaonya viongozi wa vijiji, vitongoji na kata kuacha tabia ya kuchukua fedha kwa wananchi ili kuwapatia ardhi kinyume na sheria na utaratibu.

Alisema taasisi hiyo iko macho na haitamvumilia kiongozi atakayebainika kuchukua fedha, hivyo ikidhibitika atawajibishwa kwa mujibu wa sheria.

Mwanasheria wa Halmashauri hiyo, Upendo Kivuyo, alisema eneo la Pori Tengefu la Ruvu, lilitangazwa rasmi 1974 na kwa sasa mapori tengefu nchini yamekumbwa na tatizo la kuharibiwa na wananchi ikiwamo kuingiliwa makazi.

Alisema ili kunusuru mapori hayo, kifungu cha 16 cha Sheria ya Wanyamapori Namba 05 ya mwaka 2009 kinampa nafasi waziri mwenye dhamana kunusuru maeneo ya mapori tengefu kwa kushirikiana na wizara zingine na wadau wote kwa kufanya tathmini ya maeneo hayo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Januari 3, 2023
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



## Mapinduzi ya elimu kuboresha usomaji yaanza kwa kasi Pwani

Ukurasa 14



## Hili lisipuuzwe mwaka huu, linaua wanafunzi, mabinti

Ukurasa 15

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

# Kero ya kila mwaka hata 2023 Watanzania wametinga nayo



Wanawake wilayani Temeke jijini Dar es Salaam wakiwa kwenye foleni ya kutafuta maji. **PICHA: MAKTABA**

MIAKA ya hivi karibuni kumekuwa na kero ya foleni na msongamano mkubwa kwenye maeneo mengi ya kupata huduma. Hii ni kuanzia madarasani, kwenye huduma za maji, stendi za mabasi, daladala, vivuko, hospitali na mabasi ya mwendokasi. Kila sehemu ni watu kusongamana na kujazana na kuweka mstari ili kusubiri huduma.

Hali hii inawapa changamoto kubwa wanajamii wote bila kujali umri au kabila au eneo anakotokea. Mambo haya hayajaanza leo bali ni tatizo la kila mwaka tena linakua mwaka huu na jamii inavuka nalo mwaka 2023.

Kwahiyo ni kuikubali hali na kujiandaa kukabiliana na foleni na misongamano katika mwaka ujayo kwa maana 2023 inavyoingia hakujawa na ufumbuzi wa kuziondoa na pengine changamoto hiyo ikawa kubwa zaidi mwakani kuliko ilivyo sasa kwa vile idadi ya watu inazidi kuongezeka kuanzia wenye makazi na wageni wanaoingia kila siku mijini.

Kunapokuwa na foleni na misongamano ya aina hii katika maeneo ya huduma ni ngumu kuzikwepa maana hata ikitafutwa njia mbadala kwa mtu mmoja hakutakuwa na tija kwa sababu madhara ya foleni na msongamano lazima yatamkuta ndugu yako au yeyote wa karibu, rafiki na yeyote kwenye jamii yako Mfano, asipokwenda shule mtoto wako wa ndugu yako atakwenda na kukutana na foleni na msongamano. Kadhalika usipokwenda hospitalini basi mtoto wako au ndugu yako yeyote yule atafuata matibabu na kupata adha hiyo iwe ni kumwona daktari, maabara, chumba cha x-ray na kurudisha matokeo ya vipimo kwa daktari.

Ukisema unaamua kununua na kutumia gari binafsi ili kuepuka msongamano kwenye daladala au basi la umma, wazazi wako jamaa zako watapanda daladala au mwendokasi na kupata kadhia hiyo ya foleni na msongamano. Wakikosa hao basi mjomba au ndugu yako mwingine atapata kadhia hiyo ya foleni na msongamano. Kwa maneno mengine foleni na msongamano lazima inagusa jamii nzima ya waliokuwa vijijini na mijini na kwa kuwa huduma wanazozifuatilia zina watu wengi.

**MADHARA YA USUMBUFU**

Kwa sasa kuna madhara mengi yatokanayo na misongamano hiyo katika maeneo mbalimbali ya kupata huduma ikiwa ni pamoja na kupoteza muda mwingi kusubiria kupata unachotaka, kupoteza muda ambao ungetumika vizuri kwa ajili ya shughuli za kuzalisha mali.

Mfano muda mwingine mwanajamii huhitajika kuanzia kuwahi saa10 au

11 asubuhi ili kuwahi namba za kutibiwa kumuona bingwa. Kisha hutakiwa kufika hospitalini saa 3:00 na kuanzia hapo hukaa kwenye foleni kwa muda wa saa tatu mpaka sita akisubiri kutibiwa na kumaliza matibabu yake jioni.

Kwa maana ya kutumia siku nzima bila kufanya kazi ya kumwingizia kipato , siyo peke yake pengine amesindikizwa na jamaa

INAENDELEA UK. 18

ELIMU

NA YASMINE PROTACE, PWANI

# Mapinduzi ya elimu kuboresha usomaji yaanza kwa kasi Pwani



Mkufunzi wa mafunzo ya shule bora, Raymond Kayaga, akizungumza na wanahabari kuhusu mradi huo. **PICHA: JASMINE PROTACE**

POPOTE elimu inapotolewa inalenga kuwawezesha watoto kupata maarifa bora na kuwawekea mazingira salama ya kujitegemea na kumudu kuendesha maisha yao kupitia utaratibu wa kujifunza na kufundishwa kwa ngazi mbalimbali.

Katika kuunga mkono juhudi za elimu na kupata maarifa bora kwa watoto wote, mradi wa shule bora unaodhaminiwa na Uingereza unalenga kushirikiana na serikali kuinua kiwango cha elimu jumuishi na kuweka mazingira salama ya watoto wote kujifunza.

Kwa Pwani, mratibu wa mawasiliano wa mradi wa shule bora mkoani hapa, Raymond Kayago, anasema mradi huo, ulioanza mwaka jana, utafanyika kwa miaka sita na ukiwa na matokeo bora utaongezewa miaka mitatu.

Akizungumza na Nipashe kuhusu mradi huo, anasema utafanya maboresho yatakayowezesha kila mtoto kupata msingi bora wa elimu ya awali hadi darasa la saba.

Olva Kapaya ambaye ni mratibu wa mradi mkoa wa Pwani, anasema hajawaacha walimu wanafunzwa mbinu za kufanikisha watoto kujua kusoma na kuandika.

Kupitia mradi huo, madarasa ya utayari yanaanzishwa katika sehemu zenye changamoto, anasema.

"Kama kuna maeneo mtoto hawezi kuvuka barabara, vimeanzishwa vituo vinavyomsaidia. Changamoto zitakaposhughulikiwa, wakati watoto wengi wakijiunga na kuendelea na masomo, matokeo ya elimu Tanzania yatazidi kuwa na changamoto nyingi." Anasema Kapaya.

Aidha, anataja asilimia nane ya wanafunzi katika elimu ya msingi kuwa ndiyo wanaofika kiwango cha taifa cha kujua kusoma kwa ufasaha, wakati asilimia 12 wanafikia kiwango cha taifa cha kujumlisha na kutoa.

Hatua hiyo, inachangiwa na ongezeko la mahitaji ya elimu msingi sambamba na kuongezeka idadi ya watu wakihitaji kubadilisha uwiano walimu na wanafunzi, ambako sasa ni wastani wa wanafunzi 62 kwa mwalimu kwenye shule za msingi za serikali, anasema Kapaya.

**SHULE BORA**

Kapaya anasema uzinduzi wa shule bora unalenga matokeo katika ngazi ya kitaifa na pia unatoa msaada wa kiufundi kwa serikali.

Anataja utekelezaji wa programu ya lipwa kwa matokeo 'education program for result 11' akisema: " malengo ya utekelezaji wa kitaifa yanapangwa na serikali na wahisani huku fedha zikitolewa kulingana na malengo yaliyofikiwa.

Anasema shule bora itafadhili matokeo muhimu yatakayotokana na vigezo vilivyothibitishwa kutoka katika mradi wa programu ya lipwa kwa matokeo ambavyo vitatumiwa kutoa fedha.

Aidha, Kapaya anasema kwa msaada wa Uingereza kupitia mfuko wa UK Aid, itagharamia Paundi milioni 89 sawa na Shilingi bilioni 271 na zitafanya kazi katika ngazi zote za mradi hadi 2027.

Kapaya anasema mradi wa shule bora itafanya kazi moja kwa moja na uongozi wa mkoa na halmashauri katika mikoa tisa yenye changamoto nyingi kama ilivyopendekezwa na kukubalika na serikali.

"Mradi unalenga kuweka mikakati sahihi na kutafuta suluhisho ili kuhakikisha watoto wenye ulemavu, wanaoishi katika mazingira magumu, wasichana na wavulana wanapata elimu katika mikoa ya Tanga, Pwani, Dodoma, Singida, Kigoma, Katavi, Simiyu, Mara na Rukwa," anasema na kwamba unalenga kufikia watoto takribani 4,000,000, nusu wakiwa wasichana.

**YANAYOLENGWA**

Kapaya anasema mradi wa shule bora unalenga mambo makuu manne ambayo ni kujifunza, kufundisha, ujumuishi na kujenga mfumo.

> "Mradi unalenga kuweka mikakati sahihi na kutafuta suluhisho ili kuhakikisha watoto wenye ulemavu, wanaoishi katika mazingira magumu, wasichana na wavulana wanapata elimu katika mikoa ya Tanga, Pwani, Dodoma, Singida, Kigoma, Katavi, Simiyu, Mara na Rukwa," anasema na kwamba unalenga kufikia watoto takribani 4,000,000, nusu wakiwa wasichana.

Ujumuishi ni kipaumbele cha shule bora ambapo mradi utawatupia macho kwa karibu wanafunzi wa kike, wanafunzi wenye mahitaji maalumu na wale wanaotoka katika mazingira magumu.

"Utashughulikia mambo yatakayowezesha watoto kuwa shuleni katika mazingira bora na salama ili kuwapa nafasi ya kujifunza na kuendelea na sekondari." Anasema Kapaya. Abubakari Mpili Mwalimu wa Shule ya Msingi Kibiti, anasema baadhi ya watoto walikataa kusoma wakibaki nyumbani na katika kukabiliana na changamoto hiyo, walinunua vitabu vya hadithi na kuwasimulia na sasa wameacha utoro na kurejea darasani.

Ofisa Elimu Mkoa wa Pwani, Sara Mlaki, anasema Mkuranga vimeanzishwa vituo 38 vilivyoandaliwa kutoa elimu kuelekea msingi na kwamba ni kunatokana na watoto wengi wa shule za awali kutoka mbali mno na shule,

Ofisa Elimu Kata ya Njia Nne, Mkuranga Bakari Jiri, anasema katika wilaya hiyo vimeanzishwa vituo 38 ambavyo vinatoa elimu ya msingi kwa watoto wa karibu na maeneo vilipo.

Aidha, kuanzishwa kwa vituo hivyo ni kuwawezesha watoto wanaosoma elimu ya awali kunufaika na elimu karibu na wanapoishi.

"Watoto wa elimu ya awali hawawezi kutembea umbali mrefu kwenda shule hivyo tukaona ni bora kujenga vituo hivyo karibu na maeneo wanapoishi na baadaye wakajiunge na elimu ya msingi," anasema.

Anasema mwaka 2021 wanafunzi wa darasa la nne asilimia nane hawakufanya mitihani kwa sababu ya utoro na kushinda njaa shuleni.

Anasema baada ya kufanya utafiti ikagundulika tatizo ni ukosefu wa chakula na iliandaliwa programu ya kuwapa chakula, wazazi nao wanachangia chakula, pia kulima mazao ya chakula shuleni.

Anaongeza kuwa programu nyingine ya kudhibiti utoro, ni kufunga TV 30 katika shule za mfano ambapo walimu wanatumia TV kufundishia na hiyo imesaidia watoto kwenda shule.

Anaongeza kuwa utafiti walioufanya waligundua kuwa watoto wa darasa la pili hawataki kwenda shule na wakabaini chanzo ni kukaa mitaani' na kuangalia TV za vibandani.

Anasema baada ya kubaini watoto kukimbilia mitaani' kuangalia TV, wanaziweka katika baadhi ya shule ili wajifunze kupitia katuni na sasa wametulia darasani.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Hili lisipuuzwe mwaka huu, linaua wanafunzi, mabinti

Heri ya Mwaka Mpya 2023 wapenzi wa TESA. Karibuni tena kusoma kijarida hiki mahususi kuelimisha, kutoa taarifa, teknolojia, elimu na sayansi.

Aghalabu unapomalizwa mwaka ukitazama au ukisikiliza hoja na ujumbe unaohusu utetezi wa haki za watoto kubwa linalozungumzwa zama hizi ni kunyanyasa, kubaka, kulawiti, ndoa na mimba za utotoni, wakilengwa zaidi wasichana na kuhimiza kukomesha.

Kampeni hizi zinafanyika wakati Teknolojia ya Habari na Mawasiliano IT na TEHAMA imewapa 'elimu mbaya' watoto wadogo hasa wa shule za msingi ambao huangalia vitu vingi kuanzia matendo ya ngono, uzazi, njia za kuzuia na kuharibu mimba na mengine ambayo hawakutarajiwa kuyafahamu kwa namna yoyote katika umri wao mdogo.

Wanatumia simu, kompyuta kwa kuangalia youtube, 'kupakua App' TV za mtandaoni, flash na hata CD na kwenye mitandao wanayoitaka hutazama mambo mengi na kuonyeshana huku jamii ikiendeleza kuamini kuwa hawafahamu kitu walindwe na waepushwe na mambo makubwa kuliko umri wao.

Zama hizi kwenye mikusanyiko, suala la ulinzi wa watoto ni kipaumbele iwe majukwaa ya kijamii huzungumziwa kama ilivyo demokrasia, maendeleo, amani, magonjwa kama COVID-19 na kuondoa umaskini ulinzi wa watoto na elimu ya wasichana ni lazima kutajwa .

Hata hivyo, suala la athari au 'kitanzi' kinachonyonga na kuangamiza wasichana na wanawake wa Tanzania cha kutoa mimba hakijazungumziwa kwenye kuwalinda watoto.

Ukweli ni huo, watu wapende wasipende ni tatizo linalowahusu wanafunzi na mabinti mijini na vijijini lakini halisikiki. Ni zama za kulizungumzia tatizo hilo kwa vile shuleni mabinti na wanafunzi wenzao wa kiume wanajamiiana na wengi hupata ujauzito lakini hakuna wa kuwasaidia.

Baada ya kujifunza mengi kwenye youtube na TV za mitandaoni ni vyema pia wakazungumziwa ukweli kuhusu utoaji mimba na athari zake na kuwafahamisha kuwa ulinzi wa maisha yao dhidi ya unyanyasaji ni muhimu lakini pia wafahamu madhara ya kuharibu mimba.

Ni vyema mabinti, wanafunzi wa kike na kiume, vijana na wana jamii wafahamishwe kuhusu madhara yanayoambatana na utoaji huo ili kuvunja ukimya.

Wanafunzi wengi hutolewa mimba kienyeji, ni waathirika wa tatizo hilo. Maisha ni magumu utawasikia wanafunzi wakisema na kwamba ndicho kinachowalazimisha kujamiiana ili kujikimu. Inawezekana katika umri wa chini ya miaka 18, wamekutana na wanaume kadhaa na kupitia kwenye kutolewa mimba.



Kuzungumza kuhusu utoaji mimba za utotoni na elimu pana kuhusu athari zake ni muhimu kwenye ulinzi wa watoto. **PICHA: MTANDAO**

Suala hili lisipuuzwe lisemwe sambamba na juhudi za kuhimiza ulinzi wa watoto, kuwaepusha na mimba na ndoa za utotoni, ubakaji, uhusiano na kujamiiana baina ya mwanafunzi iwe wa sekondari au shule za msingi.

Fedha limekuwa suala muhimu kwa wasichana ili kujikimu na wamelazimika kushirikiana na wanaume wengi na hulazimika kuharibu ujauzito kila mara licha ya kufahamu kuwa ni jinai na hairuhusiwi.

Tanzania kama zilivyo nchi nyingi za Afrika za Kenya, Uganda na Nigeria utoaji mimba ni kosa la jinai na hufanyika tu kuokoa maisha ya mjamzito kwa uthibitisho wa madaktari.

Ibara ya 230 ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai inaruhusu utoaji mimba kufanyika ili kuokoa maisha ya mjamzito yanayoweza kuhatarishwa na mimba aliyobeba na si vinginevyo.

Aidha, ibara ya 16 ya sheria hiyo kuanzia kifungu cha 150 hadi 152 inakataza kutoa mimba na adhabu kwa anayepatikana na hatia ni kifungo cha miaka saba jela na yeyote aliyesaidia kufanikisha mchakato huo, anafungwa jela miaka mitatu.

Hata hivyo, katika mazingira hayo mimba zaidi ya 405,000 hutolewa kila mwaka tena nyingi zikiharibiwa kienyeji na katika mazingira hatarishi ni takwimu za mwaka 2016 za Chama cha Madaktari Bingwa wa Wanawake na Afya ya Uzazi (AGOTA) na Shirika la Amref Health Africa.

Mashirika hayo yalifanya utafiti uliobaini kuwa takribani mimba 405, 000 huharibiwa kila mwaka nchini kwa njia zisizo salama.

Takwimu hizo za miaka kama saba iliyopita huenda zimeongezeka maradufu, lakini ukweli ni kwamba tatizo lipo na ni kubwa kutokana pia ukuaji wa TEHAMA unaowapa watoto fursa ya kufahamu mambo mengi ikiwamo ngono katika umri mdogo.

Wakati huo, utafiti ulipofanyika ulieleza kuna vifo vinavyotokana na ukosefu wa huduma, kutoka damu kupindukia, mambo kufanyika kienyeji pengine nyumbani, kukosa wataalamu na kwa ujumla kuharibu mimba kusiko salama. Hivi hali hiyo haiwalazimishi serikali, wanasiasa, viongozi wa dini na asasi za kiraia kuzungumzia jambo hilo hadharani na kulikemea?

Kadhalika masuala ya vifo vinavyotokana na kuharibika mimba siyo suala lenye ugumu kufahamika kwa kuwa takwimu za vifo vya wazazi hukusanywa kutoka katika hospitali kote nchini na Waratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto, hivyo lisiwe tena jambo la kificho bali ukweli usemwe.

Licha ya kwamba ni muda mrefu umepita tangu utafiti huo bado tatizo lipo na huenda linaongezeka kila wakati na ukweli sasa ni lazima usemwe.

Wanawake 405,000 ni idadi kubwa ikakaribia nusu milioni wanadaiwa kuwa huharibu mimba kwa njia ambazo si salama zinazohatarisha maisha yao kila mwaka ni vyema sasa suala hilo lisifumbiwe macho maana ni kitanzi kinachowanyonga wanawake wakiwamo wanafunzi.

Ili kupunguza njia mojawapo ya kuwasaidia ni kuzungumzia na kuhamasisha uelewa na mambo ya kujamiiana miongoni mwa watoto walio chini ya miaka 20 ili wawe na ufahamu na kujiepusha.

Kama AGOTA na AMREF Africa waligundua idadi hiyo miaka kadhaa iliyopita huenda waathirika ni wengi mno kwasababu hakuna anayeujua ukweli kwa vile mambo hayo hufanywa kwa kificho mno, umma uamke.

Ikumbukwe dunia hii ni ya ujasiriamali kuna waganga matapeli na wababaishaji mitaani wanaowasaidia mabinti na wanafunzi kuharibu mimba.

Wanafunzi na wasichana mitaani wanajitumbukiza katika mahusiano bila kujua athari za kujamiiana, kupata mimba na kuzitoa. Yote hiyo ni kwa sababu si wazazi wala walezi, walimu wala wataalamu wanaoweleza suala hilo.

**ELIMU IANZE SASA**

Ili kuondoa pengo hilo taifa liamke sasa lianze kufundisha watoto na vijana athari za utoaji mimba usio salama pamoja na kuhamasisha vijana kuacha kujamiiana katika umri mdogo ikibidi waajiriwe wataalamu wa afya shuleni.

Wasichana na wanafunzi hawajui athari na utoaji mimba kwani hufanyika kwa usiri mno na wakati mwingine bila utaalamu bali kwa kujifunza kupitia 'YouTube' wapo wanaotumia mti wa kisamvu wanatoboa wanawake mfuko wa uzazi, utumbo na kibofu. Yote haya yanaathiri afya, utaratibu wa viungo vya uzazi na hata kuleta kifo.

Kukiwa na utaratibu na mifumo ya kuwafundisha vijana, kusisitiza maadili, elimu ya kujitambua , kuacha kufanya ngono za utotoni na kuthamini afya zao shuleni, nyumbani na kwenye semina na mafundisho ya kidini huenda tatizo likapunguzwa.

Wanafunzi wanapaswa kufundishwa kuwa kutoa mimba ni hatari kwa kuwafahamisha wote mabinti mitani, shuleni, vijana wanawake na wanaume vijana kuwa utoaji unapofanywa kwa njia zisizo salama hata kwa kupewa dawa ambazo dozi hazifahamiki ni hatari. Wakati mwingine zinaweza kuchana mfuko wa kizazi, kusababisha damu nyingi kupotea na mwisho ni kufa kama hakuna msaada wa matibabu yanayostahili.

Wataalamu wawafahamishe wanafunzi na wasichana kuwa kila mara mama anapobeba mimba kizazi kinachoka hata kuwa dhaifu, hivyo kuhitaji kupata ushauri wa wataalamu kwa kila hatua na kuchunguzwa.

**DAWA MITAANI**

Wapo wanafunzi wanatumia dawa za kutoa mimba kama 'mesoprostal' wajue kuwa 'meso'ni hatari kwani waganga wa mitaani hawafahamu hali ya kizazi cha mhusika pengine hilo la dawa nalo likisemwa litapunguza balaa hilo.

Wapo wanaotoa mafunzo kwa wasichana wenzao shuleni au mitaani wakiwashauri kutumia 'meso kienyeji' kwa mfano kutumia dozi kubwa kwa kumeza, kuweka sehemu ya haja kubwa na vidonge vingine kwenye njia ya uzazi mbinu hiyo wataalamu wanasema ni hatari kwa sababu dozi ni kubwa kupindukia inaweza kusababisha kupasuka sehemu za haja kubwa, mfuko wa kizazi, kutokwa damu nyingi, kuharibika viungo vya uzazi na wakati mwingine kupoteza maisha.

Wanafunzi wafahamu kuwa dawa hizo huchochea uchungu kwa nguvu kubwa kwenye misuli ya mfuko wa kizazi na sehemu nyingine na kutishia maisha.

Ni vyema wanafunzi wakafahamu kuwa wao ni wazazi na wamama wa kesho hivyo kuharibu ujauzito na kupata maambukizi ya utoaji mimba huleta magonjwa na makovu yanayosababisha mirija ya mayai kuziba, kizazi nacho huwa na makovu yanayoweza kusababisha ugumba na kulinyima taifa watoto ambao ni nguzo na jeshi la kuleta maendeleo.

**DAWA ZA ASILI**

Baadhi ya wanafunzi wanatumia dawa za asili kama juisi ya mwarobaini, chai ya rangi yenye majani mengi, aloivera na majani ya migomba na kwamba kuna aina nyingine nyingi za majani machungu yanayoweza kutumiwa kuchochea uchungu na kuharibu mimba.

Lakini, ni kweli dawa hizo hutoa mimba? Hakuna taarifa za utafiti uliofanywa na kuhusu nguvu ya dawa hizo, hivyo hawezi kuthibitisha au kukanusha na kikubwa wanafunzi, mabinti mtaani wajiepushe na shida hizo ili kulinda afya na hatima zao.

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

# Kumbuka usalama wa chakula ni jambo linalokuhusu, jibidiishe



Kukataa kula vyakula vichafu sokoni kuanze na wateja, wasinunue bidhaa zilizotandazwa chini, chafu na mbovu. **PICHA: MTANDAO**

KARIBU mwaka mpya 2023, tunawatakia wasomaji wetu heri na furaha tele. Tunapoumaliza na kuuanza 2023 suala la usalama wa chakula ni jambo linalowahusu Watanzania wote kulisimamia ili kulinda afya za walaji wote.

Tatizo kubwa lipo na kuna haja ya kuanza mwaka kwa kufanya juu chini kulinda chakula watu wengi wanachokula. Kwa miaka kadhaa usalama wa chakula haulelekei kuwa kipaumbele jambo linalohitaji msukumo mpya 2023 na lisiwe jukumu la mtu au kundi fulani.

Kwa mfano wakulima wa mboga hujaza viautilifu vingi, mbolea za viwandani za chumvi chumvi na hata busta kwenye mchicha, matembele, spinachi, bamia, ngogwe na hoho tena kwa muda mfupi kabla ya kemikali kufyozwa na kumalizika na kuwauzia wala bila kujali afya wala hatima zao.

Mayai mnayowauzia walaji wakati mwingine kuku anapewa dawa, kadhalika nyama na maziwa pia. Licha ya kusoma maelekezo na kuzifahamu athari wapo wafugaji na wakulima wanaouza vyakula vyenye dawa za wanyama kwanini mnafanya hivyo?

Wakulima angalieni msiwaumize walaji hakikisheni mnaacha mazoea ya kuuza vyakula vyenye kemikali za sumu, anza mwaka kwa kuhakikisha kuwa chakula kinakuwa salama.

Taratibu kiafya zinakataza wanadamu kula dawa za wanyama na huelekeza kuacha kula mazao ya mifugo kwa siku tatu, saba hata mwezi kutegemeana na 'antibiotic' iliyotumika.

Kuanzia mwaka 2019 Juni 7 dunia ilianza kuadhimisha Siku ya Chakula Duniani hatua iliyokamilishwa na kupitishwa kwa Azimio namba 73/250 na Mkutano Mkuu wa Afya wa Umoja wa Mataifa, mwaka 2018.

Ni vyema wazalishaji wakazingatia kuwa usalama wa chakula kinacholiwa leo ndiyo msingi wa afya njema sasa na baadaye.

Afya za Watanzania zimevurugwa kwa kunywa au kula mazao yaliyochanganywa na 'antibiotic' za wanyama, ndege na nyama na mayai yenye dawa za mifugo pamoja na viuatilifu vya sumu kwenye nafaka na mboga.

Ukweli ni kwamba endapo unachokula leo mtu si salama huenda miaka ijayo afya yake ikaathirika pengine kwa kuugua magonjwa muda mfupi baada ya kula au hata baada ya miaka kadhaa kwani kemikali hizi hazimuachi mtu salama.

Kuna madai kuwa kemikali kama ammonia zilizo kwenye mbolea ni chanzo cha saratani, lakini maadam hakuna utafiti uliofanyika si salama kuzungumzia mambo yanayoongeza hofu ila cha msingi ni kupunguza matumizi ya kemikali hatarishi kwenye vyakula au kuzitumia kwa mujibu wa masharti ya kitaalamu.

**VYAKULA VICHAFU**

Jijini Dar es Salaam na kwenye miji mingine nchini kulishwa uchafu ni jambo la kawaida, mathalani kuna madai kuwa mama na babalishe hutumia 'masalo' kuanzia nyanya, nyanya chungu, vitunguu, nazi, karoti, viazi, hoho, pilipili na kabichi.

Hivi ni vitu vilivyoanguka chini au kupondeka wakati wa kushusha vyakula sokoni. Huokotwa na waandaa vyakula hao au huvinunua kutoka kwa wajanja wanaokusanya 'bidhaa mbovu' sokoni ili kupata riziki.

Kwa mfano katika soko la Mbezi Dar es Salaam, wafugaji na wenye hoteli hugombania masalo ya nyanya, karoti, hoho na nyanya chungu na wapika chips na wenye mahoteli.

Yapo madai kuwa hoho zilizopasuka au kuharibika kutokana na ubebaji hununuliwa na kutumiwa kuandaa kachumbari, kadhalika nyanya chungu zilizonyauka au kuharibika, karoti mbovu zilizopasuka nazo ni dhahabu kwao.

Vivyo hivyo, kwa nazi zilizopasuka nyingine zikichafuka nazo ni dili pamoja na pilipili na nyanya mbovu zinazosagwa ili kuunga vyakula

Wafugaji wanaotaka bidhaa kama hoho, kabichi nyaya kulishia wanyama wao huambulia patupu baada ya wauza vyakula kuawazidi ujanja.

Kwa ujamla watu hula vyakula ambavyo huwa na imani navyo. Wanafumba macho maana hata huchafuliwa na vitu vingi kama vimelea vya magonjwa hasa masalo hayo ambayo huokotwa wakati mwingine chini au majalalani.

Zipo kemikali za sumu pia ambavyo huchafua chakula kama zamani dizeli ilikuwa ikichafua unga unaoswagwa kwenye mashine kabla ya ujio wa umeme.

Hata hivyo, pembejeo kama dawa za kuua magugu nazo kama zinatumiwa kinyume cha maelekezo ya kitaalamu zinaweza pia kutishia afya za walaji.

Lakini, kwenye masoko mengine vyakula huchafuliwa makusudi unaweza kukuta maharage, mahindi au nafaka nyingine zina mawe, mifupa, vinyesi vya mbuzi, kuku na makapi yakiwamo magunzi.

Wafanyabiashara wafahamu kuwa kuwauzia wateja vyakula vichafu vyenye vimelea ya magonjwa hasa kuwapa kachumbari za hoho, pilipili, matango na makabichi ya kuokota majalalani sokoni wanaweza kuugua magonjwa ya tumbo, kuhara au kuhara damu, homa ya matumbo, amiba nahata kupoteza maisha hasa mgonjwa anapokosa msaada na tiba mahususi.

Kemikali nazo ni chanzo cha saratani na magonjwa mengine ambayo mwisho wake ni kuumiza afya na kusababisha kifo.

Serikali ina jukumu la kudhibiti usalama wa chakula kulinda afya ya walaji ndiyo maana chakula kinachouzwa katika masoko Shirika la Viwango Tanzania (TBS) linawajibika kuvisimamia na kuchukua hatua hasa kunapokuwa na mambo yanayofanya watu kula vyakula vichafu.

Vyakula vinatandazwa chini sokoni, matunda yanalala juu ya madimbwi ya maji machafu mengine yako karibu na vyoo kwenye masoko mfano Buguruni, lakini uuzaji wa vyakula katika Soko la Urafiki nao ni wa hali duni mno, TBS iwajibike chakula kiwe salama.

Kama hali ya masoko makubwa inatisha vipi kuhusu usalama wa wanyama wanaofugwa kwa ajili ya chakula ili kupata nyama, mayai na maziwa wanafuga kwa kuzingatia kanuni bora za ufugaji? Ni nani anayewasimamia? Wapo wataalamu wa mifugo, uvuvi na kilimo kuangalia usalama huo?

**UVUVI HARAMU**

Baadhi ya taasisi za kiraia zinazofanyakazi baharini ikiwamo Sea Sense zinashuhudia uvuvi wa kutumia kemikali kama sumu za viwandani na hata mimea sumu mfano utupa.

Mmea huo unawekwa kwenye vilindi vya maji na kuwalewesha samaki, wengine hufa wakiwamo wakubwa na wadogo, swali ni je, wateja wanapouziwa samaki hao wanabaki salama?

TBS inapofuatilia wasafirishaji na wafanyabiashara na wahifadhi ili kuweka chakula katika hali salama na kulinda afya ya walaji, isisahau pia kusisitiza umuhimu wa masoko safi na salama jambo ambalo ni la muhimu zama hizi za usalama na ubora wa chakula.

Wateja nao wawe wakali wasinunue chakula kibovu ukifika sokoni nunua mchele,safi ulliochabuliwa , ulioko mahali pa kavu na ndani ya chombo safi siyo viroba vilivyoonyeshewa na mvua.

Acha, kununua matunda yaliyozagaa chini. Chagua ya kwenye kichanja acha kula matikiti machafu yasiyooshwa yanayofungwa kwenye nailoni au mafenesi yaliyofunganywa kwenye glasi za plastiki nani kayasafisha kabla ya kuyachambua, jiulize?

Unaponunua vyakula vilivyosindikwa soma maelezo na hasa tarehe ya 'kuexpire' kujua kama vimemaliza muda wa matumizi au kuharibika.

ELIMU

NA CHRISTINA MWAKANGALE

GIBSON KAWAGO

# Mbunifu anayetazama donge nono la milioni 70

• 'Anatibu' betri chakavu kuunda vifaa matata

TULITEMBEA kilometa 51 kutoka Mgama Iringa Vijijini kwenda Ihemi Wilaya ya Mufindi Mkoa wa Iringa kufuata sehemu ya kuchajia simu. Niliwaza sana na nikatafuta namna ya kulitatua. Tanzania tuna changamoto ya umeme hasa vijijini kila mahali kuanzia kwenye vituo vya afya, shuleni ili kutoa huduma."

Ni kauli ya kijana Gibson Kawago, mhandisi, anayezungumza na Nipashe kuhusu hatua aliyopiga, ikiwa ni miaka takribani saba tangu gazeti hili lilipofanya mahojiano naye, akipokea tuzo ya ugunduzi wa chaji ya simu ya umeme jua sola.

Anasema ndoto yake imetimia na inaishi kwa vitendo, kwa kuwa alichokitamani ni kuja na ubunifu mbadala wa kuzalisha umeme, akisema akiwa shuleni alikuwa anazibomoa na kuzisuka upya redio mbovu.

Aidha, alipofika chuo kikuu aliwasumbua sana wenye kompyuta akiomba kila mara azitumie kuingia mtandaoni kujifunza chanzo cha umeme wa betri.

Gibson sasa anamiliki karakana inayozalisha nishati ya umeme kwa kutumia vifaa chakavu ikiwamo betri za kompyuta ambazo huzipata kutoka kwa wanaokusanya taka wa mikoani.

"Nimezaliwa kijiji kinachoitwa Kinyanambo B, huko tulisafiri kwenda kuchaji simu kwa baiskeli. Mwanzo kabisa niligundua 'pawa benki,' nilivunjavunja hizi hizi betri nikapata powa benki." Nilipofika chuoni DIT -Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, nilisomea na kuwa na ujuzi," anasema Gibson.

Aidha, anaongeza kuwa asili ya familia yake ni Mafinga, eneo la Kinyanambo B akizaliwa Februari 18, 1995 huko, Sawala wilayani Mufindi, kwa sasa ni kati ya vijana 15 wa nchi 15 za Afrika, wanaowania Tuzo ya Afrika ya Uhandisi yenye ubunifu 2023.

Kwenye tuzo hizo zinazotolewa na Chuo cha Uhandisi cha Uingereza, Gibson anatazamwa kama kijana mbunifu anayebuni teknolojia rafiki ya kuzalisha nishati ya umeme.

Wakati huo huo akilinda mazingira na afya ya binadamu na kupunguza athari kwa wateja. Mshindi wa tuzo hiyo atajinyakulia Paundi ya Uingereza 25,000 takribani Shilingi milioni 70.

Gibson anasema ameamua kuja na wazo la kutengeneza umeme baada ya kubaini ni changamoto nchini na maeneo mengine hayajafikiwa na huduma hiyo hasa vijijini, akibuni nishati ya kuwasha taa za barabarani, majumbani, chanzo kikuu kikiwa betri chakavu za kompyuta.



Gibson Kawago anayeunda vifaa vya kielektroniki kutokana na betri chakavu za kompyuta mpakato. **PICHA: WAGA POWER PACK**

Hivi sasa Gibson anatengeneza kifurushi chake cha umeme alichobuni kiitwacho WAGA Power Pack, huku chanzo cha nishati ya kifurushi hicho ni betri zilizokusanywa na vijana kadhaa mitaani kisha kuzifikisha kwenye karakana yake.


"Niliishi na wazazi wangu huko Sawala ambako baba yangu alikuwa anafanya kazi. Mwaka 1997 alihamishwa kikazi na tukahamia Mafinga ambako nilisoma shule ya Msingi Upendo iliyoko Kinyanambo B. Nikiwa shuleni nilikuwa nikipenda kuokota injini au motherboard za redio mbovu na kujaribu kuunganisha.

"Siku zote nilikuwa nina imani ya kwamba nitakuja kujua kutengeneza vifaa vya umeme na kielektroniki. Ilipofika 2009 nilijiunga na Seminari ya Donbosco Mafinga kusoma sekondari. Nikiwa shuleni nilikuwa naishi maabara na kufanya majaribio," anasema Gibson.

Aidha, anasema hata wakati wa mgawo wa umeme mwaka jana, wapenzi wa kombe la dunia walitumia chanzo chake cha umeme kwenye simu na televisheni, ili kutazama mechi mbalimbali.

Pia nishati yake ni tegemeo kwa wenye vibanda vya ujasiriamali huko vijijini.

"Tanzania tunasema ajira hamna, lakini vijana kutoka mikoa kadhaa wananikusanyia betri za laptop na kuniletea Kariakoo au Machinga Complex Dar es Salaam, kwenye karakana. Tunazivunja na kutoa betri na kuchakata na kupata WAGA Power Pack," anasema Gibson.



"Hata katika vituo vya afya nako umeme haujafika wanahitaji mwanga, wanatumia umeme huu. Kupata betri chakavu au zilizokufa ni rahisi, fikiria Tanzania tuna vyuo karibia 40 na wanafunzi tuseme wote hutumia mpakato -laptop ambazo hazidumu na zinatupwa katika mazingira yetu".

"Mimi nazichukua na kutengeneza nishati lakini pia nimeokoa mazingira, kwa sababu betri hiyo ikitupwa ardhini itatoa kemikali ambazo zitasalia udongoni mtu akilima eneo hilo, kemikali zinaingia kwenye mazao, tunakula," anaonya mhandisi huyo.

**ALIKOTOKA**

Gibson anasema, hakutegemea masomo pekee darasani bali aliongoza pia kwaya na hapo ndipo akaanza kuimba nyimbo za Bongo Fleva huku akitumbuiza katika sherehe mbalimbali za kishule.

"Kiukweli nilipenda kutengeneza vyombo vya kielektroniki na kuchezea kompyuta. Tatizo lilikuwa nyumbani hatukuwa na uwezo wa kununua kompyuta na hivyo niligombana na wenye kompyuta kwa kuwa nilikuwa na hamu ya kujua mambo mengi.

"Juhudi zilifanikishwa pale niliporudi likizo nilikuwa najiunga na mafundi redio na simu hapa Mafinga na kuwasaidia kutengeneza simu za wateja. Mara kadhaa nilishindwa lakini siku baada ya siku nikaja kufanikiwa. Na hapo nikaanza kutafuta simu za marafiki na kwenda benki kupata 'wireless' ya bure ili nipakue michoro ya kielektroniki mtandaoni na kuangalia jinsi ya kutengeneza kupitia Youtube."

Anasema alijiunga na sekondari Julai 23, 2014 na huko akakutana na wabunifu wakubwa wanaojua kufanya majaribio ya kisayansi na vitendo.

"Sikukata tamaa nikaamua kuanza kukesha ili niweze kusoma masomo ya darasani na yangu binafsi. Januari 2016 nilimwomba mama nisiende kulima ili nitengeneza sakiti ya kuzima taa kwa kupiga makofi. Ila baada ya kuunga vitu vyote ikawa haifanyi kazi. Nilirudia na kufeli." Anasema.

Anaongeza kuwa akaamua kuachana na elektroniki lakini mama akamshauri asikate tamaa ajaribu ataweza baada ya wiki moja ya maumivu ya kufeli.

"Dada yangu Asnath aliolewa na bibi akawa anataka kuona jinsi harusi ilivyokuwa. Niliweka video kwenye simu na kwenda kijiji cha Ibumila huko Mafinga kuwaonyesha video hiyo ndugu zangu. Lakini betri ya simu iliisha na wakashindwa kuangalia. Niliumia na kufikiri jinsi gani nitalitatua hilo tatizo. Ndipo nikapata wazo kutengeneza chaja itumiayo nguvu ya jua.

"Nilirudi Mafinga na kutengeneza na nikijaribu kwenye simu ya baba ikakubali. Nilikwenda shuleni na kujiunga na klabu ya Sayansi, Teknolojia, Uhandisi na Hisabati (STEM).

Anasema ameshiriki mashindano ya Bits and Bytes, akiwakilisha wazo la kubuni chaja ya sola.

"Fainali zilifanyika niliibuka mshindi wa pili. Namshukuru Mungu kwa kuwa fainali niliingia na wahandisi wenye kampuni wakati mimi ni mwanafunzi pekee."

# Kero ya kila mwaka hata 2023 Watanzania wametinga nayo

INATOKA UK. 13

yake , wote hupoteza muda kwenye mabenichi. Mwisho ni kushuka kwa uchumi wa mtu binafsi na jamii na taifa.

Pia hali hii ya foleni na msongamano mikubwa huleta uchovu na manung'uniko kadha kwa kadha kwa baadhi ya wanajamii ambao ikiendelea hivyo kwa muda mrefu huathiriwa afya ya akili ya akili na kuongeza tatizo jingine. Kwani wengi hubaki wakinung'unika na kupiga kelele ili kupatiwa huduma.

Hilo hufanya baadhi ya wanajamii kuanza kugombana kwa ajili kugombania nafasi za mbele kwenye foleni au kukimbilia kuwahi nafasi kwenye daladala au mabasi huku wakirushiana maneno makali na hata kuvurugana.

Hali hii hufanya baadhi ya wanajamii kuumia na kushindwa kuendelea na shughuli zao za kujiingizia kipato ili kuendesha maisha yao na familia zao. Mwisho ni kushindwa kutoa mchango wao katika ujenzi wa taifa lao kuanzia kulipa ada, kuchangia maendeleo binafsi na taifa.

Zaidi foleni na msongamano hiyo imekuwa chanzo cha vitendo visivyofaa kwenye jamii kwa mfano utoaji wa rushwa ili kupata huduma kwa upendeleo bila kufuata foleni. Aidha, foleni na misongamano ya kwenye magari na mabasi mijini imekuwa ikitumiwa na baadhi ya wanajamii kuwaibia wenzao simu, vitu kwenye mabegi hasa wanawake na fedha. Na mwisho mambo yote haya kwa pamoja huathiri uchumi wa mwanajamii, kuanzia mapato, afya ya akili na kuongeza umaskini.



Msongamano usiokwisha Kariakoo mara nyingi unasababisha wateja na wafanyabiashara kushindwa kufurahia shughuli zao. **PICHA: EATV**

**CHA KUSAIDIA**

Kwanza jamii, watoa huduma, serikali, watafiti na wataalamu wa sekta mbalimbali washirikishwe kutafuta ufumbuzi wa changamoto au kero hii ya uwepo foleni na misongamano mikubwa katika maeneo ya huduma. Hii inaweza kufanyika kwa kufanya utafiti, kusikiliza maoni ya wananchi na wadau ili kuja na majibu ya namna bora ya kukabili tatizo hilo.

Pia kujifunza kutoka kwa mataifa mengine jinsi walivyoweza kukabiliana na changamoto za foleni na misongamano katika maeneo ya kutolea huduma.

Pili jamii lazima ikubali kushiriki katika kuondoa kadhia hizo, hili linaweza kufanyika kwa kutoa maoni na ushauri wa jinsi ya kuboresha huduma kwa maana ya kuondoa foleni na misongamano kwenye maeneo wanayopatiwa huduma. Mfano mwanajamii kuja na pendekezo la kuondoa foleni za kusubiria huduma katika hospitali hasa zile kubwa kama vile hospitali za mikoa, kanda na taifa. Namna ya kuondoa foleni na misongamano mikubwa kwenye daladala na mabasi ya mwendokasi nchini. Hii itasaidia watoa huduma kupata mawazo ya wateja wao juu ya namna nzuri ya kuboresha huduma ikiwa ni pamoja na kupunguza foleni na muda wa kusubiri huduma ikiwa ni pamoja na hudma za afya, elimu, usafiri, maji na kadhalika. Suala la kutumia teknolojia nalo lina nafasi yake.

Wito wangu kwa serikali na jamii kushirikiana na kujaribu kufikiria na kuja na ufumbuzi wa namna ya kupunguza foleni na msongamano katika maeneo mbalimbali ya kutolea huduma. Mfano, hospitalini, kwenye mabasi ya daladala na mwendokasi, barabarani na visimani kwenye maji.

Mapendekezo yanapotolewa wenye kutoa huduma nao lazima wajitahidi kusikiliza na kuyafanyia kazi ushauri wanaopewa na jamii ikiwa ni pamoja na kushughulikia ili kumaliza tatizo.

## WANENAVYO MALENGA

### ILA WENGINE SI WATU

Dunia inao watu, na wengine siyo watu,
Hawa wavaa viatu, wengine bila viatu,
Huo wanasema utu, kwa mambo yasiyo utu,
Haki sawa ni kwa watu, ila wengine si watu.

Kuvaa kwao ni utu, lakini kwetu si utu,
Wasipovaa ni kutu, tusipovaa ni utu,
Hawaaminiki katu, kwa vile hawana kitu,
Haki sawa ni kwa watu, ila wengine si watu.

Malazi ni yetu watu, wanyama yao misitu,
Walakini kuna watu, hawana nyumba na vitu,
Wengine wanavyo vitu, vinaota ukurutu,
Haki sawa ni kwa watu, ila wengine si watu.

Elimu hii ya watu, ya kuerevuka watu,
Giza lisiwe ni kitu, wapate weledi watu,
Waufanye utukutu, lipendeze anga letu,
Haki sawa ni kwa watu, ila wengine si watu.

Umri kwamba ni mtu, ni kwa kushitakiwa tu,
Kwenye elimu si mtu, bali mtoto wa mtu,
Haki kwako siyo kitu, wenzako hao ni watu,
Haki sawa ni kwa watu, ila wengine si watu.

Ukitaka kopa kitu, hupewa wewe si mtu,
Wanaokopeshwa watu, mko sawa kila kitu,
Wewe bado siyo mtu, bali mtoto wa mtu,
Haki sawa ni kwa watu, ila wengine si watu.

Chagua siti kwa watu, ili nawe uwe mtu,
Vinginevyo wewe mtu, kwingineko siyo mtu,
Wakali kama kifutu, wanaojiona watu,
Haki sawa ni kwa watu, ila wengine si watu.

Ukidhani wewe ni mtu, chungulia ona watu,
Kiduku wanyoa watu, wanaonekana kwatu,
Tunduma hadi karatu, wanatamba hao watu,
Haki sawa ni kwa watu, ila wengine si watu.

Wewe jua siyo mtu, shangaa mambo ya watu,
Tafuta ndizi gurutu, za pombe si kula watu,
Ujitikise kichwa tu, ndio ulimwengu wetu,
Haki sawa ni kwa watu, ila wengine si watu.

Nakwenda fyeka msitu, nianzishe wangu utu,
Edeni ile ya watu, nikaishi roho kwatu,
Nikabaki Mungu mtu, bila kuzongwa na kitu,
Haki sawa ni kwa watu, ila wengine si watu.

Chumba changu ni msitu, sisumbuliwi na mtu,
Ni huru hakuna chatu, hivyo sitishwi na kitu,
Hata bila ya viatu, inabaki amani tu,
Haki sawa ni kwa watu, ila wengine si watu.

Mimi natamani kitu, siku sote tuwe watu,
Haki tufaidi watu, wote tulio na utu,
Huko asiweko mtu, na mwingine siyo mtu,
Haki sawa ni kwa watu, ila wengine si watu.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

# Kumekucha umeme kuchotwa kutoka angani ndani ya jua

## •Ni Marekani, Ulaya, China nyaya mahususi zaandaliwa



Vinasa mionzi ya jua vikiwekwa tayari kuvuna umeme utakaobadilisha hali ya nishati duniani . **PICHA: MTANDAO**

WAKATI Afrika na mataifa ya uchumi unaokua yakihangaika kupata umeme wa maji, makaa ya mawe na mafuta, wanasayansi wa Ulaya, China na Marekani wanafikiria kuzalisha umeme wa mionzi kutoka lilipo jua.

Magwiji wa masuala ya anga wanachunguza uwezekano wa kupatikana umeme bila kutumia waya kutoka angani na kuufikisha kwenye nyumba za wateja mamilioni duniani.

Shirika la Masuala ya Anga la Ulaya Novemba mwaka jana lilitarajiwa kuidhinisha utafiti wa miaka mitatu ili kuona kama inawezekana kuweka mitambo ya kuvuna miale ya jua kwenye anga ya juu kwa ajili ya nishati ya gharama nafuu.

Lengo lingine ni kuwa na satelaiti kubwa katika obiti, inayoweza kutoa kiwango sawa cha umeme kila moja kama kituo cha nguvu ya kuzalisha umeme huo.

Baraza la 'Environmentally Sensitive Area' ESA ndilo linalozingatia wazo hilo katika ofisi zake huko Paris Ufaransa.

Wakati mashirika kadhaa ya anga yameangalia wazo hilo, kinachojulikana kama mpango wa 'Solaris' ungekuwa wa kwanza kuweka msingi wa mpango wa kivitendo wa kuunda mfumo wa uzalishaji wa nishati mbadala unaotegemea anga ya mbali au juani.

Mpango huo ni mojawapo ya mapendekezo kadhaa yanayozingatiwa na mawaziri wa utafiti katika mkutano wa Baraza la ESA mjini Paris ambao ulitarajiwa kuamua bajeti ya awamu inayofuata ya mipango ya wakala wa anga ya juu ya uchunguzi wa ufuatiliaji wa mazingira na mawasiliano.

> "Tunahitaji kubadilika kuwa uchumi usio na hewa ukaa -kaboni na hivyo basi kubadili njia tunayozalisha nishati na hasa kupunguza mafuta katika uzalishaji wetu wa umeme," anasema

Josef Aschbacher, Mkurugenzi Mkuu wa ESA, anaiambia BBC kwamba anaamini kuwa nishati ya jua kutoka angani inaweza kuwa 'msaada mkubwa wa kushughulikia uhaba wa nishati miaka ijayo.

''Tunahitaji kubadilika kuwa uchumi usio na hewa ukaa -kaboni na hivyo basi kubadili njia tunayozalisha nishati na hasa kupunguza mafuta katika uzalishaji wetu wa umeme," anasema.

''Kama unaweza kuifanya ukiwa angani, nasema kama tunaweza, kwa sababu bado hatujafika, hii itakuwa nzuri kwa sababu ingetoa suluhisho la matatizo mengine mengi."

Nishati ya jua inaweza kukusanywa kwa ufanisi zaidi angani kwa sababu hakuna usiku wala mawingu. Wazo hilo limekuwapo kwa zaidi ya miaka 50, lakini limekuwa gumu na ghali sana kutekeleza, hadi sasa, anaongeza.

ESA inatafuta fedha kutoka kwa mataifa wanachama wake kwa ajili ya mpango wa utafiti inaouita Solaris, ili kuona kama maendeleo haya yanamaanisha kuwa sasa inawezekana kutengeneza nishati ya jua iliyotenganishwa kwa uhakika na kwa bei nafuu ili kuifanya iwe na faida kiuchumi.

Lengo kuu la mpango wa Solaris ni kubaini kama inawezekana. Kwa kweli hii haiwezi kufanywa kwa kebo ndefu sana, kwa hivyo lazima itumwe bila waya, kwa kutumia mihimili ya 'microwave.'

Timu ya Solaris tayari imeonyesha kuwa inawezekana kimsingi kusambaza umeme bila kutumia waya kwa usalama na kwa ufanisi. Wahandisi walituma kilowati mbili za nishati kwa umbali wa zaidi ya mita 30 bila waya kama sehemu ya majaribio Septemba 2022 na ikafanikiwa.

Itakuwa hatua kubwa kutuma gigawati za nguvu kutoka umbali wa zaidi ya maelfu ya maili au kilometa, lakini kwa mujibu wa Jean Dominique Coste,Meneja Mkuu wa Kitengo cha anga cha Airbus, inaweza kufikiwa lakini kupitia hatua nyingi ndogo ndogo.

Marekani, China na Japan pia zimepiga hatua katika mchakato wa kutengeneza nishati ya jua inayotegemea anga za juu na wanatarajiwa kutangaza mipango yao wenyewe hivi karibuni.

Mbali na ESA, nchini Uingereza, kampuni ya Space Solar, imeundwa, ikilenga kuonyesha nguvu inayong'aa kutoka angani ndani ya miaka sita, na kufanya hivyo kibiashara ndani ya miaka tisa.

Tathmini ya serikali ya Uingereza, isiyotegemea mpango wa ESA, ilihitimisha kuwa inawezekana kuwa na setilaiti yenye uwezo wa kuzalisha kiwango sawa cha umeme kama kituo cha uzalishaji, karibu gigawati mbili (2GW), kufikia 2040, ambayo inaambatana na makadirio ya ESA yenyewe.

Lakini, kwa mujibu wa Dk. Vijendran, ufadhili ukioongezeka na kuungwa mkono zaidi kisiasa inaweza kufanyika ndani ya muongo mmoja, sawa na tarehe ya mwisho iliyowekwa na Rais wa Marekani, John Kennedy mwaka 1961 kupeleka mwanaanga wa Marekani mwezini.

***BBC SWAHILI***

## HABARI PICHANI



Mwimbaji Mkongwe wa Nyimbo za Injili, Cosmas Chidumule, akiimba kwenye ibada ya Mwaka Mpya katika Kanisa la Free Pentecoastal jijini Tanga. **PICHA: OSCAR ASSENGA**



Mkurugenzi wa Mazubu Grand Hoteli ya Mji Mdogo wa Mirerani, wilayani Simanjiro, mkoani Manyara, Elias Kipunile, akizungumza na wakazi wa eneo hilo kuhusu kuwaruhusu watoto wao waonyeshe vipaji vyao kwa manufaa ya miaka ijayo, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**




Ofisa Tarafa ya Kwekivu, Wilaya ya Kilindi, Mkoa wa Tanga, Michael John, akikagua eneo la shamba la Shule ya Msingi Masagalu, Kata ya Masagalu wilayani humo, alipofanya ziara katika kila shule ya msingi na sekondari wilayani humo. **PICHA: DEGE MASOLI**

## CHEMSHABONGO NA -00 33 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com


Dondoo: Kulia
1. Fisi
7. mwanadamu wa kwanza
8. ugwe
9. feki
10.kiunganishi katika tungo kinachoashiria majuto
12.neno la kutilia mkazo
13.mmea mkubwa ambao hutoa mbao na kuni
15.bainika
16.chukua bila idhini ya mwenye mali 17.sifuri 18.chombo cha majini

Chini:
1. kifungo cha kufungia mkanda wa nguo
2. karo ya shule
3. mahali unapopumzika msafara
4. fuatana
5. Pesa ya China
6. Kale
11.maisha ya starehe
13.humsaidia mnyama kufukuza wadudu 14.shida



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

MKATABA
MWANGAZA
AMERIKA
AJENDA
GIDAMU
ALAMA
ALIKWA
MITAA
KAUKIA
ATIA: ADA:
MAANA, WANA
NJAA : UFA
AMI



maoni SMS: 0787 00 97 94

Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| F | A | N | A | | M | T | A | A |
| I | B | U | K | A | | A | | S |
| S | U | N | A | | A | Z | M | A |
| I | D | A | R | A | | A | | A |
| | U | | I | M | A | R | A | |
| U | | M | | I | M | A | R | A |
| K | A | T | A | N | I | | I | |
| A | L | A | M | I | N | A | | |
| M | A | W | A | K | I | L | I | |
| E | U | A | | A | | A | | |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| S | A | F | A | R | I | | M |
| O | | U | | | | | A |
| M | A | M | B | A | | | K |
| A | M | B | A | T | A | N | A |
| L | A | O | S | I | | | D |
| I | | | A | F | I | K | I |
| A | N | I | T | A | | | R |
| | N | D | A | L | A | | I |
| M | E | I | | I | | | O |





## Mahindi ya njano yafanyiwa utafiti kukabili udumavu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, imeanza kufanya utafiti wa mahindi lishe (mahindi ya njano) ili kusaidia wananchi wa mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini kukabiliana na udumavu.

Mtafiti wa mahindi katika kituo hicho, Leonald Sabula aliyasema hayo jana alipozungumza na Nipashe kuhusu shughuli mbalimbali zinazofanywa na taasisi hiyo hasa utafiti wa mbegu za mazao.

Alisema walianza kufanya utafiti huo mwaka juzi na wanatarajia kutoa matokeo ya awali mwaka huu hasa katika kipindi cha maonyesho ya wakulima (Nanenane).

Alisema wanakusudia kukamilisha utafiti huo mwakani na kuanza kusambaza mbegu hizo kwa wakulima ili zianze kulimwa kwenye maeneo ambayo watabaini kuwa yanafaa kuzalishwa.

"Kwa sasa tunapambana zaidi na tatizo la udumavu hasa kwa watoto, haya mahindi yamebainika kuwa yana virutubisho vingi ambavyo vinafaa kwa watoto kwenye mikoa yetu hii," alisema Sabula.

Sabula alisema mikoa ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini inazalisha chakula kwa wingi lakini ndiyo inayokabiliwa na udumavu kwa kiwango kikubwa.

Alisema mbali na mahindi hayo, pia kituo hicho kinazalisha mazao mengine yenye virutubishi muhimu kwa watoto ikiwamo viazi lishe na maharage.

Alisema mazao hayo yanatakiwa kuliwa na watu wote bila kujali umri, huku akisisitiza kuwa ni muhimu zaidi kwa watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano.

Hata hivyo Sabula alisema mahindi hayo yana soko kubwa duniani ambalo Watanzania wanatakiwa kuchangamkia kuzalisha hasa katika nchi ya Misri.

# Dk. Tulia aongoza mamia kufanya usafi Soko la Soweto

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MBUNGE wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson, amewaongoza wananchi wa Kata ya Ruanda mkoani hapo kufanya usafi katika Soko la Soweto ambalo lilikuwa limekithiri uchafu.

Dk. Tulia alishiriki kufanya usafi huo jana, kushuhudia mrundikano wa taka zilizotelekezwa na wafanyabiashara wa soko hilo na baadhi kuanza kutoa harufu hali ambayo inahatarisha afya za wananchi wa eneo hilo.

Akiwa eneo hilo, Dk. Tulia aliwataka wananchi wa kata hiyo kuzingatia usafi katika maeneo yao ili kuepuka magonjwa ya mlipuko ikiwamo kipindupindu ambacho husababishwa na uchafu.

Vilevile alisema kitendo cha wananchi kutofanya usafi kwenye maeneo yao kinasababisha kuwa chafu na kuondoa hadhi ya Jiji hilo ambalo kwa miaka ya karibuni lilikuwa miongoni mwa majiji safi.

"Naomba sana wananchi mjitahidi kufanya usafi kwenye maeneo yenu, sasa hivi halmashauri imeanzisha utaratibu mpya wa kufanya usafi kwa kuyaondoa maghuba ili usafi usimamiwe moja kwa moja na na viongozi wa kata," alisema Dk. Tulia.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Benki, Anna Ndimbwa, alisema amekuwa akifuatilia uzoaji wa taka zinazorundikwa na wananchi wa eneo hilo bila mafanikio.

Alisema baada ya kukuta hali inazidi kuwa ngumu aliamua kupeleka taarifa kwa Diwani wa Kata ya Ruanda lakini bado hali haijawa vizuri na sababu ya kuondoa maghuba bado wananchi hawajapewa elimu ya kutosha.

Diwani wa Kata ya Ruanda, Reuben Kipalule, amekiri mzabuni kushindwa kuzoa taka kwa wakati kutokana na mzabuni anayezoa taka hizo kutokuwa na uwezo wa kumudu kazi.

Aliahidi kutafuta mzabuni mwingine ili wagawane maeneo na kuzoa taka hizo kwa wakati tofauti na sasa ili kuwaepusha wananchi na tatizo linaloweza kutokea la magonjwa ya mlipuko.

Naye Naibu Meya wa Jiji la Mbeya, Kefasi Mwasote, alisema maeneo mengi ya Jiji hilo yanakabiliwa na tatizo la kukithiri kwa uchafu na akaahidi ofisi yake kusimamia kwa karibu ili usafi uwe unafanyika mara kwa mara.

Alisema kwenye vikao vya Baraza la Madiwani waliazimia usafi usimamiwe na wazabuni kupitia vikundi mbalimbali na kuyaondosha maghuba katika maeneo yote ili taka zizolewe kwa muda maalumu kulingana na makubaliano ya viongozi wa Kata.

Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Triphonia Kisiga, alisema watashirikiana na madiwani kila kata ili kuhakikisha Jiji linakuwa na mazingira safi.

Hata hivyo alisema utaratibu mpya umepunguza gharama za uendeshaji kutokana na shughuli zote za makusanyo hufanyika katika kila kata ambako ndiko taka zinazalishwa.

Hivi karibu Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, aliagiza halmashauri zote za mkoa huo kufanya usafi wa mazingira ili kuepuka magonjwa ya mlipuko kikiwamo kipindupindu.




Spika wa Bunge ambaye ni Mbunge wa Mbeya Mjini, Dk. Tulia Ackson (kushoto), akipakia taka kwenye gari baada ya kufanya usafi jana katika soko la Soweto jijini hapo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Ma-DC wapewa siku 20 kufanya tathmini ya mifugo

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imetoa siku 20 kwa wakuu wa wilaya zote za mkoa huo kufanya tathmini ya mifugo iliyoko katika maeneo yao na uwezo wa maeneo ya malisho yaliyotengwa ili kukabiliana na tatizo la uharibifu wa mazingira.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera alitoa agizo hilo jana alipozungumza na waandishi wa habari ambapo aliwataka kuwasilisha taarifa ya tathmini hiyo Januari 20, mwaka huu.

Homera alisema tathmini hiyo ni utekelezaji wa maagizo yaliyotolewa hivi karibuni na Rais Samia Suluhu Hassan alipokuwa anazindua ujazaji wa maji kwenye Bwawa la Kuzalisha Umeme la Mwalimu Nyerere.

Alisema mbali na maagizo hayo, pia yapo maagizo yaliyotolewa na Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa kwa wakuu wa mikoa.

Alisema endapo idadi ya mifugo iliyopo kwenye wilaya itakuwa haiendani na maeneo yaliyotengwa viongozi wa maeneo hayo watatakiwa kutafuta namna ya kukabiliana na tatizo hilo.

"Tunatakiwa kulinda mazingira yetu ikiwamo vyanzo vya maji, mkoa wetu ni muhimu sana kwenye kulinda vyanzo vya umeme ikiwamo Bwawa la Mtera, Kidatu na Bwawa la Nyerere," alisema Homera.

Alisema baada ya viongozi hao kuwasilisha taarifa ya tathmini yao, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa itaangalia namna ya kushirikiana nao kukabiliana na tatizo la mifugo.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon Mayeka, wiki iliyopita alipiga marufuku wafugaji kutoka katika maeneo mbalimbali kuingiza mifugo wilayani humo kwa maelezo kuwa mifugo iliyoko ndani ya wilaya hiyo inatosheleza maeneo yaliyotengwa.

Alisema ongezeko la mifugo kwenye wilaya hiyo linaweza likasababisha migogoro ya wakulima na wafugaji kama ambavyo imekuwa ikitokea kwenye maeneo mengine nchini.

Alisema baadhi ya wafugaji wamekuwa wakiingiza mifugo kinyemela kutoka katika Wilaya ya Mbarali na Wilaya ya Songwe na hivyo kusababisha matatizo mbalimbali kwenye maeneo wanayokwenda kuchungia.

Alisema mbali na uingizaji huo wa mifugo kusababisha migogoro kati ya wakulima na wafugaji, pia imekuwa ikisababisha migogoro kati ya wafugaji na hifadhi za taifa.



# Askofu ashauri kutengwa siku 3 kuliombea taifa

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Karmeli Assemblies of God, Dk. Evance Chande, ameiomba serikali kutenga siku tatu maalumu kila mwaka kwa ajili ya maombi ya kuliombea taifa na viongozi wake.

Aliutoa ushauri huo juzi wakati wa ibada ya mkesha wa mwaka mpya na maombi maalum kwa ajili ya kuliombea taifa.

Dk. Chande akihubiri kwenye kanisa hilo lililoko Ipagala jijini Dodoma aliiomba serikali kutenga siku hizo kuwa maalumu kwa Watanzania kuomba kwa Mungu kwa ajili ya maombezi mbalimbali yatakayofanyika nchi nzima.

"Ikipendeza serikali yetu sikivu kuangalia hilo, itenge siku yake ambayo itakayokuwa maalumu kwa Watanzania wote kufanya ibada ya maombi ambayo yatakayokuwa kwa ajili ya kumwombea Rais, wasaidizi wake, uchumi wetu, rasilimali zetu, kilimo pamoja na ibada zetu zinazofanyika," alisema.

Aidha, alisema kama ilivyokuwa kwa kipindi ambacho nchi mbalimbali ikiwamo Tanzania ilivyokumbwa na ugonjwa wa UVIKO-19, Rais aliyekuwapo madarakani alitoa siku tatu kwa ajili ya kumuomba Mungu ni wakati sasa serikali kuliangali hilo.

"Ni imani yangu serikali kwa kushirikiana na madhehebu ya dini ikifanya hivyo nchi itafanikiwa katika kutatua matatizo mbalimbali yanayoigusa serikali na wananchi na hatimaye Mungu atafanikisha maendeleo zaidi na kutuponya na magonjwa,"alisema.

Askofu huyo aliwaomba Watanzania katika mwaka 2023 uwe wa kufanya kazi kwa bidii kwa ajili ya kujiimarisha kiuchumi huku wakiungana kwa pamoja kuwaombea viongozi, taifa na watu wake.

"Watanzania kwa mwaka huu wa 2023 uwe wa kujituma zaidi kwenye kufanya kazi katika sekta mbalimbali zikiwamo za kilimo na ufugaji na zinginezo kwa ajili ya kuliletea taifa maendeleo ambayo yatakayoinua uchumi wetu, "alisema.



Baadhi ya wachuuzi wa samaki wakisubiri wateja nje ya soko kuu la Majengo jijini Dodoma jana. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

## Vijana 530 wajengewa uwezo ushiriki maamuzi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

TAASISI ya Vijana Mkoa wa Dodoma (DOYODO) imefanikiwa kuwajengea uwezo vijana zaidi ya 530 kuhusu umuhimu wa ushiriki na ushirikishwaji katika ngazi za maamuzi.

Mkurungenzi wa DOYODO, Rajabu Nhunga, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake kuhusu mafanikio ya taasisi hiyo kwa mwaka jana 2022.

Alisema idadi hiyo ya vijana imejengewa uwezo kuhusu umuhimu wa ushiriki na ushirikishwaji katika ngazi za maamuzi kupitia kutoa elimu juu ya umuhimu wa Baraza la Vijana la Taifa.

Kadhalika alisema sababu ya kuwajengea uwezo vijana hao ni kusaidia kuwa sehemu ya kutunga sera katika kufanya maamuzi kwenye mabaraza wanayowakilisha wenzao.

Nhunga, alisema vijana hao waliojengewa uwezo wanatoka kwenye halmashauri saba za Mkoa wa Dodoma ambazo ni Bahi, Kondoa, Dodoma Jiji, Mpwapwa, Kongwa, Chamwino na chemba.

Pia alisema taasisi imefanikiwa kuzijengea uwezo taasisi 15 za vijana kutambua umuhimu wa uanzishwaji wa Baraza la Vijana Taifa kwenye halmashauri hizo.

Alisema DOYODO pia imekuwa ikiwajengea uwezo wanafunzi kwa kuwapa elimu ya kujikinga na mimba za utotoni na kuwajengea uwezo kuhusu elimu ya ujasiriamali watakapomaliza masomo yao.

Aidha, alisema taasisi hiyo imeendelea kuendesha mradi wa ujasiriamali wa kufyatua matofali ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha ushiriki wa vijana katika kujenga uchumi na kujiajiri.

Alisema DOYODO, inaendelea kuboresha ushirikiano na wadau mbalimbali husnsani Shirika la DSW Tanzania ambalo limekuwa likiwezesha katika utekelezaji wa miradi ya afya ya uzazi kwa vijana ili kupunguza matatizo ya mimba za utotoni mkoani Dodoma.

Aliwataja wadau wengine kuwa ni Pact Tanzania na Segal Family Foundation ambao wamekuwa wakisaidia katika maeneo mbalimbali ya utekelezaji wa shughuli zao.

Alisem: "Wadau wengine tunaoshirikiana nao ni pamoja na Shirika la UNFPA Tanzania, EANNASO".

# Kaya 156,586 kuondolewa mfuko TASAF

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) umesema unatarajia kuziondoa kaya 156,586 ambazo zimeimarika kiuchumi, kwamba zitaanza kujitegemea.

Hayo yalibainishwa na Mkurugenzi Mkuu wa TASAF, Ladislaus Mwamanga, wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma kuhusu kuhitimu kwa walengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini nchini.

Alisema mfuko huo umeendelea kutoa elimu ya kujitambua pamoja na kuwekeza fedha katika vikundi vya akiba.

Mwamanga, alisema dhana ya elimu kwa walengwa juu ya uhitimu inahitajika kwa kiasi kikubwa ili muda unapofika wasishangae kuondolewa na kuingia wengine wenye uhitaji.

Kutokana na hilo alisema wamekuwa wakitoa elimu ya namna ya kutunza fedha ikiwamo kujiunga na vikundi mbalimbali vya maendeleo ili kuanzisha miradi.

"Elimu hii imesaidia sana kuna baadhi ya walengwa hadi sasa wanajitegemea na wanasubiri kuondolewa katika mpango huo mwaka huu," alisema Mwamanga.

Hata hivyo aliishukuru serikali kutokana na kutoa fedha kwa ajili ya walengwa hao, huku akiahidi TASAF itaendelea kuwapatia misaada walengwa katika kaya ambazo zinastahili kupewa.

Akizungumzia mafanikio ya mwaka uliopita alisema wanatarajia kuziondoa kaya 156,586 ambazo zimeimarika kiuchumi na zinakwenda kujitegema zenyewe.

Alisema hayo ni mafanikio makubwa kwa sababu kaya hizo zilikuwa na hali duni lakini hivi sasa wameimarika kiuchumi ikiwamo kuendesha miradi mbalimbali ya kujipatia kipato cha kila siku.

Alisema kaya 16,490 zimepokea ruzuku ya uzalishaji ambapo kaya hizo zinatoka katika Halmashauri ya Bagamoyo, Lindi, Kibaha, Chalinze na katika Manispaa ya Mtwara, Lindi na Unguja.

Pia alifafanua kuwa utaratibu wa kuziondoa kaya zilizoimarika kiuchumi utakuwa endelevu, hivyo walengwa wanapaswa kuzingatia elimu wanayopewa.

Alisema kaya hizo zitaondolewa kwa awamu lakini kwa utaratibu ambao utatumika kuwatambua walioimarika kiuchumi ili waweze kuapisha wengine.

Alisema pia uhakiki wa walengwa kutathmini hali zao ulifanyika katika mamlaka zote 186 za utekelezaji wa mpango huo na kubaini baadhi ya kaya zimeimarika kiuchumi.



## Wananchi wakumbushwa kutunza mazingira muda wote

**Na Mwandishi Wetu**

KATIBU Mkuu Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Dk. Mngereza Mzee Miraji, amesema ili mji uwe katika haiba nzuri jamii inapaswa kutunza mazingira.

Alitoa ushauri huo baada ya kukamilika kwa kazi ya kusafisha eneo la Sebleni Nyumba za Wazee ikiwa ni sehemu za shamra shamra za kuelekea miaka 59 ya Mapinduzi Zanzibar.

Alisema moja kati ya majukumu ya taasisi yake ambayo inasimamia makazi ni kuhakikisha mazingira ya maeneo ya makazi yanakuwa safi na yenye mwonekano wenye kuvutia.

Alisema kufanya usafi katika eneo ambalo wanakaa wazee ni kuwathamini wazee na kuyaenzi maeneo wanayoishi na wao ni hazina muhimu, hivyo ni lazima kuhakikisha mazingira wanayoishi ni safi na salama.

"Wizara ya Ardhi tunapasawa kuhakikisha tunasimamia makazi bora pamoja na usafi wa mazingira yote yaliyoizunguka jamii," alisema Dk. Mngereza.

Aidha, alizitaka taasisi nyingine kujenga utamaduni wa kushiriki katika shughuli za usafi katika maeneo mbalimbali ya Mji wa Zanzibar.

Naibu Katibu Mkuu Wizara hiyo, Mzee Ali Haji, alimpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi namna anavyokwenda sambamba na kasi ya kuleta maendeleo.

Mkurugenzi Mkuu Shirika la Nyumba Zanzibar, Mwanaisha Ali Saidi, alisema kuwa moja ya jukumu la wizara hiyo katika taasisi yake ya Shirika la Nyumba ni kutoa huduma bora zenye kuzingatia mazingira ya usafi, hivyo siku hiyo imekwenda sambamba na dhana nzima ya utekelezaji wa majukumu kwa shirika hilo.

# Kicheko wavuvi wakipewa kifaa cha kutafuta samaki

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAVUVI wanaopatiwa mafunzo ya mbinu za kisasa za kutafuta samaki kwa kutumia kifaa cha kutafutia samaki (Fish Finder), wamesema njia hiyo itawarahisishia kazi pamoja na kuondokana na uvuvi wa kutumia zana za kizamani.

Waliyasema hayo jana kwenye mafunzo maalum kwa wavuvi juu ya utumiaji wa vifaa vya kuongozea vyombo vya baharini na kutafuta samaki.

Miongoni mwa wavuvi hao ni Issa Salum Mussa ambaye alisema njia za sasa za kutumia kutafuta samaki ni rahisi na zitarahisisha upatikanaji wa samaki kwa haraka ukilinganisha na njia zilizokuwa zikitumika hapo awali.

Alisema njia ya kutumia kutafuta samaki (Fish Finder), zitawasaidia kupata samaki kwa wingi na kwa uhakika jambo ambalo litainua kipato chao kwa haraka kulinganisha na njia za kianalogi ambazo zilikuwa zinatumia muda mwingi kutafuta samaki baharini.

Mvuvi Kheria Ramadhani Juma alisema, walilazimika kutumia muda mwingi kuwa baharini jambo ambalo lilikuwa likiwafanya wawe mbali na familia hivyo, anaamini uwapo wa vifaa hivyo vipya hali itabadilika.

"Tulikuwa tunahamia kwenye dago siku 15 hadi 20 kutafuta samaki na wakati mwingine tulikuwa tunakosa samaki na kurudi nyumbani mikono mitupu," alisema.

Hata hivyo aliitaka wizara kuongeza mafunzo kwa wavuvi wingine ambao hawajapatiwa mafunzo ili kufikisha elimu ya utumiaji vifaa vya kisasa kwa wavuvi wote Unguja na Pemba.

Naye Mratibu kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Shabaan Hassan Ramadhan, alisema lengo la kutoa mafunzo kwa wavuvi ni kuwasaidia kutumia vifaa vya kisasa na kuondokana na uvuvi wa kimazoea ambao hauna tija kubwa kwa wavuvi.

Alisema mafunzo wanayopewa wavuvi juu ya namna bora ya kutumia vifaa vya kuongozea na kutafuta samaki ni mwendelezo wa mafunzo kutoka Wizara ya Uchumi wa Buluu kwa wavuvi.

Alisema mafunzo hayo yanakwenda sambamba na ugawaji wa boti na mashine zake kwa wavuvi hao ili kufanya kazi zao za uvuvi.



Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, akisalimiana na Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Utalii Zanzibar, Hafsa Mbamba, wakati wa uzinduzi wa hoteli ya kitalii yenye hadhi ya nyota tano Toa Hoteli iliyoko Uroa Pongwe Mkoa wa Kusini Unguja. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Elimu kujikinga na ebola, surua bado inahitajika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKUU wa Wilaya ya Magharibi 'A', Suzan Peter Kunambi, amesema elimu kuhusu maradhi ya ebola na surua, inahitajika kwa kila mtu ili jamii kujikinga na maradhi hayo.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mafunzo kwa wafanyakazi wa ofisi hiyo kuhusu maradhi hayo, yaliyoandaliwa na Ofisi ya Mkuu na Wilaya hiyo kwa lengo la kuwapa elimu na jinsi ya kujikinga na maradhi hayo.

Alisema mafunzo kwa watumishi hao yatasaidia kuongeza uelewa na kuwa mabalozi wazuri katika kuelimisha jamii kwa vile ofisi za wilaya zinahudumia wananchi mbalimbali.


Alisema kuwa ni vyema kwa sasa kila mmoja kufahamu madhara yanayotokana na mlipuko wa maradhi hayo kwa kusikiliza wataalamu wa afya pamoja na kuishi kwa tahadhari na endapo mtu atabaini dalili zinazotajwa afike kituo cha afya mapema kwa ajili ya matibabu.

"Jamii tunatakiwa tubadilike tusikilize ushauri kutoka kwa wataalamu wa afya nini tufanye pindi inapotokea maradhi ya milipuko," alisema Kunambi.

Alisema mafunzo ya kuwajengea uwezo wafanyakazi katika majukumu yao yatawasaidia kuongeza ubunifu na bidii ya uwajibikaji, hivyo mafunzo hayo yatawaongoza katika kuzifuata kanuni na sheria za utumishi wa umma.

Akitoa mafunzo hayo Mratibu wa Huduma za Afya kutoka Wilaya ya Magharibi 'A' (DHMT), Rajab Khamis Rajab, alisema wameona kuna umuhimu wa kutolewa elimu ya maradhi ya ebola na surua kwa watumishi wa umma kwa kujitambua na kuwaelimisha jamii haswa kwa wale watakaofika kufuata huduma katika taasisi za kiserikali.

Wafanyakazi walioshiriki mafunzo hayo waliupongeza uongozi wa wilaya hiyo kwa kuwapatia mafunzo yanayohusu maradhi hayo.





# Waogopa kufichua vitendo ukatili wakihofia familia kusambaratika

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BAADHI ya wanawake wa Kata ya Muhongolo, Halmashauri ya Manispaa ya Kahama mkoani Shinyanga, wamesema wanashindwa kutoa taarifa za vitendo vya ukatili wanavyofanyiwa na waume zao wakihofia kunyimwa mahitaji na familia kusambaratika.

Waliyabainisha hayo hivi karibuni wakati wa kampeni ya mtaa kwa mtaa ya kutoa elimu ya kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto, iliyoandaliwa na ofisi ya Ustawi wa Jamii katika Manispaa ya Kahama.

Walisema vitendo hivyo vimekithiri lakini hawawezi kutoa taarifa yoyote kwenye vyombo vya sheria kwa kuhofia kunyimwa hela za matumizi na wanaume wao.

Wakizungumza na Nipashe mmoja wa wakazi hao, Naomi Kusekwa alisema familia nyingi wanaume wanawabaka wajukuu zao kwa tamaa za kimwili, lakini wanashindwa kutoa taarifa kutokana na kuhofia kukosa mahitaji muhimu.

Alisema familia nyingi zikikutana na mikasa hiyo zinabaki kimya na kulazimika kuwatibu watoto waliofanyiwa vitendo hivyo.

Naomi alisema ili kuondoa hali hiyo ni vyema mashirika yanayotoa elimu ya ukatili wa kijinsia kwa kushirikiana na serikali kuwaelimisha wanaume.

Aliongeza kuwa kupitia elimu hiyo watawauliza wanaume kwa nini wanafanya vitendo hivyo na kuvitafutia ufumbuzi wa haraka, lengo likiwa ni kuwanusuru watoto wa kike.

Mkazi mwingine Prisca Mabula alisema sababu za wanaume kubaka watoto na wajukuu zao zinasababishwa na watoto wenyewe kuvaa nguo fupi ambazo hazisitiri miili yao. Mwenyekiti wa Mtaa wa Muhongolo, Emmanuel Charles, alisema hivi karibuni kuna binti alibakwa katika mazingira ya kutatanisha na wahusika waliwakamata kwa kushirikiana na wananchi na kuwafikisha katika vyombo vya sheria na kesi hiyo inaendelea mahakamani katika Mahakama ya Wilaya.

Alisema kampeni ya mtaa kwa mtaa itasaidia kuongeza uelewa kwa wananchi na kufahamu madhara ya ukatili wa kijinsia.

Hivyo aliwataka wananchi kujenga desturi ya kutoa elimu pale matukio ya namna hiyo yanapotokea kwenye jamii.

Ofisa Ustawi wa Jamii Manispaa ya Kahama, Swaiba Chemchemu, aliwasihi wananchi wanapotoa taarifa ya vitendo hivyo wawe tayari kutoa ushirikiano kwa kutoa ushahidi mahakamani.

Alisema kwa kipindi cha Januari hadi Septemba mwaka jana watoto 881 walibainika, kufanyiwa vitendo mbalimbali vya ukatili ikiwamo kubakwa, kulawitiwa na kuozeshwa na kusababisha baadhi yao kukatisha masomo.

Alisema kati ya watoto hao, 70 mashauri yao yameshafanyiwa kazi na wahusika wameshachukuliwa hatua za kisheria.

Swaiba alisema kati ya idadi hiyo watoto tisa walikuwa wa kiume na 61 wa kike na bado wanaendelea kushughulikia yaliyobaki ili kuhakikisha kila mtoto anapata haki yake.



Wakazi wa Mji wa Muheza, mkoani Tanga wakinunua bidhaa mbalimbali za vyakula katika soko la mboga Mtaa wa Msikiti Mkuu jana. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

## Waitupia lawama TANESCO kuchelewa kuwapa umeme

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI Kata ya Ndala Manispaa ya Shinyanga wamelalamikia kuchelewa kuunganishiwa huduma ya umeme na kusema inakwamisha shughuli zao za maendeleo.

Walibainisha hayo juzi kwenye mkutano wa hadhara uliоitishwa na Diwani wa Kata ya Ndala Manispaa ya Shinyanga, Zamda Shabani, ambao ulifanyika katika Mtaa wa Mlepa.

Mmoja wa wananchi hao, Claud Joseph alisema hawaridhishwi na huduma ambazo zinatolewa na Shirika la Umeme Nchini (TANESCO) mkoani Shinyanga.

Alisema wananchi walioomba kuunganishiwa na huduma ya umeme wanakaa muda mrefu bila kupata huduma hiyo.

"Haturidhishwi na huduma ambazo zinatolewa na TANESCO, kasi yao ni ndogo sana kuunganishia wananchi umeme," alisema Joseph.

Akitoa ufafanuzi wa malalamiko hayo, Kaimu Meneja wa TANESCO mkoani Shinyanga, Kulwa Mangara, aliahidi kuyashughulikia pamoja na kuongeza kasi ya kuunganisha umeme.

Alisema moja ya sababu ya wananchi kusubiri muda mrefu kuunganishiwa nishati hiyo ni kutokana na kuwa na wateja wengi wanaohitaji.

Diwani wa kata hiyo, akizungumza kwenye mkutano huo, aliisisitiza TANESCO kuongeza kasi ya kuunganishia umeme kwa wananchi ili kuchochea shughuli za maendeleo kwenye maeneo yao.

Pia aliwataka wananchi kushirikiana na serikali katika kuchangia shughuli za maendeleo ikiwamo uanzishaji wa maboma ya shule na zahanati.

# Serikali yashauriwa kujenga soko kubwa, kituo cha mabasi

**Na Lilian Lugakingira,** BUKOBA

BAADHI ya wakazi wa Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera wameishauri serikali kutafuta eneo jipya kwa ajili ya ujenzi wa soko kubwa na la kisasa na kukamilisha ujenzi wa kituo kikuu cha mabasi, ambacho ujenzi wake umeanza katika eneo la Kyakailabwa.

Wakizungumza na Nipashe wakazi hao walisema kujengwa kwa soko na kituo hicho cha mabasi kutafungua fursa za kiuchumi kwa mkoa huo, ambao unatajwa kuwa miongoni mwa mikoa ya mwisho kwa umaskini.

Mmoja wa wakazi hao, Abubakary Ramadhan ambaye ni mfanyabiashara katika Soko Kuu la Bukoba alisema kuwa wanakubaliana na jitihada zinazofanywa na serikali katika kuhakikisha pato la mkoa linapanda. Alisema endapo kutajengwa soko kubwa na kituo bora cha mabasi kutachangia uchumi mkoani humo.

"Soko letu hili tunalolitumia hivi sasa ni finyu, nashauri lipatikane eneo lingine kwa sababu wafanyabiashara tumekuwa wengi, kipindi kile tunaingia humu tulikuwa 600, lakini kwa sasa tupo kama 2,000," alisema Ramadhan.

Mfanyabiashara mwingine, Anold Mwombeki ambaye ni mkazi wa manispaa hiyo alisema pamoja na ujenzi wa soko la kisasa bado serikali inapaswa kukamilisha mradi wa kituo kikuu cha mabasi ili kuwaepusha na adha ambazo huwakumba wasafiri na watu wanaofanya shughuli zao katika kituo cha sasa kutokana na uchakavu.

Alisema: "Bado kituo chetu hiki kinachotegemewa na wenyeji na wageni wanaokuja Kagera ni tatizo hususani wakati wa mvua zikinyesha panajaa matope, nitafurahi sana endapo kitajegwa kituo kipya maana itakuwa moja ya fursa na kivutio kwa wawekezaji wanaotamani kuja kuwekeza katika mkoa wetu," alisema Mwombeki.

Akizungumza na waandishi wa habari Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Albert Chalamila, alisema mwaka 2023 kuna fursa nyingi za kiuchumi ambazo zitafunguka na kuwataka wawekezaji kujitokeza kuwekeza katika sekta mbalimbali ikiwamo za kilimo, viwanda na ufugaji. "Fursa mojawapo ni mradi mkubwa ambao una zaidi ya Sh. bilioni 50 kwa ajili ya kujenga kituo kipya cha mabasi na cha malori, masoko, barabara na kutengeneza taa, utakaogharamiwa na serikali kupitia Benki ya Dunia (WB) na fedha hizo Mungu akipenda haitazidi Machi tutazipokea," alisema Chalamila.

Maombi ya wakazi hao yamekuja siku chache baada ya Chalamila kutaka wananchi kutoa maoni yao ili kuona kama ujenzi wa kituo hicho katika eneo hilo uendelee au litafutwe eneo lingine.

# Rais da Silva aahidi kuijenga upya Brazil

**BRASILIA, Brazil**

RAIS wa Brazil, Luiz Inacio Lula da Silva, ameahidi kuijenga na kuliunganisha upya taifa hilo ambalo lilikumbwa na mgawanyiko mkubwa wa kisiasa wakati wa utawala wa kiongozi wa zamani Jair Bolsonaro.

Da Silva alitoa ahadi hiyo jana baada ya kuapishwa kuiongoza Brazil kwa mara nyingine, ikielezwa kuwa kiapo hicho kilishuhudiwa na maelfu ya watu wa taifa, na kwamba mtangulizi wake Bolsonaro alisusia kushiriki hafla hiyo, kinyume na tamaduni za nchi hiyo, zinazomtaka kiongozi mpya hukabidhiwa joho la njano na kijani na mtangulizi wake.

Pia kiongozi huyo aliahidi kupigania watu wa mapato ya chini, kupigana na ubaguzi na ukataji miti kwenye msitu wa Amazon, jambo linalotajwa kukithiri wakati wa utawala wa Bolsonaro.

Aidha, aliwaomba raia wa Brazil ambao hawakumuunga mkono kwa kumpigia kura, kuungana naye katika ujenzi wa taifa akisema raia wa Brazil ni kitu kimoja.

Hata hivyo, Rais Da Silva, aliwahi kuongoza taifa hilo mwaka 2003 hadi 2010, kabla ya kukabiliwa na kesi ya ufisadi iliyomlazimu kukaa jela kwa miaka mitano.

***RFI***



Rais mpya wa Brazil, Luiz Inacio Lula da Silva, akila kiapo cha kuongoza nchi hiyo. **PICHA: RFI**

# EU yapongeza mafanikio ya Croatia

**EU**

MKUU wa Umoja wa Ulaya (EU) amepongeza hatua kubwa ya mafanikio iliyopigwa na Croatia, taifa changa la umoja huo ambalo lilijiunga na ukanda wa sarafu ya Euro na eneo la Schengen.

Inaelezwa kuwa siku ya mwaka mpya, Croatia ilianza kutumia sarafu ya euro na kuwa mwanachama wa 27 wa eneo kubwa ulimwenguni la kusafiri bila pasipoti la Schengen.

Rais wa Halmashauri Kuu ya Ulaya, Ursula von der Leyen, alikutana na viongozi wa Croatia na Slovenia katika kivuko cha mpaka cha Bregana baina ya nchi hizo mbili za Balkan, ambacho kiliwekwa wazi katika dakika za mwanzo za mwaka huu wakati eneo la usafiri huria la Schengen likipanuliwa na kujumuisha Croatia.

Von der Leyen, alisema ilikuwa siku ya kuandikwa kwenye vitabu vya kumbukumbu.

"Kizazi kijacho cha Wacroatia kitakulia katika eneo la Schengen. Watu wataweza kusafiri kwa uhuru, biashara haitaathiriwa na ukaguzi. Usafiri usio na vizuizi utaleta matokeo yanayoonekana kwa watu wanaoishi mpakani, wanaofanya kazi katika pande mbili za mpaka au kuwa na familia katika pande zote za mpaka. Jamii zitaungana pamoja tena," alisema von der Leyen.

Inabainishwa kuwa Croatia pia iliiweka pembeni sarafu yake ya kitaifa, na kuwa mwanachama wa 20 wa sarafu ya euro inayotumiwa na watu milioni 347 barani Ulaya.

Wataalamu wanasema kuanza kutumia sarafu ya euro kutasaidia kuulinda uchumi wa Croatia katika wakati ambao mfumuko wa bei unaongezeka duniani kote baada ya uvamizi wa Urusi nchini Ukraine kusababisha kupanda kwa bei za chakula na mafuta.

Hata hivyo, inaelezwa kuwa baadhi ya Wacroatia wanahofia kuhamia kwenye sarafu ya euro kutasababisha kuongezeka kwa gharama ya maisha kwa sababu wafanyabiashara wataongeza wakati wanapobadilisha sarafu.

Maofisa wanatetea uamuzi wa kujiunga na kanda ya euro na Schengen, wakisema kwa kufanya hivyo, Croatia imekamilisha ushirikiano wake kamili na EU.

Wataalamu wanasema matumizi ya euro yatapunguza masharti ya kukopa wakati huu mgumu wa kiuchumi.

Tangu Urusi ilipoivamia Ukraine Februari 2022, maofisa wa EU wamesisitiza kuwa kuimarisha ushirikiano wa jumuiya hiyo na mataifa ya magharibi mwa Balkan ni muhimu zaidi kuliko wakati mwingine wowote katika kudumisha usalama wa Ulaya.

Croatia ambayo ina jumla ya watu milioni 3.9 ilijiunga na EU mwaka 2013. ***DW***

# Wakatoliki waanza kutoa heshima za mwisho

**VATICAN**

WAUMINI wa Kanisa Katoliki wameanza kutoa heshima zao za mwisho mjini Vatican kwa papa mstaafu Benedict XVI, ambaye mwili wake utawekwa katika Kanisa la Mtakatifu Petro kwa siku tatu kabla ya mazishi yake.

Kwa mujibu wa DW, waumini hao walianza kutoa heshima za mwisho jana Mjini Vatican, kwa kiongozi huyo wa kidini mwenye asili ya Ujerumani, ambaye alifariki dunia wiki iliyopita.

Inaelezwa kuwa kiongozi huyo aliliongoza kanisa hilo kwa miaka minane kabla ya kuwa papa wa kwanza katika karne sita kujiuzulu mwaka wa 2013.

Mrithi wake Papa Francis ataongoza mazishi Alhamisi katika uwanja wa Mtume Petro, kabla ya mwili wake kuzikwa katika makaburi yaliyoko chini ya kanisa kuu la Mtume Petro.

Uongozi wa kanisa katoliki mjini Vatican ulitoa jana picha za maiti ya Benedict XVI, akiwa amevalishwa mavazi mekundu ya maombolezo ya upapa na akiwa na kilemba chenye ncha za dhahabu kichwani.

**DW**

# Mashambulizi mapya yashuhudiwa Ukraine

**KYIV, Ukraine**

SHAMBULIZI jipya la kutokea angani liliulenga mji mkuu wa Ukraine, Kyiv jana, baada ya siku kuu ya Mwaka Mpya kukumbwa na mfululizo wa mashambulizi ya Russia yaliyowaua watu wanne katika mji huo mkuu.

Kwa mujibu wa DW, Kyiv na miji mingine Jumamosi ilishambuliwa kwa makombora na ndege zisizoruka na rubani na kuwaua watu watatu na kwamba shambulizi jipya lilitokea jana na kumuua mtu mmoja katika eneo la Zaporizhzhia.

Ilielezwa kuwa uongozi wa kijeshi mjini Kyiv uliwaamuru wakazi kukimbilia katika mahandaki ya kujikinga na mabomu.

Mshauri wa Rais wa Ukraine, Mykhailo Podolyak, alisema mashambulizi ya siku kuu ya Mwaka Mpya yaliyalenga maeneo yenye shughuli nyingi ya miji mikubwa.

**DW**

# HABARI PICHA



Mke wa Rais wa Zanzibar, Mariam Mwinyi, akisalimiana na viongozi alipowasili katika ukumbi wa Umoja ni Nguvu mkoani Pemba jana kwa ajili ya kugawa vifaa vya uvuvi kwa vikundi vya wakulima wa mwani katika shamra shamra za maadhimisho ya Miaka 59 ya Mapinduzi Zanzibar.



Mke wa Rais wa Zanzibar, Mariam Mwinyi (wa pili kushoto), akimkabidhi mashine ya kusagia mwani Katibu wa Kikundi cha Umoja ni Nguvu cha Kikuu, Lailat Mussa Othman (katikati), Mkoa wa Kusini Pemba.



Mama Mariam Mwinyi akimkabidhi fimbo nyeupe (white cane) mtoto Habibu Abdalla wa Chokocho Wilaya ya Micheweni mwenye tatizo la kutoona katika hafla ya kugawa vifaa mbalimbali kwa wenye uhitaji.



Mama Mariam Mwinyi akimkabidhi fimbo nyeupe Habiba Nassib Makame Gongomawe wa Wilaya ya Chakechake mwenye tatizo la kutoona.



Mariam Mwinyi akimkabidhi begi lenye vifaa vya shule mtoto Haitham Marouk Fakih.



Ismail Suleiman Ali akikabidhiwa begi lenye vifaa vya shule na mke wa Rais wa Zanzibar, Mariam Mwinyi jana. **PICHA ZOTE: IKULU**

## BURUDANI

# NANDY AWAJIBU WANAOULIZA KUNYONYESHA



MSANII Faustina Charles maarufu Nandy, amewacharukia baadhi ya mashabiki wake ambao wanataka kujua kuhusu kuonyesha mtoto wake na Billnass.

Msanii huyo katika ujumbe mrefu ambao aliuandika Instagram, alionekana kuchukia maswali kama hayo huku akiwaambia mashabiki kuacha kuchokonoa mambo ya kifamilia.


Nandy alisema kuwa si mara ya kwanza anaulizwa iwapo mtoto wake anafurahia ukaribu wake na kunyonya saa ngapi kutokana na mishe zake nyingi ambapo hajawahi onekana hata mara moja na mwanawe.

Aliwatoa wasiwasi kwa kujibu kuwa mtoto wake ana muda naye mwingi tu kila anapoenda.

"Hili suala kila nikiposti watu wanauliza mtoto yuko wapi? Mara mtoto ananyonya saa ngapi? Jamani hivi mnahisi mambo ya familia ni maigizo au nimezaa fasheni? Mtoto wangu nipo naye kila muda na anapata malezi yote kwa wazazi kama watoto wengine kwa wazazi wao," aliandika Nandy.

Aliwataka mashabiki zake kuona utofauti kati ya maisha ya uhalisia na yale ya mitandaoni huku akisema kuwa wakianza kufuatilia maisha ya mitandaoni na kufikiri ni ya uhalisia, watakuwa hata robo ya maisha yake hawajayajua.

## SIDIKA ASHEREHEKEA MIAKA 10




MWANAMITINDO Vera Sidika anasherehekea kudumu kwa miaka 10 kama mwanasosholaiti na mtu maarufu ambaye amekuwa akitajwa sana kwenye nyimbo za wasanii wa ndani na nje ya Kenya.

Sidika alikuwa akijibu swali la shabiki wake mmoja aliyetaka kujua jinsi anavyojihisi anapotajwa kwenye ngoma za wasanii na kila mtu kumzungumzia mitandaoni.

"Huwa unajihisi vipi wakati wasanii haswa kutoka Tanzania wanapokutaja kwenye mashairi yao ya ngoma," shabiki alitaka kujua.

"Kusema kweli mimi ndiye mtu maarufu kutoka Kenya ambaye ametajwa sana kwenye ngoma za wasanii. Nimekuwa maarufu kwa miaka 10 na Desemba 17 nilisherehekea miaka 10 ya kuwa maarufu," alisema Sidika.

"Hii pia ni kumbukumbu ya harusi ya wazazi wangu."

# DOGO JANJA AJIGAMBA KWA FEDHA



MSANII Dogo Janja amezua gumzo kwenye mitandao ya kijamii akisema kuwa wanyama hatari wa porini haswa Simba huwa hana haja na mtu ambaye 'amejiseti' vizuri upande wa mfuko.

Dogo Janja alikuwa katika ziara kwenye mbuga ya wanyama na mpenzi wake ambapo walipigwa picha moja wakiwa wamekaribia mti ambao chui alikuwa amejilaza.

Wawili hao walionekana wakinyata kwa mwendo kukaribia mti huo ili kuhakikisha kama kweli mnyama huyo alikuwa chui ama simba jike.

"Sisi huwaambia tafuteni fedha, simba hatafuni mtu mwenye hela," aliandika Dogo Janja kwenye Instagram.

Maneno haya yanakuja siku chache baada ya msanii Diamond Platnumz kudai kuwa alikuwa anawaza kupanda kwenye jukwaa akiandamana na mnyama aina ya simba.

Diamond ambaye alikuwa amezuru maeneo ya maandalizi ya shoo yake akimshirikisha Zuchu.

HABARI MICHEZO

# AZAM, MALINDI ZAPANIANA KOMBE LA MAPINDUZI LEO

**Saada Akida na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKATI Azam FC ikishuka Uwanja wa Amaan visiwani Zanzibar leo kuvaana na timu ya Malindi kwenye mechi ya Kombe la Mapinduzi, uongozi wa timu hiyo umesema hawataki masihara msimu huu katika ushiriki wao kwenye michuano hiyo.

Azam FC ambayo ipo Kundi A pamoja na Malindi na Jamhuri ya Pemba, imeondoka jana asubuhi kuelekea visiwani Zanzibar tayari kwa ajili ya michuano hiyo iliyoanza kutimua vumbi juzi.

Mara ya mwisho Azam FC kutwaa taji hilo ni msimu wa 2019 kwa kuifunga Simba mabao 2-1 kwenye mechi ya fainali iliyopigwa Uwanja wa Gombani, kisiwani Pemba.

Akizungumza na gazeti hili jana Kaimu Kocha Mkuu wa Azam FC, Kali Ongala, alisema baada ya kulikosa kombe hilo kwa misimu mingi sasa wameenda kivingine kuhakikisha wanaondoka na taji hilo.

Alisema baada ya kujiondoa katika mbio za ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, nguvu na akili zao wanazielekeza katika mashindano yaliyoko mbele yao ikiwamo Kombe la Mapinduzi na Shirikisho la Azam (ASFC) maarufu FA Cup.

"Kwa sasa tunatumia mashindano hayo ya Mapinduzi kufikia malengo yetu ya kutwaa taji hilo, lakini ni maandalizi ya kufanyia kazi mapungufu yetu kuelekea michuano ya Kombe la Shirikisho ambalo tuko katika hatua ya 32-bora.

"Tumejiondoa katika ubingwa wa Ligi Kuu, lakini tuna nafasi katika mashindano hayo, sasa tunahitaji kufanya vizuri katika michuano hii ya Mapinduzi na kwa sababu ya umuhimu wa mashindano hayo, tumeondoka na baadhi ya wachezaji wa kikosi cha kwanza, wengine watajiunga nasi baadaye," alisema Ongala.

Wakati Azam ikipania michuano hiyo, wapinzani wao Malindi, wamesema kasi waliyoanza nayo Kombe la Mapinduzi, wataiendeleza ili kuhakikisha timu hiyo inafanya vizuri mwaka huu.

Malindi SC juzi iliibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya timu ya Jamhuri kutokea Kisiwani Pemba, mabao yakifungwa na Mudrik Ali dakika ya 48 na Mohmed Modi dakika 59.

Akizungumza na gazeti hili Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Ali Kisaka, alisema ushindi walioupata utakuwa mwendelezo kuhakikisha wanazidisha hamasa kikosini katika mchezo ujao.

Alisema kwa sasa wanaiangalia mechi iliyoko mbele yao dhidi Azam mchezo utakaopigwa leo majira ya saa kumi alasiri.

"Mchezo wa kwanza tumemaliza kwa alama tatu, tunaenda kuzisaka alama tatu nyingine katika mechi ngumu dhidi ya Azam na matarajio yetu mechi hii tushinde,"alisema.

WAYAAA...



Beki wa Kulia wa Nottingham Forest, Serge Aurier (kushoto), akiifungia timu yake bao la kusawazisha wakati ikitoka sare ya 1-1 dhidi ya Chelsea kwenye mechi ya Ligi Kuu England iliyopigwa juzi katika Uwanja wa City Ground. **PICHA: MTANDAO**

# Banka arejeshwa Ruvu Shooting

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA kile kinachoonekana ni kutaka kukiimarisha kikosi chake ili kubakia Ligi Kuu, Klabu ya Ruvu Shooting imemrudisha mchezaji wake wa zamani Mohamed Issa 'Banka' akitokea Namungo FC.

Taarifa iliyotolewa jana na klabu hiyo imesema kuwa mchezaji huyo amerejea kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi hicho hasa sehemu ya kiungo.

"Fundi wa mpira amerejea nyumbani, mwamba huyu hapa Mo Banka," iliandika sehemu ya taarifa hiyo kwenye mtandao rasmi wa kijamii wa klabu hiyo.

Huyo ni mchezaji wa pili kusajiliwa na klabu hiyo kipindi hiki cha dirisha dogo, kwani tayari imepata saini ya straika mkongwe, Atupele Green kwa ajili ya kuongeza nguvu kwenye eneo la ushambuliaji.

Banka alikuwa kwenye kikosi hicho msimu wa 2020/21 na kukichezea msimu huo tu, akitokea Yanga timu ambayo aliichezea pia kwa msimu mmoja wa 2019/20.

Kabla ya kujiunga na Yanga, kiungo huyo alikuwa kwenye kikosi cha Mtibwa Sugar, akikipiga kwenye klabu hiyo tangu 2016 hadi 2018 ambapo alicheza kwa misimu miwili.

Ruvu Shooting haina matokeo mazuri kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu ambapo hadi kufikia raundi ya 19 inashika nafasi ya 15, nafasi moja kabla ya timu inayoburuza mkia Polisi Tanzania.

Hadi sasa Ruvu Shooting ina pointi 12, ikiwa imezidiwa jumla ya pointi tano na timu iliyo juu yake Coastal Union yenye alama 17, lakini ikiizidi pointi mbili tu timu iliyo chini, Polisi Tanzania yenye pointi 10.

Imeshinda mechi tatu, sare tatu na kupoteza 12 kama zilivyo pointi zake.

# Kipenga FA Cup Zanzibar chapulizwa

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

MICHUANO ya Kombe la ZFF (FA Cup), inatarajiwa kuanza kutimua vumbi Januari 15, mwaka huu baada ya kumalizika mashindano ya Kombe la Mapinduzi yaliyoanza juzi visiwani hapo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mwenyekiti wa Kamati ya Mashindano ya ZFF, Ali Bakari, alisema michuano hiyo itachezwa kwa kanda mbili, Unguja na Pemba.

Alisema kwa upande wa Kanda ya Unguja kutakuwa na timu 36 ambazo ni za Ligi Kuu Zanzibar na Ligi Daraja la Kwanza Kanda Unguja.

Aidha, alisema kwa upande wa timu za mikoa, Mkoa wa Mjini Magharib utatoa timu nane wakati Mkoa wa Kusini Unguja na Kaskazini Unguja, itatoa timu sita.

Kwa upande wa Kanda ya Pemba, alisema jumla ya timu 28 zitashiriki michuano hiyo ambapo timu 22 zitakuwa ni kutoka Ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Pemba na timu sita kutoka mikoa miwili ya Pemba ambapo kila mkoa utatoa timu tatu.

Alisema kwa mujibu wa kanuni za mashindano hayo msimu huu, timu za Ligi Kuu hazitaanzia hatua ya kwanza badala yake zitaanzia hatua ya pili.

"Tunaendelea na maandalizi ya michuano ya FA, kwa msimu huu tumefanya mabadiliko makubwa ya kanuni katika mashindano haya ili kupunguza changamoto nyingi,"alisema.

Bakari, alisema tayari kamati ya mashindano imetoa ratiba ya michuano hiyo kwa timu zote zinazoshiriki kinyang'anyiro hicho msimu huu, ambacho bingwa hukata tiketi ya kuiwakilisha Zanzibar kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Hata hivyo, alisema kamati inaendelea na jitahada za kutafuta mdhamini wa michuano hiyo ili kuongeza hamasa na ushindani kwa timu shiriki.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### DE JONG NA UNITED

KIUNGO wa kati wa Barcelona na Uholanzi, Frenkie de Jong, mwenye umri wa miaka 25, amebadili nia kuhusu Manchester United na anataka kujiunga nao msimu wa majira ya joto. ***(Fichajes)***

### BADIASHILE SAFI CHELSEA

KLABU ya Chelsea imefikia makubaliano na Monaco kumsajili beki wa Ufaransa, Benoit Badiashile mwenye umri wa miaka 21. ***(The Athletic)***

### DUMFRIES AGOMBEWA EPL

KLABU ya Manchester United na Chelsea huenda zikakabiliana katika kinyang'anyiro cha kumsajili beki wa Inter Milan na Uholanzi, Denzel Dumfries, 26. ***(Marco Barzaghi, via Express)***

### MUDRYK KIMEELEWEKA ARSENAL

WINGA wa Shakhtar Donetsk, Mykhailo Mudryk, mwenye umri wa miaka 21, amekubali masharti kibinafsi katika mkataba wa miaka mitano na Arsenal. ***(Sport Arena)***

### FERNANDEZ AKARIBIA CHELSEA

CHELSEA inapanga mazungumzo zaidi na Benfica kwa ajili ya kumnunua kiungo wa kati aliyeshinda Kombe la Dunia, Enzo Fernandez, mwenye umri wa miaka 21, baada ya kuanza harakati za kumtafuta mchezaji huyo wa Argentina. (Metro)

### THURAM AWANIWA UNITED

KLABU ya Manchester United inamfuatilia mshambuliaji wa Borussia Monchengladbach na Ufaransa, Marcus Thuram, mwenye umri wa miaka 25, ambaye mkataba wake utakamilika msimu wa majira ya joto. ***(Daily Mail)***

### TIELEMANS KUTUA ARSENAL

ARSENAL huenda wakafanikiwa kumsajili kiungo wa kati wa Leicester City na Ubelgiji, Youri Tielemans, mwenye umri wa miaka 25. ***(Express)***

### ELANGA AMULIKWA EVERTON

KLABU ya Everton imewasilisha ombi la kutaka kumnunua winga wa Manchester United na Sweden, Anthony Elanga, mwenye umri wa miaka 20. ***(Football Insider)***

### BALOGUN ATAJWA MILAN

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Folarin Balogun huenda akaondoka katika klabu hiyo, huku AC Milan ikionyesha nia ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, ambaye yuko kwa mkopo Reims. ***(CalcioMercato)***


### KONE AWINDWA BORUSSIA

KIUNGO wa kati wa Borussia Monchengladbach mwenye umri wa miaka 21, Kouadio Kone, ambaye analengwa na Newcastle United amewasiliana na Paris St-Germain. ***(Media Foot)***

### UNITED KUTAFUTA KIPA

KLABU ya Manchester United inaweza kutafuta mlinda mlango mpya Januari hii baada ya Newcastle United kumrudisha Martin Dubravka wa Slovakia mwenye umri wa miaka 33, kutoka katika kipindi chake cha mkopo. ***(Mirror)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SANTOS WAACHA MPANGO WA KUSTAAFISHA JEZI YA PELE

**Dhana imebadilika kidogo, sasa tutaiacha ili tuzungumze na familia baadaye...**

**SAO PAULO, Brazil**

SANTOS imeachana na mpango wa kustaafisha jezi nambari 10 ambayo Pele alivaa wakati wa maisha yake ya soka akiwa na klabu hiyo ya Brazil.

Wanachama wa klabu hiyo waligawanyika kuhusu suala hilo na kuibuka kwa video ya zamani ambapo Pele alisema ilikuwa kinyume na wazo hilo.

Katika mahojiano ya YouTube ya 2017, Pele aliripotiwa akisema: "Ni bora, labda, kuondoa namba 10 kwa sababu watu hawatawahi kusahau."

Rais wa Santos, Andres Rueda alisema punde tu baada ya kifo cha Pele kwamba kustaafisha jezi namba 10 itakuwa "sifa nzuri", akifichua kuwa itawekwa kwenye kabati la klabu hiyo.

Ripoti nyingi nchini Brazil zilisema mabinti zake Pele waliomba namba hiyo kustaafisha, lakini Santos hatachukua hatua hiyo.

Pele alishinda Kombe la Dunia mara tatu akiwa na Brazil - mnamo 1958, 1962 na 1970.

Rueda sasa amesema, kulingana na gazeti la Folha la Sao Paulo: "Kuna video ya zamani ambayo ilitufikia ambapo Pele anazungumza kuhusu nia yake ya kubakisha jezi namba 10.

"Dhana imebadilika kidogo sasa. Tutaiacha ili tuzungumze na familia baadaye, sasa si wakati wake."

Pele aliichezea Santos kuanzia mwaka 1956 hadi 1974 na klabu hiyo ilitangaza muda wa siku saba wa maombolezo kutokana na kifo chake kilichotokea Alhamisi akiwa na umri wa miaka 82.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,063,6

JACKPOT
MECHI WIKI HII
TAREHE: 03,04,05 NA 06 JANUARI 2023
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 03/01/23 | 17:00 | Umraniyespor vs Hatayspor | 2.27 | 3.28 | 3.03 |
| 02. 03/01/23 | 18:00 | Cape Town City vs SuperSport Utd | 2.41 | 3.05 | 3.05 |
| 03. 03/01/23 | 18:00 | Ismaily SC vs National Bank | 2.65 | 2.89 | 2.84 |
| 04. 03/01/23 | 23:00 | Sporting Gijon vs Rayo Vallecano | 2.68 | 3.18 | 2.58 |
| 05. 03/01/23 | 23:00 | Levante vs Getafe | 2.59 | 3.14 | 2.69 |
| 06. 04/01/23 | 17:00 | Kasimpasa vs Alanyaspor | 2.30 | 3.42 | 2.87 |
| 07. 04/01/23 | 19:00 | Panetolikos vs Atromitos | 2.26 | 3.14 | 3.19 |
| 08. 04/01/23 | 22:45 | Inter vs Napoli | 2.24 | 3.37 | 2.97 |
| 09. 04/01/23 | 22:45 | Leeds vs West Ham | 2.61 | 3.35 | 2.51 |
| 10. 04/01/23 | 23:00 | Alaves vs Valladolid | 2.84 | 3.14 | 2.47 |
| 11. 05/01/23 | 17:00 | FC Goa vs Hyderabad FC | 2.52 | 3.35 | 2.47 |
| 12. 05/01/23 | 21:00 | Leixoes vs Moreirense | 2.81 | 3.30 | 2.35 |
| 13. 06/01/23 | 14:00 | Perth Glory vs Western Sydney | 2.90 | 3.40 | 2.32 |

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CONTE: NI MIUJIZA KWA SPURS



**LONDON, England**

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte, amedai kumaliza mwaka katika nafasi ya nne bora kwenye Ligi Kuu England ilikuwa "muujiza".

Akizungumza baada ya kichapo kibaya cha mabao 2-0 Jumapili kutoka kwa Aston Villa ambacho kiliiacha Tottenham katika nafasi ya tano, pointi 13 nyuma ya vinara Arsenal, Muitaliano huyo alisema hawakutarajia hilo.

"Msimu uliopita tulifanya muujiza," alisema Conte, ambaye alichukua nafasi ya kuinoa klabu hiyo Novemba 2021.

"Kwa sababu tulicheza shindano moja tu, na tulicheza na wachezaji 12 au 13 na hawakuwa na majeraha katika mechi 15 zilizopita. Tulicheza na wachezaji wetu bora kila mechi.

"Usisahau zikiwa zimesalia mechi tatu, Arsenal walikuwa mbele yetu kwa pointi nne na kwamba tulimaliza kwa pointi 20 chini ya Manchester City na tulifanya miujiza, lakini nilijua hali hiyo."

Tottenham walizomewa Jumapili kwa kuwa hawakuweza kupiga shuti kwenye lango la Villa.

"Nakumbuka vizuri sana wakati wa kiangazi, mwanzoni, watu walizungumza juu ya Tottenham kama washindani wa taji, lakini kwa uzoefu wangu ilikuwa wazimu kusoma hii," alisema.

"Ili kuwa mshindani wa taji, kuwa timu iliyo tayari kupigana ili kushinda kitu unahitaji kuwa na msingi imara. Hiyo ina maana kuwa na wachezaji 14 au 15 wenye nguvu, ubora na wachezaji wengine vijana kuendeleza."

# Lukaku amtaka Henry kupewa ukocha Ubelgiji

**MILAN, Italia**

THIERRY Henry ndiye anafaa kuwa mtu wa kuchukua nafasi ya Roberto Martinez kama kocha mkuu wa Ubelgiji, kwa mjibu wa mshambuliaji, Romelu Lukaku.

Ubelgiji inatafuta bosi mpya baada ya Martinez kujiuzulu kutokana na kutolewa hatua ya makundi kwenye Kombe la Dunia, baada ya kukaa miaka sita na miezi minne katika nafasi hiyo.

Mshambuliaji huyo wa zamani wa Arsenal, Barcelona na Ufaransa, Henry, alijiunga naye kama msaidizi kwa misimu miwili.

Lukaku pia anasema kile kinachojulikana kama 'kizazi cha dhahabu' cha nchi yake kinastahili nafasi nyingine ya kutinga hatua hiyo kubwa, ingawa Eden Hazard tayari amestaafu soka la kimataifa.

"Kwangu mimi, Henry ndiye kocha ajaye wa Ubelgiji. Hakuna shaka. Nasema wazi: atakuwa kocha ajaye," alisema Lukaku akinukuliwa na Sky Sport ya Italia.

"Ana heshima ya wachezaji wote, ameshinda kila kitu, anajua kufundisha, anajua tunachotakiwa kufanya ili kufika huko.

"Anaijua timu, ligi, wafanyakazi. Kwangu mimi ndiye kocha bora kwa timu yetu ya taifa, basi sijui watamchukua nani. Lakini sidhani kama Ubelgiji inapaswa kuanza kutoka mwanzo.

"Hadi sasa kizazi hiki hakijashinda, lakini lazima tuendelee kujaribu kushinda, anataka kushinda na sidhani kama shirikisho litapata kocha ambaye anataka kubadilisha kila kitu na kuanza kutoka mwanzo."



605,974/-

# NAMUNGO YAANZA NA DOMAYO, BADO WA3

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Namungo FC, Denis Kitambi, amesema watafanya usajili kujaza nafasi tatu katika dirisha hili dogo ambazo ni beki, mshambuliaji na kiungo na tayari wamemsajili Frank Domayo kwa ajili ya kukiimarisha kikosi chao.

Namungo FC inayoshika nafasi ya tano kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na alama 26, imedhamiria kuimarisha kikosi chake ili kuendelea kutoa ushindani katika ligi hiyo ikilenga kuwatumia nyota hao wapya katika michuano ya Kombe la Mapinduzi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kitambi alisema hatafanya mabadiliko makubwa katika kikosi chake kwa sasa, na wamemalizana na Domayo na sasa wanaangalia nafasi zingine za kusajili.

"Tutafanya usajili wa wachezaji watatu hadi wanne, kwa nafasi hizo kwenye kiungo tayari Domayo anatosha, kazi kubwa ni kuangalia mshambuliaji na beki wenye uzoefu mkubwa watakaosaidia timu yetu kufikia malengo," alisema Kitambi.

Alisema wachezaji watakaosajiliwa anatarajia kuwatumia katika michuano ya Kombe la Mapinduzi kwa ajili ya kutengeneza muunganiko mzuri na nyota walikuwapo kikosini hapo tangu kuanza kwa msimu.

Kikosi cha Namungo FC kinatarajia kuondoka leo kuelekea Zanzibar tayari kwa michuano ya Mapinduzi, ambapo kipo Kundi D pamoja na timu ya Aigle Noir ya Burundi na Chipukizi SC.



Domayo

# SIMBA BILA CHAMA MAPINDUZI CUP

INATOKA UK. 32

kiongeza kikosi, kama unavyojua usajili ni wachezaji 30, sasa kama wakipungua hao ni lazima uongezee wachezaji wa kikosi cha vijana chini ya miaka 20, lengo letu kwenye michuano hii tunakwenda kupambana na kutoa burudani," alisema meneja huyo.

Wakati baadhi ya wachezaji wakikosekana, kikosi hicho kina baadhi ya nyota kama Pape Sakho, Sadio Kanoute na mchezaji mpya aliyesajiliwa hivi karibuni, Saido Ntibazonkiza.

Kwa upande wake, Sakho amesema michuano hii kwa kiasi kikubwa mwaka jana ndiyo iliyomfanya kuwa maarufu na kujipatia mashabiki wengi nchini, hivyo amewaahidi mashabiki kufanya vema tena.

"Tuko tayari kwa michuano, hatuna muda wa kupoteza, tunakwenda kulichukua tena. Nawaahidi mashabiki nitafanya vema zaidi msimu huu kuliko uliopita, tunacheza kwa ajili ya mashabiki kwa hiyo watuombee," alisema.

Mapema, kabla ya kikosi cha Simba kuondoka, Kaimu Ofisa Habari wa Azam FC, Hashim Ibwe, alisema safari hii hawafanyi makosa kama ya msimu uliopita.

"Tunakwenda Zanzibar hatuogopi chochote, tuko tayari kwa ajili ya haya mapambano, timu yetu iko sawa, imejiandaa, hatujabeba watoto, wala vijana, tumebeba timu ya soka ya wanaume wa Azam wale walioichapa Mbeya City mabao 6-1 ndiyo hao hao wanaokwenda Zanzibar, tunakwenda kuchukua hili kombe, ikumbukwe sisi ni mabingwa wa kihistoria wa kombe hili," alisema.

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Aggrey Morris, alisema kila mchezaji anafahamu majukumu yake, huku akiweka wazi kuwa Idris Mbombo na Issa Ndala hawajaongozana na kikosi hicho kutokana na matatizo ya kifamilia.

"Kila mchezaji anajua jukumu lake kuwa tunakwenda kwenye mashindano, wacheze mpira wasidharau, kwetu hili kombe lina umuhimu mkubwa na wanaelewa hilo. Hatukuja na Idriss Mbombo, Isa Ndala, wana matatizo ya kifamilia, lakini kwenye michuano hii tunatawatumia zaidi baadhi ya wachezaji ambao hawajatumika sana kwenye mzunguko wa kwanza wa Ligi Kuu," alisema nahodha huyo wa zamani wa kikosi hicho.

Kikosi cha Yanga nacho kilitarajia kuondoka jana jioni saa 10 kikiwa na wachezaji 24, viongozi na benchi la ufundi.

Kwenye mechi ya ufunguzi, Januari Mosi, timu ya Malindi iliichapa Jamhuri mabao 2-0.

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 07/01/23 | 18:00 | KAS Eupen vs Royal Charleroi SC | 2.65 | 3.55 | 2.44 |
| 02. 07/01/23 | 18:00 | Millwall FC vs Sheffield United | 2.90 | 3.20 | 2.43 |
| 03. 07/01/23 | 18:00 | AFC Bournemouth vs Burnley FC | 2.32 | 3.40 | 2.90 |
| 04. 07/01/23 | 18:00 | Cambridge United vs Bristol Rovers | 2.85 | 3.30 | 2.41 |
| 05. 07/01/23 | 18:00 | Morecambe FC vs Cheltenham Town | 2.50 | 3.25 | 2.75 |
| 06. 07/01/23 | 18:30 | RKC Waalwijk vs SC Heerenveen | 2.43 | 3.50 | 2.70 |
| 07. 07/01/23 | 20:30 | Brentford FC vs West Ham United | 2.65 | 3.25 | 2.65 |
| 08. 07/01/23 | 22:00 | Fortuna Sittard vs Go Ahead Eagles | 2.60 | 3.30 | 2.65 |
| 09. 07/01/23 | 22:45 | Royal Antwerp FC vs KAA Gent | 2.44 | 3.40 | 2.70 |
| 10. 07/01/23 | 23:00 | Espanyol Barcelona vs Girona FC | 2.25 | 3.30 | 3.10 |
| 11. 08/01/23 | 14:30 | US Salernitana vs Torino FC | 3.20 | 3.20 | 2.25 |
| 12. 08/01/23 | 15:30 | Bristol City vs Swansea City | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 13. 08/01/23 | 17:00 | Spezia Calcio vs US Lecce | 2.55 | 3.10 | 2.85 |
| 14. 08/01/23 | 18:00 | SV Zulte Waregem vs Yellow-Red KV Mechelen | 2.70 | 3.70 | 2.32 |
| 15. 08/01/23 | 18:30 | FC Pacos Ferreira vs GD Chaves | 2.85 | 3.25 | 2.46 |
| 16. 08/01/23 | 18:45 | Excelsior Rotterdam vs FC Groningen | 2.65 | 3.55 | 2.45 |
| 17. 08/01/23 | 19:00 | Fenerbahce Istanbul vs Galatasaray Istanbul | 2.39 | 3.50 | 2.75 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 03/01/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 4604 | Malaysia vs Singapore | 1.56 | 3.65 | 5.45 |
| 15:30 | 5262 | Vietnam vs Myanmar | 1.04 | 9.75 | 25.36 |
| 15:35 | 2849 | Al Jabalain vs Hajer Club | 1.84 | 3.20 | 4.08 |
| 15:35 | 5346 | Al Orubah vs AL Riyadh | 2.44 | 2.97 | 2.83 |
| 15:45 | 1217 | Apollon 1926 vs Panserraikos | 26.35 | 6.44 | 1.10 |
| 15:45 | 1903 | Arab Contractors vs Haras EL Hodood | 1.75 | 3.09 | 5.59 |
| 15:45 | 3315 | Ghazl EL Mahallah vs Ceramica Cleopatra | 3.14 | 2.89 | 2.44 |
| 16:00 | 1216 | Avenir S Marsa vs AS Oued Ellil | 1.81 | 3.02 | 4.58 |
| 16:00 | 1410 | ES Rades vs AS Mhamdia | 1.80 | 3.10 | 5.20 |
| 16:00 | 3650 | Ihefu FC vs KMC | 2.50 | 2.79 | 2.94 |
| 16:00 | 3792 | CO Mednine vs Avenir Sportif Gabesien | 1.89 | 2.97 | 4.28 |
| 16:00 | 4870 | CS Korba vs ES Jerba Midoun | 2.02 | 2.83 | 3.99 |
| 17:00 | 1992 | Kerala Blasters FC vs Jamshedpur | 1.84 | 3.45 | 3.74 |
| 17:00 | 3126 | Umraniyespor vs Hatayspor | 2.20 | 3.33 | 3.13 |
| 17:30 | 4535 | OFI Crete vs Volos | 2.24 | 3.23 | 3.13 |
| 18:00 | 1178 | Ittihad Tanger vs Mouloudia Oujda | 2.29 | 2.92 | 3.11 |
| 18:00 | 2703 | Bahrain Club vs Muharraq SC | 6.60 | 4.30 | 1.45 |
| 18:00 | 2830 | Cape Town City vs SuperSport Utd | 2.34 | 3.16 | 2.97 |
| 18:00 | 3865 | Levadiakos vs Panathinaikos | 10.96 | 4.48 | 1.31 |
| 18:20 | 4137 | Ohud Medina vs Al Qadisiyah | 2.77 | 2.86 | 2.57 |
| 20:00 | 3237 | Doxa Katokopia vs AEL Limassol | 3.31 | 3.31 | 2.15 |
| 20:00 | 3376 | Apoel Nicosia vs Olympiakos Nicosia | 1.25 | 5.39 | 11.98 |
| 20:00 | 3899 | Antalyaspor vs Fenerbahce | 4.08 | 3.73 | 1.78 |
| 20:00 | 5662 | Ismaily SC vs National Bank | 2.84 | 2.89 | 2.65 |
| 20:15 | 2987 | Hassania Agadir vs Difaa El Jadidi | 1.78 | 3.22 | 4.38 |
| 20:30 | 2551 | Mamelodi Sundowns vs Moroka Swallows FC | 1.41 | 4.16 | 7.73 |
| 20:30 | 4049 | Sekhukhune United vs Marumo Gallants FC | 2.35 | 2.83 | 3.32 |
| 20:30 | 4504 | Bloemfontein Celtic vs TS Galaxy FC | 1.87 | 3.27 | 4.16 |
| 20:30 | 4895 | Ironi Hasharon vs FC Ashdod | 3.60 | 3.36 | 1.91 |
| 20:45 | 3022 | Ahi Nazareth vs Maccabi Netanya | 3.70 | 3.50 | 1.84 |
| 21:00 | 1573 | FC Cartagena vs Villarreal | 4.48 | 3.73 | 1.71 |
| 21:00 | 2414 | Maccabi Tel Aviv vs Bnei Sakhnin | 1.27 | 4.75 | 9.70 |
| 21:00 | 2429 | PAS Giannina vs AEK Athens | 9.95 | 4.58 | 1.32 |
| 21:00 | 4567 | CF La Nucia vs Valencia | 7.56 | 4.78 | 1.36 |
| 21:00 | 5168 | Coca Cola vs Smouha Club | 1.80 | 3.23 | 4.77 |
| 21:00 | 5577 | Espanyol vs Celta Vigo | 2.33 | 3.20 | 3.00 |
| 22:30 | 5595 | Olympique Khouribga vs Raja Casablanca | 6.05 | 3.61 | 1.52 |
| 22:30 | 5854 | Ionikos Nikea FC vs Olympiakos | 11.85 | 5.53 | 1.23 |
| 22:45 | 3050 | Leicester vs Fulham | 2.16 | 3.50 | 3.01 |
| 22:45 | 3138 | Arsenal vs Newcastle | 1.82 | 3.56 | 3.98 |
| 22:45 | 3512 | Pontypridd Town vs Bala Town | 6.02 | 4.47 | 1.41 |
| 22:45 | 3793 | Everton vs Brighton | 3.36 | 3.32 | 2.08 |
| 22:45 | 4406 | Penybont vs Airbus UK Broughton | 1.02 | 11.69 | 27.27 |
| 22:45 | 5073 | Caernarfon Town vs The New Saints | 14.62 | 7.60 | 1.11 |
| 22:45 | 5617 | Newington YC vs Knockbreda | 1.81 | 3.75 | 3.55 |
| 23:00 | 1271 | Sporting Gijon vs Rayo Vallecano | 2.89 | 3.19 | 2.41 |
| 23:00 | 1747 | AD Ceuta vs Elche | 4.38 | 3.63 | 1.75 |
| 23:00 | 2342 | Levante vs Getafe | 2.42 | 3.18 | 2.88 |
| 23:00 | 2822 | CP Cacereno vs Real Madrid | 19.91 | 8.36 | 1.10 |
| 23:00 | 5178 | Manchester Utd vs Bournemouth | 1.28 | 5.24 | 9.03 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumanne Januari 3, 2023

Nipashe




UKURASA 29

## Santos waacha mpango wa kustaafisha jezi ya Pele

TUMEWASILI...




Miongoni mwa wachezaji wa Simba, Pape Sakho (mbele) na Sadio Kanoute, wakitua Zanzibar jana mchana tayari kwa michuano ya Kombe la Mapinduzi, ambapo leo usiku watavaana na Mlandege FC katika Uwanja wa Amaan visiwani humo. **PICHA: SIMBA**

# SIMBA BILA CHAMA MAPINDUZI CUP

## ●●●Yatamba kutwaa tena ubingwa ikianza kampeni dhidi ya Mlandege leo usiku, huku...

**Na Adam Fungamwango**

MABINGWA watetezi wa Kombe la Mapinduzi, Simba, wametua Zanzibar jana mchana bila wachezaji wake tegemeo, Clatous Chama, Mosses Phiri, na Henock Inonga, lakini wakitamba kutwaa tena ubingwa huo msimu huu.

Kikosi cha Simba kiliondoka jijini Dar es Salaam jana mchana kwa boti, muda mfupi tu baada ya Azam FC kuondoka ambao nao wametamba kuwa safari hii hawacheki na nyani kwani wakifanya hivyo wataishia kuvuna mabua.

Simba itaanza kampeni ya kutetea taji lake hilo leo saa 2:15 usiku kwa kucheza dhidi ya Mlandege FC ya Zanzibar.

Meneja wa Klabu hiyo, Patrick Rweymamu, amesema wamewaongeza baadhi ya wachezaji chini ya miaka 20 kwa ajili ya kujazia nafasi za wachezaji ambao hawakwenda kwenye michuano hiyo.

"Haya ni mashindano ya Mapinduzi, kwanza ni kuunganisha Muungano wetu, tunakwenda kuhakikisha tunafanya vizuri na kutetea ubingwa wetu.

"Wachezaji ambao wengi hawajaonekana hapa leo (jana) ni majeruhi na wanaendelea na matibabu, kuna Inonga, Banda, Phiri na wengine, kwa hiyo tume-

INAENDELEA UK. 31

## Lukaku: Henry ainoe Ubelgiji



**MILAN, Italia**

THIERRY Henry ndiye anafaa kuwa mtu wa kuchukua nafasi ya Roberto Martinez kama kocha mkuu wa Ubelgiji, kwa mujibu wa mshambuliaji, Romelu Lukaku.

Ubelgiji inatafuta bosi mpya baada ya Martinez kujiuzulu kutokana na kutolewa hatua ya makundi kwenye Kombe la Dunia, baada ya kukaa miaka sita na miezi minne katika nafasi hiyo...

UK. 30

## Azam FC, Malindi vita kali Z'bar leo



**Saada Akida na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKATI Azam FC ikishuka Uwanja wa Amaan visiwani Zanzibar leo kuvaana na timu ya Malindi kwenye mechi ya Kombe la Mapinduzi, uongozi wa timu hiyo umesema hawataki masihara msimu huu katika ushiriki wao kwenye michuano hiyo.

Azam FC ambayo ipo Kundi A pamoja na Malindi na Jamhuri ya Pemba, imeondoka jana asubuhi kuelekea visiwani Zanzibar tayari...

UK. 28

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >